# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Juni 11, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579941

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mmiliki Lucky Vincent ahukumiwa kifungo miaka minne gerezani

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM ataja sababu kumng'oa bosi TRA

**AMUASA** akishindwa majukumu mapya pia atamtema, awapa pole wateule wapya, Airtel yamwaga mabilioni Ikulu...*Endelea uk. 2*





Wafanyakazi wa Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, wakinyunyizia dawa ya kuua viruirui vya mbu wanaoeneza homa ya Dengue, katika mitaro yenye maji yaliyotuama katika eneo la Ilala Bungoni, jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Darasa la saba waitwa JKT

UKURASA 3

## PSSSF yasema malipo ya wastaafu siku 60

UKURASA 2


MICHEZO AJIBU AINYIMA USINGIZI YANGA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM ataja sababu kumng'oa bosi TRA

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametaja sababu za kumng'oa Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charles Kichere, huku akitoa pole kwa walioteuliwa kushika nyadhifa hizo.

Rais Magufuli alitaja sababu hizo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati akiwaapisha viongozi aliowateua hivi karibuni ambao ni Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, Kamishna Mkuu wa TRA, Edwin Mhede na Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Kichere.

Katika mkutano huo, Rais Magufuli alishuhudia Kampuni ya Bharti Airtel ikiikabidhi serikali gawio la Sh. bilioni tatu la miezi mitatu kuanzia Aprili pamoja na fedha binafsi iliyotolewa na mwanzilishi na Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni hiyo, Sunil Mittal, dola za kimarekani milioni moja (Sh. bilioni 2.2).

Akitaja sababu za kuwaondoa kwenye nafasi zao Kakunda na Kichere, Rais Magufuli alisema: "Tutaambizana maneno mazuri mazuri, lakini maneno mazuri hayasaidii, ukitaka maneno mazuri kaelezwe na mume wako, mke wako basi, lakini sisi tunataka matokeo mazuri basi," alisema.

Rais Magufuli alisema jukumu lake ni kuteua ili kusudi nia ya Watanzania wanayohitaji ikatimie.

"Ninapotengua mahali siyo kwamba wewe ninakuchukia, nakupenda tu na ninakupongeza mheshimiwa Joseph Kakunda kwa kuja, huku ndiko kukomaa kisiasa, hizi kazi ni muda mfupi, maisha yenyewe ni ya muda mfupi, hakuna kazi ya kudumu," alisema.

Alisema, "Lakini amejitoa amekuja, safi sana lakini ni ukweli kwenye wizara hakuisukuma ninavyotaka, ni mimi ninataka matokeo na Watanzania walionichagua wakatupigia kura wanataka kuona utekelezaji wa ilani ya uchaguzi."

"Changamoto za wafanyabiashara kwani kulikuwa na ubaya gani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Waziri mwenyewe siwangekuwa wameshapanga mikutano wa wafanyabiashara, palikuwa na dhambi gani? Nani angewakata? kwamba leo tunazungumza na wafanyabiashara wa Kanda ya Ziwa, leo Kanda ya Kaskazini, leo Kusini, nisikie shida na changamoto zao."

Rais Magufuli alisema: "Wanasema hawajawahi kumuona, hata ningeuliza hata Manyanya (Stella Manyanya, Naibu Waziri wa Viwanda) nikasema labda

INAENDELEA UK. 8

## Ofisa TRA, askari polisi kortini tuhuma za rushwa

**Na Hellen Mwango**

OFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charity Ngalawa, na askari wawili wenye vyeo vya konstebo, Ramadhani Uweza na Simon Sungu, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na shtaka la kushawishi rushwa ya Sh. milioni mbili.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Sophia Gura, alidai kuwa Oktoba 29, 2016 katika maeneo ya Kimara Mwisho, jijini Dar es Salaam, walishawishi rushwa ya Sh. milioni mbili.

Gura alidai kuwa washtakiwa walishawishi rushwa kutoka kwa mfanyabiashara Ramadhani Ntunzwe kwamba mali yake imefanyiwa makisio ya chini ya malipo ya kodi.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walidai kuwa mali hiyo imefanyiwa makisio ya chini tofauti na thamani yake. Washtakiwa walikana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu aliwataka washtakiwa kuwa na mdhamini mmoja kila mmoja atakayetia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano.

Washtakiwa walitimiza masharti na wako nje kwa dhamana na kesi itatajwa Julai 10, mwaka huu.



Meneja Kiongozi Uhusiano na Elimu kwa Umma wa PSSSF, Eunice Chiume (wa tatu kushoto), akizungumza na wahariri na waandishi wa habari waandamizi wa kampuni ya The Guardian Ltd, kuhusu changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wastaafu, alipotembelea ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# PSSSF: Siku 60 mstaafu kulipwa mafao

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umesema wanachama walio hakiki taarifa zao kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii 2018 wanaendelea kulipwa mafao yao ya kustaafu bila kupata usumbufu.

Kwa mujibu wa sheria, mstaafu anatakiwa kulipwa mafao yake ndani ya siku 60 baada ya kustaafu kazi na iwapo kutakuwa na ucheleweshwaji wowote aliyechelewesha atatakiwa kulipa faini.

Akizungumza jana na uongozi wa kampuni ya The Guardian Ltd, katika ziara maalum, Meneja Kiongozi Uhusiano na Elimu kwa Umma wa PSSSF, Eunice Chiume, alisema mstaafu yeyote aliyehakikiwa analipwa mafao yake kila mwezi.

Alisema kila mwaka uhakiki unafanyika ili kusafisha daftari ni kuwa na idadi sahihi ya wanaostahili kulipwa mafao, kwa kuwa wapo wanaofariki na wanatakiwa kulipwa wategemezi na bila kufanya hivyo ni kuendelea kulipa wasiostahili.

Alisema kwa mwaka huu muda wa uhakiki ulifanyika mwezi Januari hadi Machi.

"Kila mwaka ni lazima tufanye uhakiki ili kupata idadi sahihi ya wanaostahili kulipwa, tusipofanya hivyo watalipwa wasiostahili na wapo wanaojaribu kufanya mambo yasiyofaa. Wazee au wagonjwa wanaoshindwa kufika kwenye ofisi zetu kuhakiki tunawafuata hadi nyumbani kuwahakiki, lengo letu kila mmoja apate haki yake," alisema.

Chiume alisema PSSSF ina wastaafu 124,000 na kwamba wapo ambao majina yao yalirukwa na mfumo na wamesharejeshwa na wengine walikuwa hawajahakiki, na kwamba kila ambaye taarifa zake ziko vizuri anastahili kulipwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema wanachama 227 walisitishwa kulipwa mafao kutokana na uhakiki.

Alisema kuna changamoto za ulipaji wa mafao ambazo nyingine ni kutokana na wanachama kutokuwa na taarifa sahihi au viambatanisho kutokamilika ikiwamo vyeti vya kidato cha nne.

Kwa mujibu wa Chiume, tangu kuanza kwa PSSSF Agosti mwaka jana, wamefungua ofisi za mikoa 29 ambazo zinalipa mafao hadi Sh. milioni 20 na kuondoa usumbufu kwa wanachama kwenda makao makuu.

Alisema wenye malipo ya zaidi ya Sh. milioni 20 ndiyo wanaopaswa kwenda makao makuu.

"Kabla ya kujenga mfumo utaratibu ulikuwa kila kitu kinafanyika makao makuu, kwa sasa tumejenga mifuko kwenye ofisi zetu mikoani zinafanyakazi muda wote kuhudumia wanachama," alisema.

**UTAPELI**

Alitahadharisha wastaafu kuhusu kuwapo kwa matapeli wanaokwenda kwenye ofisi za PSSSF na kupiga picha majina kitabu cha wageni na baadaye kuwapigia wastaafu kuwa suala lao linashughulikiwa na lipo katika hatua nzuri na kuwataka wawape pesa ili waweze kulisukuma haraka.

Alitoa mfano wa mzee ambaye alitapeliwa kwa kuambiwa atoe Sh. 500,000 kama namna ya kusaidiwa.

"Hivi karibuni kuna mzee alikuwa anafuatilia mafao yake, alijitokeza mtu alichukua namba akampigia simu na kuahidi kumsaidia kwa masharti ya kutoa Sh. 500,000, alitoa fedha alipokuja kwetu tulimweleza hakuna uta ratibu wa kutoa fedha kwa kuwa huduma ni bure," alisema.

Alisema kuna changamoto ya uelewa kwa wastaafu wengi kuhusu utaratibu wa malipo ya mafao yao na ili kuondoa tatizo hilo PSSSF imeingia makubaliano na CRDB kwa ajili ya kutoa elimu hiyo na kila wakati kuna mafunzo ya kuwafundisha wastaafu mambo mbalimbali.

INAENDELEA UK. 3

## HABARI KITAIFA

# Spika awashangaa wabunge kuwekeza kwenye bodaboda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametoa wito kwa wabunge kuwekeza kwenye sekta ya elimu badala ya magari aina ya Noah au pikipiki, akieleza kuwa wanamtia aibu.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni jana alipokuwa akitangaza wageni wa Mbunge wa Bukoba Vijijini, Jasson Rweikiza (CCM), ambao ni wanafunzi waliofanya vizuri kidato cha nne na darasa la saba mwaka 2018.

Wanafunzi waliotambulishwa ni waliomaliza kidato cha nne mwaka 2018 katika Shule ya Sekondari Sunshine na kupata ufaulu wa daraja la kwanza na pili.

"Pia kuna wanafunzi 59 waliomaliza darasa la saba mwaka 2018 kutoka Shule ya Msingi ya Anne Marie Academy ya jijini Dar es Salaam, kwenye wilaya, hii shule ya ilikuwa ya kwanza na kimkoa ilikuwa ya kwanza na kitaifa ilikuwa ya sita," alisema.

Kutokana na ufaulu huyo, Spika Ndugai alimpongeza Rweikiza ambaye ni mmiliki wa Shule ya Anne Marie kwa kuimarisha elimu.

"Haya ndo mambo ambayo wabunge tunatakiwa tufanye, siyo mbunge unamiliki Noah, unamtia aibu Spika, kila siku unaonekana trafiki huko, mbunge unamiliki bodaboda!

"Tuvuke jamani, bodaboda zikikamatwa, unampigia Spika, Spika bodaboda zangu zimekamatwa huku," Ndugai alisema na kuibua vicheko bungeni.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa rai kwa watunga sheria hao kuwekeza kwenye mambo makubwa, akisema wanapaswa "kuvuka kidogo kwenye uwekezaji".

Nje ya Ukumbi wa Bunge, Mkuu wa Shule ya Msingi, St. Anne Marie, Gladius Ndyetabura, alisema wanafunzi 59 wa shule hiyo waliofanya mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka jana, walipata wastani wa alama A na kuiwezesha kushika nafasi ya sita kitaifa na ya kwanza Mkoa wa Dar es Salaam.

Ndyetabura alisema imekuwa kawaida kwa shule hiyo kuwapa motisha wanafunzi wa shule hizo na ndiyo sababu shule imekuwa ikipata matokeo mazuri kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa.

Alisema mbali na kufanya ziara bungeni, wanatarajia kuanza kuwapeleka Dubai, Uingereza na Marekani wanafunzi watakaokuwa wanafanya vizuri kwenye mitihani yao ili iwe chachu kwa wengine kufanya vyema zaidi.

"Shule imejiwekea utaratibu wa kuwapa motisha wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi na huwa tuna kawaida ya kuwapeleka mbuga za wanyama kama Serengeti, Mikumi, Ngorongoro... tutaanza kuwapeleka Ulaya," alisema.



Rais John Magufuli pamoja na mkewe Mama Janeth Magufuli wakimwombea mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere anayepatiwa matibabu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU.**

# Mmiliki wa Lucky Vincent ahukumiwa jela miaka 4

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imemhukumu mmiliki wa Shule ya Lucky Vincent, Inocent Mosha, kwenda jela miaka minne au kulipa faini Sh. milioni 4.5 baada ya kutiwa hatiani kwa makosa manne.

INAENDELEA UK. 8

# Mwanafunzi ashikiliwa kwa tuhuma za mauaji

**Na Futuna Seleman,** PWANI

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia mwanafunzi wa sekondari mwenye umri wa miaka 14 kwa tuhuma za kumuua mkulima Rashid Said (17) kwa kumpiga jiwe lililomjeruhi eneo la kisogoni na kumsababishia umauti.

Katika taarifa yake aliyoitoa kwa vyombo vya habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, ACP Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo limetokea Kibaha Picha ya Ndege, majira ya saa 11:30 jioni Juni 7, chanzo kikiwa ni ugomvi baina ya marehemu na mtuhumiwa.

Alisema kabla ya umauti kumfika, Saidi alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Tumbi kwa matibabu, lakini alifariki dunia Juni 8, wakati akiendelea na matibabu hayo majira ya saa 9:50 alasiri.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda Wankyo alisema chanzo kilikuwa mtuhumiwa wakati anarejea nyumbani kwao alikutana na vijana wenzake akiwamo marehemu Said ambao wanadaiwa kumzuia na Saidi anadaiwa kuanza kumtukana mtuhumiwa.

"Mtuhumiwa alianza jitihada za kukimbia, lakini kabla hajafika mbali Said alimrushia jiwe lililompiga ubavu wa kulia, hivyo kumfanya mtuhumiwa kumrushia jiwe Said lililompata kichwani maeneo ya upande wa kulia kisogoni," alisema kamanda katika taarifa yake.

"Baada ya tukio hilo Saidi alipelekwa katika Hospitali ya Rufani Tumbi wakati anaendelea na matibabu alifariki,"

Kamanda Wankyo alitoa wito kwa jamii kutojichukulia sheria mkononi kwa kuwa kuna viongozi wa familia, vijiji, kata ambako wanapaswa kuripoti ama polisi ili hatua zaidi zichukuliwe kuliko kufanya uamuzi unaoweza kuwagharimu," alisema. mwisho.

# PSSSF: Siku 60 mstaafu kulipwa mafao

INATOKA UK 2

"Kuna watu wamekaa kazi yao ni kutafuta namba za wastaafu na kuwapigia simu kuwasumbua, wanawapa ahadi mbalimbali na wanajitambulisha ni wafanyakazi PSSSF, tunashirikiana na vyombo vya dola kukabiliana nao," alisema.

**MALIPO**

Kuhusu malipo, alisema PSSSF imelipa Sh. bilioni 800 kwa wastaafu na Sh. bilioni 119 zililipwa kuanzia Februari mwaka huu, ikiwa ni ya tofauti ya kikokotoo kabla ya maelekezo ya Rais ya kubadili kikokotoo.

Kuhusu wastaafu kulipwa ndani ya siku 60, alisema kuna changamoto kubwa ya wastaafu kwenda kudai mafao siku chache baada ya kustaafu, wakati kwa mujibu wa sheria ni siku 60.

"Kwa mfano mtu akistaafu mwezi Juni atalipwa mafao yake Agosti mwaka huu, kukiwa na ucheleweshaji wowote mtumishi aliyecheleweshwa atatozwa faini, kwa sababu hakuna mtu anayekubali kutozwa faini, kuna uwajibikaji mkubwa," alibainisha.




# Takukuru yaanza uchunguzi madai ya rushwa tumbaku

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli dhidi ya watumishi waliotuhumiwa na unyanyasaji na madai ya rushwa kwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Tumbaku cha mkoani Morogoro.

Watumishi hao ni pamoja na askari polisi katika mkoa huo wa Morogoro ambao wanatuhumiwa kwa hongo dhidi ya wafanyakazi wa kiwanda hicho.

Takukuru wanachukua hatua hiyo, ikiwa ni utekelezaji wa agizo hilo la Rais Magufuli alilolitoa Ikulu Ijumaa iliyopita katika kikao na wafanyabiashara.

Rais Magufuli aliitaka Takukuru kufanya uchunguzi na kuchukua hatua za haraka baada ya mmoja wa wawakilishi wa wafanyabiashara Mkoa wa Morogoro kudai kuna mpango wa kufungwa kiwanda hicho, huku miongoni mwa sababu zikidaiwa kuwa ni kutokana na kudaiwa kusumbuliwa na baadhi ya askari.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwenye vyombo vya habari jana, tayari Takukuru makao makuu imeongezea nguvu timu ya uchunguzi mkoani humo ambayo ilikuwa imeshaanza kazi hiyo ya uchunguzi.

"Kufuatia tuhuma za unyanyasaji pamoja na madai ya hongo yanayodaiwa kufanywa na askari polisi mkoani Morogoro dhidi ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Tumbaku, tayari Takukuru makao makuu imeongezea nguvu timu ya uchunguzi mkoani humo ambayo ilikuwa imeshaanza kazi chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Morogoro," ilisema taarifa hiyo iliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Diwan Athumani.



Ofisa Kodi Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charity Ngalawa (wa pili kushoto) na makonstebo wawili wa polisi, Ramadhani Uweza (katikati), Simon Sungu (wa pili kulia), wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, na kusomewa mashtaka ya kushawishi rushwa ya Sh. milioni mbili. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Mfumuko wa bei waongezeka

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MFUMUKO wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.5 kutoka asilimia 3.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Mkurugenzi wa shughuli za kitakwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Irenius Ruyobya, alisema kuwa hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 imeongezeka ikilinganishwa na iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Aprili, 2019.

"Kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi cha mwaka ulioishia Mei, 2019 zikilinganishwa na bei za mwaka ulioishia mwezi Mei, 2018," alisema.

Aidha, alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 ni pamoja na unga wa mahindi kwa asilimia 2.8, nyama kwa asilimia 4.7, samaki kwa asilimia 13.5, matunda kwa asilimia 15.3, viazi kwa asilimia 21.7 na mihogo mibichi kwa asilimia 24.8.

Alifafanua kuwa kwa upande wa baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa taifa ni pamoja na mavazi na viatu kwa asilimia 3.7, mkaa kwa asilimia 13.1, vyombo vya jikoni kwa asilimia 2.5, gharama za kumuona daktari hospitali za binafsi kwa asilimia 6.4, dizeli kwa asilimia 11.1 na petroli kwa asilimia 4.2.

Pia alisema kuwa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 umeongezeka hdi asilimia 2.2 kutoka asilimia 0.9 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019.

Akizungumzia hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, alisema kuwa nchini Uganda, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 umepungua hadi asilimia 3.3 kutoka 3.5 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019.

"Kwa upande wa Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2019 umepungua hadi asilimia 5.49 kutoka asilimia 6.58 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019," alisema.

# Shahidi adai malipo Dola 902,981 TFF hayakuwa na nyaraka

**Na Hellen Mwango**

ALIYEKUWA Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Richard Magongo, amedai mahakamani kwamba ripoti ya ukaguzi wa ndani ilionyesha matumizi ya Dola za Marekani 902,981.98 kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kumlipa deni Rais wake wa zamani, Jamali Malinzi na wenzake kwa nyakati tofauti.

Kadhalika, amedai kuwa malipo hayo hayakuwa na nyaraka za kuthibitisha jinsi gani Malinzi aliikopesha TFF na badala yake zilikuwapo nyaraka za bosi huyo wa zamani kulipwa mkopo huo.

Ushahidi huo ulisikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde katika kesi ya kutakatisha Dola za Marekani 173,335 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi ya Malinzi na wenzake wanne.

Magongo (43), ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Benki ya Barclays alitoa ushahidi wake wakati akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai.

"Nyaraka za matumizi na mkopo kutoka kwa Malinzi kwenda akaunti ya TFF hazikuwapo kama mkataba wa TBL na shirikisho hilo, hivyo kulikuwa na upungufu wa kiutawala kutoka TFF katika utekelezaji wa mkataba wao," alidai shahidi.

Alidai kuwa nyaraka zilizokosekana katika ukaguzi wake ni malipo ya mkopo kutoka TFF kwenda kwa Malinzi hayakuwa na uthibitisho wa kulipwa na shirikisho hilo. Aidha, shahidi alidai kuwa katika ripoti hiyo hakuna mkataba wa ukopeshaji huo au risiti za kuonyesha TFF imeingiziwa mkopo huo.

Alidai kuwa TBL iliingia mkataba na TFF Mei 12, 2012 wa kuidhamini Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) wa miaka mitano.

"Katika mkataba huo tulikubaliana kila robo ya mwaka TFF ilipwe Dola za Marekani milioni mbili na kwamba kwa mwaka mzima Dola milioni 10," alidai na kuongeza.

"Mheshimiwa hakimu masharti udhamini huo, TBL ilitaka kila robo mwaka kabla ya kulipwa fedha nyingine TFF iwasilishe mahesabu ya kuthibitisha matumizi yake," alidai Magongo.

Hata hivyo, katika ukaguzi wake ulianza 2013 mpaka 2017.

Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Juni 20, mwaka huu.

# ACT yampa Maalim Seif kazi maalum

**Na Enock Charles**

KAMATI Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, imemteua mwanachama namba moja wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, kuwa mshauri mkuu wa chama.

Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mwenezi wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema nafasi hiyo ambayo awali ilikuwa ikishikiliwa na Prof. Kitila Mkumbo.

"Kama mnavyofahamu, Maalim Seif ni mwanasiasa mkongwe katika siasa za Tanzania, hivyo Kamati Kuu imemteua kuwa mshauri mkuu wa chama," Ado alisema.

Kamati Kuu hiyo pia imemteua aliyewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Nassoro Mazrui, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Miradi.

Mbali na mkongwe huyo wa siasa, wengine walioteuliwa ni Salim Bimani, ambaye anakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Itikadi, Mawasiliano na Uenezi, Joram Bashange aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kampeni na Uchaguzi na Ismail Jusa kuwa Mwenyekiti wa Kamati Usimamizi na Ufuatiliaji.

Wateule wengine ambao ni wajumbe wa Kamati Kuu ni Theopista Kumwenda, Mwajabu Dhahabu, Fatma Fereji na Eddy Riyami. Nafasi za ukatibu

INAENDELEA UK.8

## PM mgeni rasmi kongamano la kiuchumi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la nne la kuwawezesha wananchi kiuchumi litakalofanywa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), jijini Dodoma.

Katibu wa Baraza hilo, Beng'I Issa, alieleza jana kuwa kongamano hilo litahudhuriwa na washiriki zaidi ya 350 kutoka taasisi za serikali, halmashauri na wilaya.

"Juni 15 tutafanya kongamano hilo, ambapo tutapata mrejesho kutoka mifuko ya serikali namna ilivyokusanya madeni, kuboresha mazingira ya wafanyabiashara, pamoja na namna mikoa na halmashauri nchini zilivyotenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda," alisema Issa.

Alisema kaulimbiu ya kongamano hilo inakwenda sambamba ya serikali ya ujenzi wa viwanda ambayo ni 'kuwezesha wananchi kujenga viwanda'.


Meneja Uhusiano wa serikali na umma kutoka benki ya NBC, Willium Kallage ambaye ni Meneja Uhusiano wa serikali na umma kutoka benki ya NBC, ambayo ni mojawapo ya wadhamini wa kongamano hilo, alisema wametenga Sh. milioni 54 katika kulipa nguvu kongamano hilo.

Alisema kwa sasa NBC wanajitanua kwa kuwapa mitaji wajasiriamali wadogo ambao ndiyo chachu ya maendeleo nchini.

"Tunashiriki mwaka wa pili sasa kwenye majukumu ya kiuchumi na kudhamini NEEC, lakini kwa sasa tumejikita katika kuwajengea mfumo wa elimu wajasiriamali wadogo kuhusu biashara na matumizi ya fedha," alisema Kallage.

Naye Alex Bitekeye ambaye ni Ofisa Uhusiano wa Vodacom ambao ni moja ya wadhamini wa kongamano hilo, alisema nchi haiwezi kuwa na viwanda kama hakuna mawasiliano ya uhakika.

Alisema Vodacom itashirikiana katika kufikia Tanzania ya viwanda kwa kuhakikisha mawasiliano ya simu yanapatikana nchini kote.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mafanikio yapo kwenye uadilifu

**TUNAWAPONGEZA** Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Nhende na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, kwa kupewa dhamana hizo za kuwatumikia Watanzania.

Wosia wetu kwenu ni kuwa na uadilifu na kusimamia kwa bidii zote watumishi ili wawe waadilifu.

Tunatoa wosia wa uadilifu kwa kuwa ndiyo msingi mkuu wa uongozi. Uadilifu ambao ndani yake kuna uaminifu mkubwa, uzalendo, hekima na hofu ya Mungu, ndiyo mambo yakuambatana nayo katika kufanyakazi.

Uadilifu tunaouzungumzia unamaanisha kusema na kuishi ukweli hata kama kufanya hivyo kutawaumiza.

Tunapenda kuwaambia kuwa mnasimamia taasisi nyeti za serikali, hivyo ni vyema kuwa waaminifu kulinda maslahi ya nchi kuliko kuhadaa na kudanganya ili kumnufaisha asiye na haki wala maslahi na taifa.

Tunawakumbusha kuwa hakuna kufanikiwa kwa mipango yoyote kama hakuna uadilifu. Mikakati ya kuondoa umaskini, kufikia Tanzania ya viwanda na yenye uchumi imara haitakamilika kama hakuna viongozi waadilifu.

Kama viongozi wa wizara nyeti yenye kushughulikia vitega uchumi, uwekezaji na biashara na kukuza uchumi wa nchi kwa upande wa Bashungwa na taasisi muhimu ya kusimamia mapato ya taifa ya TRA simamieni kila mnachokiamini ili mambo yafanyike kwa uadilifu, uzalendo na hofu ya Mungu.

Tunajifunza kuwa uadilifu na uzalendo, ndiyo unayoyafanya mataifa ya wenzetu hasa ya Asia kwa mfano Japan na China kuendelea kwa viwango vikubwa kwenye sekta zote, kung'ara kwenye sayansi na teknolojia kutokana na uchapaji kazi wa hali ya juu.

Tunajifunza kuwa Japan inasifika kwa falsafa yake ya Samurai, ambayo inahamasisha jitihada katika kazi, heshima na kuthaminiana, ushindani, uzalendo na uadilifu mkubwa yote hayo yameliwezesha taifa hilo kuwa la mfano.

Ni nchi iliyoendelea na inayoheshimika tena ni ya mfano kwenye uchapaji kazi na mafanikio kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia.

Inasifika kwenye utengenezaji magari ya kila aina na mitambo ya kila aina, inaunda vifaa vya usafiri kwa teknolojia ya kisasa zikiwamo meli.

Si Wajapani pekee hata Wachina wanajulikana duniani kwenye uchapaji kazi, kujituma, utiifu, uadilifu, heshima na uzalendo kupitia falsafa ya Confucius.

Mataifa hayo yana maendeleo na yanajitahidi kuongeza ushindani na ufanyakazi kwa bidii na kujiepusha na kutekwa na hisia za ufisadi.

Maeneo mnayoyaongoza ni kama moyo wa taifa kama Rais John Magufuli, alivyowaagiza simamieni utendaji kazi.

Ondoeni kulindani, kubebana na kulea mafisadi wanaokwamisha maendeleo ya taifa.

Dokta Nhede, kama ambavyo umepewa rungu na Rais kwa kusisitiza kuongeza mapato na kusimamia utendaji kazi wenye tija ili kukusanya kodi, huku ukilinda vyanzo vya kodi, usikubali kurubuniwa na wachache ambao wanaifanya mamlaka hiyo kuonekana kama eneo la mafisadi.

Mara nyingi katika vikao vya Rais na wafanyabiashara TRA imekuwa ni eneo linalolalamikiwa mno.

Ni wakati wa kushirikisha wadau na kufanya utafiti ili kufahamu chanzo cha tatizo, namna ya kulirekebisha na mbinu za kutumia ili kurudisha heshima kwa taasisi hiyo.

Tunapomtakia Bashungwa kazi njema ya kuiongoza Wizara ya Viwanda na Biashara, tunamshauri kushirikisha wadau na kufanya tafiti zitakazosaidia kujua chanzo cha udhaifu na namna ya kuurekebisha.

Tunawakumbusha tena kuishi na kuuendeleza uzalendo na uadilifu ili mfanikiwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Sasa zamu iwe ya wakulima kuwa na mkutano na Rais

Na Raphael Kibiriti

**BAADA** ya tija ya mikutano miwili aliyoifanya Rais John Magufuli na sehemu ya makundi ya Watanzania yaliyo na mchango kwenye uchumi wa nchi, nimeshawishika kumsihi aendeleze utaratibu huo.

Ninasema hivyo kwa sababu kwa maoni yangu mikutano hiyo imempa alichokitaka na imemuwezesha kuchukua maamuzi ambayo yanasaidia sekta zinazohusika kufanya vizuri zaidi.

Januari mwaka huu, Rais Magufuli alikutana na wachimbaji, wafanyabiashara na wadau wa sekta ya madini katika mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam ili kusikiliza kero zao.

Si kero tu pia ushauri wa nini kifanyike ili wao na taifa lifaidike na madini yaliyoko nchini.

Inashangaza kwa hali ilivyo kwamba Ripoti ya Benki ya Dunia (WB) inaonyesha kutoitambua Tanzania kwa kuuza madini hata katika eneo la Afrika Mashariki pamoja na kumiliki utajiri mkubwa wa rasilimali hiyo kuliko nchi zingine za eneo hili.

Na ndiyo maana aliwataka wadau hao kueleza kero zote zinazosababisha hali hiyo na ushauri wao ambao ungehakikisha vikwazo vilivyomo katika mnyororo wa biashara ya madini vinaondolewa.

Wadau wakataja sababu za madini kuibiwa kwamba ni utitiri wa kodi kuanzia kwa mchimbaji hadi mfanyabiashara wa madini.

Na mmoja wa washiriki wa mkutano huo akatoa mfano kwamba mchimbaji akitaka kuuza dhahabu kwa mfano, alikumbana na tozo ya service levy ya asilimia 0.3, mrahaba asilimia 6, ukaguzi asilimia moja na ada ya clearance.

Kwamba hiyo ilikuwa mbali na kodi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambapo zikijumlishwa zilikuwa zinamfanya mchimbaji kulipa kodi ya jumla ya asilimia 12.3.

Kwa wafuatiliaji wanajua matunda ya mkutano huo kwamba ni pamoja na baadhi ya kodi zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara na wachimbaji hususani wadogo zimefutwa.

Hizo ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Zuio ya asilimia tano inayotozwa kwenye bei ya kuuzia madini ya aina zote.

Aidha, masoko ya madini katika mikoa mbalimbali nchini yameanzishwa na taarifa za awali zinaonyesha kuwa mambo yanakwenda vizuri.

Ikumbukwe kwamba ufanisi katika sekta ya madini una tija kwa Watanzania wengi, kwani taarifa za Shirikisho la Vyama vya Uchimbaji Madini Tanzania (Femata), zinaonyesha kwamba watu milioni sita wanashughulika na sekta hiyo nchini.

Mkutano mwingine ulioacha mshindo ni ule uliofanyika wiki iliyopita Juni 7, jijini Dar es Salaam kati ya Rais Magufuli na wawakilishi wa wafanyabiashara kutoka wilaya 139 nchini na wajumbe wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC).

Mengi yalielezwa na wafanyabiashara, hasa wakilalamikia tozo na kodi zisizo rafiki, lakini baadhi ya maofisa wa TRA wanaodai rushwa kutoka kwa wafanyabiashara.

Rais Magufuli naye alieleza dosari ya wafanyabiashara ikiwamo mbinu wanazotumia kukwepa kulipa kodi ya serikali kwa kutengeneza vitabu viwili vya mahesabu, kimoja kikibeba takwimu za uongo na kingine za ukweli.

Japokuwa matunda ya mkutano huyo ndiyo yanaanza kuonekana likiwamo la mabadiliko madogo katika baraza la mawaziri na TRA, Muungwana anatarajia tija kubwa zaidi ya mkutano huo.

Ni kwa msingi huo, Muungwana ana maoni kwa Rais kuwa na mkutano wa aina hiyo na wakulima nchini, kundi ambalo linachukua asilimia 70 ya Watanzania wote.

Kwamba iwapo mkutano kama huo utafanyika, Rais atapata changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wakulima wa pamba, korosho, kahawa, tumbaku, chai, mahindi, mpunga, iliki, karanga na mengineo kutoka katika midomo ya wahusika.

Kimsingi bado kuna yanayopaswa kufanywa kwa kundi hili ambalo ni muhimu katika suala zima la kupambana na umaskini, ili kuifikia Tanzania ya viwanda na kipato cha kati 2025.

Muungwana anaona mkutano kama huo utakuwa na tija zaidi katika sekta ya kilimo, ikichukuliwa kuwa maamuzi aliyofanya Rais Magufuli baada ya mikutano hiyo miwili ya inazidi kuleta manufaa kwa nchi.

# BARUA/MJADALA

## *Uchafuzi huu Tandale haukubaliki*

**Mhariri habari**

NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lililo na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.

Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisadia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.

Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.

Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.

Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.

**Muathirika-Tandale**

## *Walezi tusifuge tabia zisizokubalika*

Mhariri

KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao kwa kiasi kikubwa hawako tayari kusikiliza ushauri wanaopewa na majirani zao juu ya tabia za watoto wao.

Katika mtaa ninaoishi hapa Mbalizi mkoani Mbeya, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya wastaarabu na hata katika mwenendo wa kawaida wa maisha ya watu.

Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu.

Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.

Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.

Kwamba wanaoenda kulalamika kwao wanamuonea gere kijana wao kutokana na maendeleo anayoyafanya.

Naomba serikali ya mtaa wetu ichukue hatua ya kumkanya kijana huyo ili aachane na tabia hiyo kwani inaweza ikamhatarishia maisha yake siku moja na hasa pale wananchi watakapojichukulia sheria mkononi

**Jason Mandyanga- Mbalizi**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Maji haya ya mvua yaanze kutunufaisha



**Na Gaudensia Mngumi**

KWA wakazi wa Dar es Salaam na ukanda wa mzima wa pwani kinachoonekana sasa ni upepo ambao licha ya kuleta magonjwa, kama vikohozi na matatizo ya macho, kwa upande mwingine hutishia maisha kwa kuvunja miti na kuezua mapaa.

Habari mbaya inayoambatana na upepo huo ni kukausha maji kwenye vyanzo mbalimbali, kukausha ardhi na mazao pia. Upepo huo unatokea huo unaanza kuvuruga hali ya hewa, wiki tatu baada ya mvua kubwa kunyesha sehemu mbalimbali nchini.

Ni jambo la kusikitisha kuwa baada ya mvua kujaza madimbwi, mito, mikondo ya maji, maziwa na vyanzo mbalimbali kwa mwezi mzima wa tano, kinachojiri sasa ni ukame na ukosefu wa maji kwenye baadhi ya mikoa utakapovuma na wananchi wengi kuendelea kuteseka. Wataendelea kutegemea maji ya madimbwi, visima vifupi na hata kunywa maji ya chumvi.

Ukipita maeneo mengi ya Dar es Salaam na mikoa ya pwani na mikoa yenye upepo, utakubaliana na wataalamu kuwa muda huu haukuwa wa kuhangaika na maji kwani wananchi walitakiwa kufunzwa namna ya kuvuna maji ya mvua ambayo sasa yangekuwa yanatumika.

Kwa jinsi jitihada zinavyofanyika kusaidia kupata maji kutoka vyanzo mbalimbali, taifa halina budi kuanza mpango kabambe wa kujenga miundombinu ya kukusanya maji ya mvua na kuweka akiba ya maji hayo, yatakayotumika kwa muda mrefu.

Jitihada zinazofanywa kuwa na akiba ya chakula , ni vyema pia kuwa na akiba ya maji . Kwa kila kijiji, wilaya na mikoa. Chanzo cha akiba hiyo ni maji ya mvua.

Kwa jinsi ambavyo taifa linajitahidi kujenga miundombinu ya usafiri, shule na hospitali ni wakati pia wa kuanza kuweka mikakati ya kujenga miundombinu ya kuhifadhi maji ya mvua ambayo ni jambo la kuhuzunisha kuwa karibu yote hupotea na kuacha nchi na wakati kama yangevunwa watu wasingekuwa na shida ya maji.

Kama ambavyo juhudi zinafanywa kufikisha mawasiliano ya simu mijini na vijijini , kadhalika kuwafikishia wananchi umeme wa jua na wa gridi ya taifa , vivyo hivyo kuna haja ya kuandaa mikakati ili kuwawezesha kuvuna maji ya mvua.

**FAIDA ZAKE**

Maji ya mvua hayana gharama yanaanguka juu ya mapaa hivyo ni rahisi kuyakusanya kwani hayatumii nguvu wala mbinu za kitaalamu au za kiuhandisi. Ni salama kwa vile hayana magonjwa, uchafu wala vimelea kama vile ambavyo vinapatikana kutoka kwenye maji ya ardhini.

Kwa upande wa mazingira maji ya mvua ni muhimu kwenye kupunguza uwezekano wa mafuriko unaoumiza wananchi wengi mijini na vijijini.

Ikumbukwe kila mwaka Juni 9, ni Siku ya Mazingira Duniani , taifa linapoadhimisha siku ya mazingira duniani ni vyema pia kuangalia jinsi kama nchi inavyoweza kunufaika na kuvuna maji ya mvua yanayotiririka pembeni ya barabara, kwenye mito, mabondeni na kwenye mikondo ili kutunza mazingira.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka jijini Dar es Salaam (DAWASA) inastahili pongezi kwa kujenga mradi wa bwawa la Kidunda mkoani Morogoro ambao pamoja na mambo mengi utahifadhi akiba kubwa ya maji ya mvua yatakayotumika jijini Dar es Salaam na mkoa na miji ya Bagamoyo, Mlandizi na Kibaha. Hili ni jambo linaloweza kuigwa na mamlaka nyingine zikiwamo za mabonde.

Kwa mfano Mamlaka za Kuendeleza Mabonde la Mto Rufiji Bonde la Mto Pangani, Wami -Ruvu, Bonde la Ziwa Victoria, Mto Ruvuma na Ziwa Tanganyika kujaribu uwekezaji kwenye kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ili kusaidia kupunguza matatizo ya maji.

Ni dhahiri kuwa huenda kama maji ya mvua yangevunwa kwenye mabonde mbalimbali miji inayotishiwa na mafuriko kama Dar es Salaam ingekuwa salama wakati wa masika, lakini kila mwaka tatizo hilo hutishia maisha japo ufumbuzi wake unaweza pengine kupatikana kupitia uvunaji huo.

Kuvuna maji hayo kuna faida kwani kunapunguza ongezeka wa kuwa na makorongo makubwa, kuongezeka ukubwa wa mito, na kupanuka mikondo ya maji mijini na vijijini na kwa ujumla kunasaidia kukabiliana na uharibifu wa mazingira kunakotokana na maji ya mafuriko.

**UVUNAJI NYUMBANI**

Kuvuna maji ya mvua nyumbani yanayokusanywa kwenye mabati ya mapaa na kuingizwa kwenye visima vya familia ni njia mojawapo ya kusaidia kupunguza gharama za maji.

Gharama hizo hupungua si kwa familia pekee bali hata kampuni za majitaka na majisafi mijini kukiwa na maji hayo ya ziada hupunguziwa gharama za uendeshaji.

Gharama hizo ni kama kununua kemikali za kusafisha maji, kutumia umeme kuyasukuma na kuyafikisha kwenye vituo vilivyoko maeneo mbalimbali mijini kabla ya kuwafikishia wateja.

Faida nyingine nyingi hupatikana kwa watumiaji wa nyumbani ambao watatumia maji hayo kwenye kilimo, ufugaji na shughuli nyingine nyingi za nyumbani. Ni vyema kujaribu sasa. Kama kuna nia na njia itapatikana.

**KABWELA NA FADHIL MOHAMMED**



## HABARI KITAIFA



Mafundi wakiendelea na kazi ya uboreshaji wa mitaro ya maji ya mvua katika Barabara ya Malamba Mawili, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**.

# JPM ataja sababu kumng'oa bosi TRA

INATOKA UK.2

hawajawahi kumuona, kwa sababu Watanzania siyo wanafiki," alisema.

Kuhusu korosho, Rais Magufuli alisema wamefanya biashara hiyo zaidi ya tani 223,000 na kuhoji ni tani ngapi zimeshauzwa.

"Wizara inaitwa Wizara ya Viwanda na Biashara ni biashara gani inafanya? Wizara ya Kilimo imetimiza wajibu wake, imenunua, wanajeshi wametimiza wajibu wao wamesomba korosho yote wameweka kwenye maghala, Wizara ya Biashara inafanya nini? Ipo tu, korosho zimekaa," alihoji.

"Wakati huo Tanzania ilikuwa ndiyo wazalishaji peke yetu, tumesubiri hadi mwezi wa tatu mpaka wa nne ukaingia nchi nyingine za Benin, Nigeria, Cote d'Ivoire nazo zikazalisha bado hatujauza, wapo tu, sasa unakuwa unajiuliza wa nini? Kupeperusha bendera barabarani? Haiwezekani," alisema.

Rais Magufuli alimwambia Bashungwa kuwa nawezekana wamempongeza, lakini alifikiri wangempa pole kwa sababu akiona mambo hayaendi atamtengua.

"Kwa sabbabu nitaangalia yale ambayo hayaendi, nikiona hayaendi ninatengua nasema ukweli, Prof. Palamagamba Kabudi (Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki) na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wamezungumza tu hapa hawataki kusema, lakini kama ni 'pumbavu' kwenye simu wametukanwa mno waulizeni," alisema na kuongeza:

"Wananizidi umri, lakini neno pumbavu linakuja tu haraka haraka, ndiyo ukweli kwa sababu hii kazi siyo ya kubembelezana, lazima tuipeleke kijeshi, mwanajeshi usiposonga mbele kupigwa risasi na mwenzako siyo tatizo, mpo kwenye vita... hatuwezi kukawa na vita halafu tukawa tunabembelezana na kupeana maneno mazuri tu, lazima tubadilike, wanaotuangalia hawana muda wa kusubiri."

Rais Magufuli alisema Wizara ya Viwanda na Biashara wamebangua tani 2000, nyingine wanasubiri atelemke nani ndiyo waziuze.

"Na una waziri pale wa biashara ana vyombo vyote vya kufanya biashara nikitakiwa nimpandie kutoka juu mpaka chini, pamoja na wewe Muhende ulikuwa uende huko huko, ukienda kafanye kazi usibembeleze mtu usimchekee mtu nafuu wakuchukue mimi ninayekuteua nikusimamie kinyume na hapo utakwenda kunusa tu pale urudi Karagwe," alimweleza waziri mpya.

Rais Magufuli alimtaka waziri huyo yale ambayo yamekaa yatatuliwe, viwanda vilivyoshindwa kuendelezwa visiorodheshwe tu, vitafutiwe watu wavichukue.

INAENDELEA UK. 26


NHC

TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA NHC WANAODAIWA KODI NA MALIMBIKIZO

Shirikia la Nyumba la Taifa (NHC) linapenda kuwafahamisha wapangaji wake wanaodaiwa kodi na malimbikizo kuwa linawapa siku kumi na nne (14) hadi ifikapo tarehe 25/6/2019, kuhakikisha kuwa wanalipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa.Majina ya wadaiwa wote wa kodi na malimbikizo yatawekwa kwenye mbao za matangazo za Ofisi za NHC katika Mikoa yote na kwenye tovuti ya NHC ya www.nhc.co.tz. Muda huu umewekwa ili kuwapa fursa wapangaji kuhakikisha wanalipa madeni yote wanayodaiwa na Shirika. Taarifa hii inawahusu wapangaji walipo kwenye nyumba za Shirika na hata wale waliohama na kuacha malimbikizo ya kodi.

Aidha, Shirika linakaribisha wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za Shirika zilizo karibu nao ili kuweka utaratibu unaofaa wa kuwawezesha kukamilisha kodi na malimbikizo wanayodaiwa kwa wakati.

Shirika linaomba wapangaji wote kutumia fursa hii kulipa madeni yao na baada ya muda huu uliowekwa kukamilika, Shirika litapita nyumba hadi nyumba kukagua utekelezaji wa maelekezo haya. Kadhalika, baada ya ukaguzi huo, Shirika litatumia taratibu za kisheria kukusanya kodi na malimbikizo yanayodaiwa kwa kila mpangaji, ikiwemo kukamata na kupiga mnada mali za wapangaji ili kufidia kodi na malimbikizo yanayodaiwa.

Tunawashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika na Taifa kuwaletea watanzania maendeleo kwenye sekta ya nyumba.

IMETOLEWA NA:

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
MAKAO MAKUU S.L.P 2977 I DAR ES SALAAM TANZANIA I SIMU: +255 22 2105001-5 I NUKUSHI: +255 22 2105000
BARUA PEPE: dg@nhctz.com I TOVUTI: www.nhctz.com

BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI MKUU

OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII
NHC-MAKAO MAKUU.


# Mmiliki wa Lucky Vincent ahukumiwa jela miaka 4

INATOKA UK.3

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahama hiyo, Niku Mwakatobe, alisema mshtakiwa wa kwanza Inocent, mahakama imemuamuru kwa kosa la kwanza kulipa faini ya Sh.500,000 au kwenda jela miaka miwili.

Mwakatobe alisema kosa la pili mshtakiwa wa kwanza anatakiwa kulipa faini ya Sh. 200,000 au kwenda jela miezi sita.

Kosa la tatu hakimu alisema mshtakiwa wa kwanza anatakiwa kulipa faini ya Sh.300,000 au kutumikia kifungo cha mwaka mmoja gerezani.

Kwa upande wa kosa la nne, hakimu Mwakakatobe alisema mshtakiwa wa kwanza ametiwa hatiani na anatakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela mwaka mmoja.

Kosa la tano lilikuwa kwa mshtakiwa wa pili kwa Longino Nkana, ambaye ni Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, alihukumiwa kwenda jela kwa mwaka mmoja au kulipa faini ya Sh. 500,000.

Naye wakili wa upande wa utetezi, Method Kimomogolo, aliiomba mahakama hiyo, kuangalia hukumu hiyo, kwa kuwa makosa aliyoshtakiwa mteja wake kwa nafasi yake ya ukurugenzi wa shule .

Alisema makosa hayo yalifanywa na kampuni ya Lucky Vincent ya siyo mmliki hivyo aliiomba mahakama hiyo, kutoa adhabu ya faini kwa kuwa kosa hilo limefanywa kwa mara ya kwanza.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Mashtaka kifungu cha 69, 73, makosa haya yanapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini, " alisema Kimomogolo.

Washtakiwa hao walitimiza masharti ya kulipa faini hizo na wapo huru.

Mapema Mei 12, 2017, washtakiwa katika kesi hiyo mmiliki wa shule hiyo, Inocent Moshi, pamoja na Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Longino Nkana, walisomewa mashtaka matano, ikiwamo kusafirisha wanafunzi bila vibali maalum.

Moshi alikabiliwa na mashtaka manne ikiwamo kufanya biashara ya usafirishaji abiria bila kuwa na leseni, kuruhusu gari kutumika bila kuwa na bima pamoja na kushindwa kuingia mkataba na mwajiriwa wake na kuzidisha abiria 13.

Mshtakiwa wa pili, Nkana alikuwa akikabiliwa na shitaka moja la kuzidisha abiria katika chombo cha usafiri.

Katika ajali hiyo iliyosababisha wanafunzi 32 kufariki, walimu wawili na dereva mmoja kupoteza maisha.

# ACT yampa Maalim Seif kazi maalum

INATOKA UK.5

katika kamati za chama hicho ni Kuruthumu Mchuchuli (Katiba na Sheria), Mbarala Maharagande (Uadilifu) na Recho Kimambo (Mikakati, Usimamizi na Ufuatiliaji).

Kikao hicho ni cha kwanza kufanyika tangu Maalim Seif alipojiunga na chama hicho Machi mwaka huu, akiambatana na waliokuwa viongozi waandamizi wa CUF akiwamo aliyekuwa mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2015 kupitia Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ambaye kwa sasa ni Naibu Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji.

Awali akizungumzia ajenda za kikao hicho, Shaibu alisema ni kutathmini mwelekeo wa chama hicho kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu pamoja na operesheni mbalimbali za chama hicho kama "Shusha tanga, pandisha tanga".

"Kamati Kuu itatathmini na kupanga mwelekeo wa chama chetu kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tunakwenda namna gani, matarajio yetu ni yapi, lakini la muhimu tunakwenda na nani," Shaibu alisema.

HABARI MIKOANI

# Watano wafa kwa kufukiwa kifusi

**Na Idda Mushi,** GAIRO

WATU watano wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi cha mchanga kwenye mgodi usio rasmi wa madini ya dhahabu mkoani Morogoro.

Tukio hilo lililotokea eneo la Ndulutu, kijiji cha Kilama, Kata ya Iyogwe wilayani Gairo, huku watu sita wakijeruhiwa.

Watu zaidi ya 1,000 wanadaiwa walivamia eneo hilo kuanzia mwishoni mwa Mei mwaka huu, kutoka maeneo mbalimbali nchini baada ya kusikia uwapo wa madini ya dhahabu.

Inaelezwa kuwa wakati wakiendelea na uchimbaji, miongoni mwa waliopoteza maisha waliona kipande cha dhahabu na kuingia shimoni kuwahi kukichukua, lakini mchanga uliwaangukia na kuwafukia na wanne wakapoteza maisha papo hapo, huku mwingine akipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen Kebwe, alifika eneo la tukio na kubainisha mgodi huo usio utafungwa kwa muda kutokana na kukosekana huduma za msingi na uchimbaji usiofuata taratibu zikiwamo za kiusalama, ili kuepusha madhara zaidi yanayoweza kutokea.

"Kwanza kwa uchimbaji huu kulikuwa na hatari pia ya kuibuka kwa magonjwa ya milipuko kikiwamo kipindupindu, eneo hili halina hata choo wala sehemu salama ya malazi na chakula, acha hatari iliyopo ya uchimbaji holela uliokuwa ukiendelea,"alisema Dk. Kebwe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, alisema mpaka sasa miili mitano imechukuliwa na ndugu zao kwenda wilayani Kilindi kwa ajili ya taratibu zaidi za maziko.

Kamanda Mutafungwa alisema tukio hilo lilitokea Juni Jumamosi jioni na kuwa wote waliofariki dunia ni Magele Muya, Juma Chabala Mabagala, Paulo Francis na wengine wawili ambao majina yao hayajaweza kufahamika mara moja.

Kamanda Mutafungwa alisema Jeshi la Polisi limeimarisha ulinzi katika eneo la machimbo, na wanatarajia kuongeza askari zaidi ili kukabiliana na idadi kubwa ya watu waliokuwa wamevamia eneo hilo.

Alisema majeruhi sita wa tukio hilo wamepelekwa Hospitali ya Misheni ya Berega wilayani Kilosa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe, alisema baada ya uvamizi wa wananchi katika eneo hilo, alikwenda eneo la tukio na akawataka wachimbaji hao kuunda vikundi ili kujisajili na kupata leseni badala ya kuendelea na uchimbaji usiozingatia sheria na taratibu.

Alisema kwa mara nyingine alipokwenda eneo hilo na kamati yake ya ulinzi na usalama ya wilaya, walikuta kuna kikundi kimoja cha watu 15 kilichoundwa kikiongozwa na mwenyekiti wa kijiji, lakini kikawa na ajenda nyingine ya kuwarubuni wachimbaji waliopo kuwa wangewasimamia katika shughuli za uchimbaji.

Nao baadhi ya wachimbaji wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa dharura, Tembo Josephat, Ally Kuni Makule na Sospeter Kiama waliiomba serikali kufunga eneo lililosababisha maafa pekee na kwingine waachiwe kuendelea na uchimbaji ili kujikimu kimaisha sambamba na kuwatengenezea utaratibu wa kila kikundi kutumia shimo lake, na watakokuwa wakiingia kuorodheshwa majina kwa ajili ya usalama wao.

Naibu Waziri wa Madini, Stanislaus Nyongo, alifika eneo hilo na kuwataka wachimbaji hao kutambua kuwa ardhi yote ni mali ya serikali, hivyo pamoja na kupata madini, bado eneo hilo litafungwa hadi pale taratibu zitakapofuatwa.



Shimo katika mgodi usio rasmi liliosababisha vifo vya watu watano na wengine sita kujeruhiwa kijiji cha Kilama, Kata ya Iyogwe wilayani Gairo, Mkoa wa Morogoro. **PICHA: IDDA MUSHI**.



## Mwanafunzi atoweka

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu, Zakia Maghembe (16), mkazi wa Kawe Ukwamani jijini Dar es Salaam anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani tangu sikukuu ya Iddi pili.

Mama mdogo wa mwanafunzi huyo, Mwajab Salum ambaye alifika jana kwenye ofisi za The Guardian zilizopo Mikocheni jijini Dar es Salaam, alisema siku ya tukio Zakia aliamka asubuhi na kufanya kazi za asubuhi kisha kuondoka na hajarudi hadi jana.

"Baada ya kuamka wakati anafua nguo mimi nilitoka kidogo niliporudi msaidizi wangu wa ndani akaniambia Zakia ameondoka, hadi leo hajarudi na tumemtafuta kwa ndugu jamaa na marafiki bila mafanikio," alisema.

Mwajab alisema hiyo ndiyo mara yake ya kwanza kufanya tukio hilo na kwamba wakati anaondoka hakuwa na mgogoro naye.

Alisema ameshatoa taarifa kituo cha Polisi Kawe na kupewa RB/3748/ 2019 na ameomba kwa yeyote atakayemuona apige simu 0713 513374 au awasiliane na kituo chochote cha polisi.

# Wachimbaji walia Tume ya Madini

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, amekutana na kilio cha wachimbaji wa madini mkoani Lindi, kuhusu ongezeko la tozo zilizo kinyume cha sheria ya madini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wachimbaji hao walisema halmashauri za wilaya na vijiji zimekuwa zinawatoza tozo zaidi na ile iliyowekwa na sheria mama ambayo ni 0.03 badala yake wamekuwa wakitumia sheria ndogo zilizopitishwa na Baraza la Madiwani kuwatoza tozo zaidi kinyume cha sheria mama.

Waliongeza kuwa halmashauri zinatoza tozo zao, na halmashauri za vijiji nazo zinajipangia ushuru wao, hivyo kuwa kero na kusababisha usumbufu.

Kilio hicho walikiwasilisha wakati wa mkutano mkuu wa sekta ya madini uliofanyika tarehe Januari 22, 2019 chini ya uenyekiti wa Rais John Magufuli.

Prof. Kikula alikutana na kilio hicho akiwa ziara mkoani humo kutembelea na kukagua shughuli za madini, kusikiliza na kutatua kero za wadau wa madini.

Kufuatia kilio hicho, Prof. Kikula alitoa wito kwa wachimbaji wa madini ya gypsum, kokoto, chumvi na mchanga nchini kote kuwa na subira wakati Tume ya Madini ikihangaikia utatuzi wa changamoto hiyo ya utozwaji wa tozo zinazo tozwa na baadhi ya halmashauri za wilaya na vijiji kinyume cha taratibu za sheria ya madini.

Prof. Kikula alitoa kauli hiyo baada ya kutembelea machimbo mbalimbali ya madini ya gypsum ikiwamo ya kampuni ya KNAUF Gypsum Tanzania Ltd, machimbo ya mavuji yanayomilikiwa na mchimbaji mdogo Faridu Sheweji na mchimbo ya chumvi yanayomilikiwa na Magereza Lindi eneo la Machole.

Akijibu hoja ya kero hiyo, Prof. Kikula alikiri uwapo wa malalamiko hayo kutoka kwa wachimbaji wa mikoa mbalimbali nchini na kuwa siyo kwa Lindi peke yake.

Alishangazwa na hali hiyo kwa kuwa sheria ya madini na miongozo mbalimbali iko wazi na inaelekeza vizuri kuhusu tozo zinazotakiwa kutozwa.

Alisema wanafanya jitihada kutatua kero hiyo, hivyo watawasilisha malalamiko yao kwa mamlaka ya juu ambayo ni Waziri wa Madini, Doto Biteko ili azungumze na Waziri wa Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, ili kuondoa kero hiyo.

"Nalitambua hili tatizo, kila tunapofanya ziara mikoa mbalimbali hii changamoto inajitokeza, sijui ni kwa nini inakuwa hivyo kwa sababu sheria iko wazi namna tozo zinavyotakiwa kutozwa. Naomba niwaahidi tutalishughulikia hili haraka sana, na mara baada ya ziara hii tutaandaa ripoti na kuiwasilisha kwa Waziri Biteko, pamoja na ripoti, lakini pia nitamwambia kwa mdomo ili kusisitiza juu ya kero hii," alisema Prof. Kikula. Prof. Kikula aliziomba halmashauri na kila mdau wa madini kote nchini wazisome na kuzipitia vizuri sheria ya madini hususani inayohusu tozo mbalimbali za madini kabla ya kuanza kuwatoza wachimbaji.

Aliambatana na Kamishna wa Madini, Prof. Abdulkarim Mruma, katika ziara ya kikazi katika mikoa ya Lindi, Ruvuma, Njombe na Iringa kukagua shughuli za madini na kusikiliza na kutatua kero.

# Spika aitaka serikali kupitia tozo mizigo bandarini

Na Augusta Njoji, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka serikali kupitia upya vigezo vilivyowekwa kwenye mizigo inayopita Bandari kwenda Zanzibar kutokana na kulalamikiwa na wananchi ikiwamo wabunge.

Mwongozo wa tozo kifungu cha 29 wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), tozo ya 'Wharfage' inatozwa kwa mizigo ya biashara yenye uzito zaidi ya kilo 21 au yenye zaidi ya mita moja ya ujazo (CBM) inayopita kwenye gati, jeti na maboya yaliyo chini ya TPA.

Kauli hiyo ya Spika imekuja baada ya kujibiwa swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Maryam Salum Msabaha, kudai kuwa kuna changamoto bandarini na kwamba hata kilo 10 zinatozwa fedha hali inayosababisha malalamiko kwa wananchi.

Mbunge huyo alihoji ni vigezo gani ambavyo vinatumika kwa mizigo ya biashara na mizigo binafsi kwa wasafiri.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema vigezo vipo mwongozo wa tozo TPA na kwamba tatizo linaonekana ni uelewa.

"Niwaelekeze Bandari watoe elimu ya kutosha kwa wananchi wanaotumia usafiri kwenda Zanzibar ikiwamo hili la uzito wa kilo 21 na kuendelea ndio unatakiwa kutozwa, sio nia ya serikali kuona wananchi wake wanalalamika," alisema.

Kufuatia majibu hayo, Spika Ndugai, alisema kama kweli kilo 21 ndio kiwango cha chini ipo haja kuangalia kwenye boti.

"Maana kilo 20 hata sanduku la mwanafunzi linazidi, hata baadhi ya mashirika ya ndege yanatoa zaidi ya kilo 20, sasa kwenye boti kilo 20 ni kidogo sana."

Aliongeza "Ipo haja ya kuangalia kama sio sheria ni kanuni tu...Mtu akibeba mihogo mitatu kilo 20 tu anakuwa ameshavuka kwa hiyo tuliangalie, hawa wenzetu wanaotoka Zanzibar wapate raha kidogo na imekuwa kero kwa wananchi serikali iliangalie hili."

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema abiria wanaokwenda Zanzibar kwa boti hulipishwa ushuru wa Bandari kwa mizigo hata kama boksi la kilo 10 au kilo 20 za mchele kwa Sh. 9,750.

"Je, ni mizigo gani ambayo abiria anapaswa kulipia ushuru huo wa Bandari (Wharfage)," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kwandikwa alisema TPA huikusanyi tozo yoyote kwa abiria ambao wana vifurushi binafsi vyenye uzito au ujazo mdogo wanaotumia Bandari kwenda Zanzibar kwa boti eneo la 'Baggage room.

Aidha, alisema abiria wanaotumia Bandari kwenda Zanzibar kwa boti ambao hutozwa ushuru katika eneo la 'Bagage room' ni wale tu wanaokuwa na mizigo mikubwa tena kwa madhumuni ya kibiashara.

Alitoa wito kwa wateja wote wanaotumia Bandari kwenda Zanzibar kwa boti wahakikishe kuwa mizigo yao inapimwa kabla ya kupakiwa ili wajue uzito wake unaostahiki kutozwa ushuru.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akimsikiliza Spika wa Bunge la Rwanda, Mukabalisa Donatille, baada ya kumpokea katika uwanja wa ndege wa jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE.**

# 'Biashara ya kuni, mkaa ni rasmi'

BUNGE limeelezwa kuwa biashara ya kuni na mkaa ni rasmi na haina kizuizi chochote kwa mwananchi yeyote.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zubeda Sakuru.

Katika swali lake, alihoji ongezeko la gharama za nishati nchini hasa umeme na gesi kusababisha kuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya kuni na mkaa.

"Je, ni lini serikali itarasimisha biashara ya mkaa ili kupunguza makali ya maisha hasa kwa Watanzania wenye kipato duni," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kanyasu, alisema biashara hiyo inafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za misitu pamoja na tangazo la serikali Na. 324 la 14/08/2016 na mwongozo wa uvunaji wa mazao ya misitu wa mwaka 2007 uliofanyiwa marekebisho mwaka 2015.

"Hivyo, biashara hii ni rasmi na haina kizuizi chochote kwa mwananchi yeyote. Kinachotakiwa ni kufuata sheria na taratibu za kufanya biashara ambazo zimefafanuliwa vyema katika mwongozo wa uvunaji ambao unamtaka kila mvunaji wa miti kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa kuzifuata," alisema.

Alieleza kuwa kutokana na uhaba mkubwa wa nishati ya miti serikali inawahimiza Watanzania na wadau wote kuanzisha mashamba ya miti kwa ajili ya matumizi ya nishati.

Aliwaomba wabunge kuisaidia sekta ya misitu kwa kuishauri serikali kutoa ruzuku kwenye umeme, gesi na uzalishaji wa nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ambayo inaongeza uharibifu wa misitu.

Hata hivyo, Kanyasu alifafanua kuwa kitu ambacho baadhi ya wafanyabiashara na wachoma mkaa hawatimizi ni pamoja na kutambua na kutenga maeneo ya misitu kwa ajili ya kutengeneza mkaa.

"Kila atakayehusika na shughuli ya biashara ya mkaa kutakiwa kusajiliwa na meneja wa misitu wa wilaya na atatakiwa kuwa na leseni, maombi ya usajili na leseni yanapaswa kupelekwa kwa ofisa misitu wa wilaya na kujadiliwa na kamati ya kusimamia uvunaji wa wilaya," alisema.

Pia alisema kila mfanyabiashara wa mkaa anatakiwa kulipia mrabaha kama ilivyoainishwa katika jedwali la 14 katika sheria ya misitu.

# Mpango kudhibiti magonjwa yasiyoambukizwa waja

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kuanzisha mpango wa taifa wa udhibiti wa magonjwa yasiyoambukizwa na ugonjwa wa selimundu utakuwa ni moja ya magonjwa yatakayokuwa yanaratibiwa kitaifa.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo, ambaye alihoji serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wagonjwa wa selimundu kupata matibabu bure.

Akijibu swali hilo, Dk. Ndugulile alisema kuwa watoto wenye ugonjwa huo wanahitaji matibabu mfululizo kwa kuwa huwa wanapata maumivu na madhara ya ugonjwa huo mara kwa mara.

"Familia, jamii na wadau mbalimbali wamekuwa wakijitahidi sana kuwahudumia watoto hao, kwa kuwapatia mahitaji maalum, hata hivyo, misaada hiyo haikidhi mahitaji ya wagonjwa wote na kuna baadhi ya familia hazina uwezo wa kuwahudumia watoto wenye selimundu," alisema.

Kwa kutambua hilo, Naibu Waziri alisema serikali kupitia wizara hiyo imeandaa mwongozo wa kutoa msamaha kwa makundi tofauti yasiyo na uwezo likiwamo kundi la watu wenye magonjwa sugu kama selimundu.

"Kupitia maofisa ustawi wa jamii, familia zisizo na uwezo uhakikiwa na kupatiwa kibali cha huduma bila malipo," alisema.



# RC aagiza wake wa vigogo kutibu vijijini

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amemwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa huo, kuwaondoa madaktari wanaofanyakazi katika hospitali ya Babati Mrara, wanaowaomba wananchi rushwa.

Aidha, amemwagizwa pia kuwahamisha wanawake wa vigogo madaktari wanaofanya kazi hospitali ya mji wa Babati Mrara na kuwapeleka zahanati zilizopo vijijini.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wazee wa Halmashauri ya Babati na Halmashauri ya Mji wa Babati baada ya baadhi ya wazee kulalamikia zahanati za vijijini kukosa madaktari kwa muda mrefu na hivyo wananchi kuikosa huduma ya afya.

"Mganga mkuu ondoeni wale madaktari Hospitali ya Mrara wanaokula rushwa maana wapo ambao wanadaiwa kulazimisha wananchi kutoa fedha nyingi, operesheni inalipiwa Sh. 100,000 wao wanaifanya kwa Sh. 250,000. Na madaktari wake wa wakubwa ondoeni kabisa," aliagiza Mnyeti.

"Madaktari ambao akili zao haziko sawa waondoeni peleka zahanati ya Endabeg na zingine zenye uhaba. Na wanaokulakula rushwa na kulewa wakipelekwa kule zahanati zilizoko vijijini akili zitakaa sawa," alifafanua.

Aidha, alimtaka mganga huyo mkuu kukaa pamoja na katibu tawala wa mkoa huo, ili waone madaktari wa kuwaondoa na kuwatupa porini ambako hamna madaktari licha ya kuwapo zahanati.

Katika muda wa maswali kwa wazee, Mzee Ndege Gwalai kutoka Endabeg alimuuliza Mnyeti ni lini watapata daktari ahadi ambayo aliwahi kuwaahidi kipindi cha nyuma.

Wazee hao pia walilalamikia huduma duni za afya katika hospitali za umma, vituo vya afya na zahanati wakisema hawapewi dawa bali wanaambiwa wakanunue.

Baada ya kusikiliza kero hizo Mnyeti aliwauliza wakurugenzi kama wameshawapatia vitambulisho wazee wote, wakurugenzi wote walikiri kuwa bado hawajawapa vitambulisho wazee hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati Fortunatus Fwema, alisema wazee waliopatiwa vitambulisho ni asilimia 50, ambapo jumla yao ni 5,492, lakini waliowapatia ni 2,347.

Baada ya kujibu hivyo Fwema alimuuliza Mnyeti vitambulisho vilivyobaki vinagharimu Sh. ngapi na kujibiwa Sh. milioni 8.4 na kutakiwa kuahidi ni lini vitakuwa tayari. Alisema baada ya mwezi mmoja na mwenzake wa Babati Wilaya, Hamisi Malinga naye akaomba mwezi mmoja kuviandaa.

Mnyeti alihitimisha kwa kusema wakurugenzi waandae hivyo na baada ya mwezi mmoja watafanya mkutano kama huo na kuwataka wazee wawe na vitambulisho katika mkutano mwingine na kuahidi kuvikagua.



Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha, Hassan Kimanta (kushoto), akimkabidhi Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Titus Mmasi, sehemu ya msaada wa mabati yenye thamani ya Sh. milioni 5, kutoka benki ya NMB, kwa ajili ya uendelezaji wa Kituo cha Afya Mto wa Mbu, katika hafla iliyofanyika juzi. Kulia ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro na (katikati) ni Meneja wa benki hiyo, tawi la Monduli, Rebecca Lobulu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinamama wajitosa zahanati ya kijiji

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

KATIKA jitihada za kupunguza vifo vya wazazi, wajawazito na watoto, wanawake wa Kijiji cha Laandai, wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara wamejitosa kujenga zahanati ya kijiji hicho.

Kinamama hao wanashiriki kubeba mawe, mchanga na kuchanga Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho.

Wamelazimika kuchukua uamuzi huo ili kuepuka adha ya kujifungulia nyumbani, kufa nyakati za uzazi, lakini pia kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma za afya.

Magdalena Laizer, akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake jana mbele ya Mbunge wa Jimbo la Simajiro, James Ole Millya, wakati wa siku ya kwanza ya ziara yake jimboni humo, alisema wamelazimika kuchukua hatua hiyo kutokana na adha kubwa wanayoipata wanawake.

"Tunaomba serikali ituunge mkono ili kuondokana na ukosefu wa huduma za afya hasa kwa kinamama na mtoto katika kijiji chetu na kata ya Laangai ambayo hatuna huduma hizo, hali inayosababisha baadhi ya wananchi hasa wajawazito na watoto kupoteza maisha."

Licha ya changamoto hiyo wananchi hao walimwomba mbunge kutatua kero ya maji kutokana na wanawake kusafiri umbali mrefu kutafuta maji ya visima na wakati mwingine wanatumbikia visimani na kupoteza maisha.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gasto Silayo, alisema halmashauri inatambua adha wanayopata wanawake wa Laangai na kwamba imetenga Sh.milioni 30, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa zahanati hiyo.

Kwa mujibu wa Silayo baada ya uongozi wa halmashauri kuona jitihada za wanawake hao uliamua kupima eneo hilo na kukipa kijiji hati miliki na kwamba wiki hii, ofisa mtendaji atapewa vitabu maalum kwa ajili ya kuchagisha fedha kwa wadau wa maendeleo ili zahanati hiyo iweze kumalizika mara moja.

Aidha, Mbunge Ole Millya, alichangia Sh.5,000,000 na kuungwa mkono na wafanyabiashara Phinihas Njeree aliyetoa Sh. milioni mbili na Samwel Katambaoi Sh.500,000.

Kuhusu kero ya maji, Ole Millya alisema kuna mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa na serikali wenye thamani ya Sh. bilioni 41 kutoka mto Ruvu hadi makao makuu ya wilaya hiyo yaliyoko Orkesmet, unaokamilika Mei mwakani.

Ole Millya alisema baada ya maji hayo kufika eneo la Orkesmet yatasambazwa katika sehemu mbalimbali ili wananchi waweze kupata maji ya uhakika.

# Mwenge wahimiza ushirika uchaguzi serikali za mitaa

**Woinde Shizza**, ARUSHA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019, Mzee Mkongea Ally, amewataka wananchi kujitokeza kikamilifu na kushiriki kwenye uchaguzi wa serikali za vijiji na mitaa, unaofanyika Oktoba mwaka huu.

Aliwahimiza husussan vijana wenye mahitaji maalumu na kinamama, kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ambazo zinagombaniwa ili kuwa sehemu ya uongozi wa taifa.

Aliwataka wananchi kujitokeza kusikiliza sera za wagombea wa vyama mbalimbali ili kufanya maamuzi ya kuchagua kiongozi ambaye ataweza kuwaongoza vyema na kuwaletea wananchi maendeleo.

"Wananchi wenzangu jitokezeni kwenye mikutano na kusikiliza sera za hawa viongozi wanaogombea ili muweze kufanya uchaguzi sahihi katika chaguzi za serikali zijazo na msichague bora kiongozi, bali chagueni kiongozi bora," Ally.

Aidha, aliwataka wananchi kulipa kodi kwani ndiyo msingi na chanzo kikuu cha fedha za maendeleo ya taifa kwa kuwa kwa kufanya hivyo ndivyo wanavyosaidia kuleta maendeleo katika halmashauri, mijini na vijijini.

Wakati huo huo, aliwahimiza wananchi kutunza maji pamoja na vyanzo vyake ili viwanufaishe kwenye kilimo na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019, Mkongea Ally, alisema jana wakati akizindua miradi ya maji na kuweka jiwe la msingi wilayani Arumeru.

Alisema maji ni rasilimali muhimu ambayo inahusika kuleta maendeleo na ni ya lazima kwa maisha, hivyo wananchi wanatakiwa kutunza mazingira hususani vyanzo hivyo vya maji.

Aidha, alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali na imetenga Sh.trilioni 9.2 kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama.

"Na katika suala hili la kutunza vyanzo vya maji napenda kuwasihi wananchi wenzangu kuacha kuchunga mifugo yenu katika vyanzo vya maji pamoja na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu ili vidumu," alisema Ally.

Alisema maji ni haki ya kila mtu hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuyatunza na kuhifadhi vyanzo hivyo.

Katika mbio hizo za Mwenge wilayani Arumeru, Mwenge ulizindua miradi mbalimbali ikiwamo ya Sekondari ya Odonyowas, mradi wa maji wa Layout Srwsita, mradi wa nyuki na hospitali ya mama na mtoto ya Olturmenti.

# TFS yaonya kuhusu utapeli mashamba

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika mashamba ya serikali yaliyoko Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, imetoa tahadhari kwa wananchi kuwa makini na watu wanaojifanya watumishi wa taasisi hiyo ambao wanawarubuni wananchi na kujipatia fedha isivyo halali.

Watu hao wanaojifanya kuwa ni watumishi wa wakala hiyo, wanadaiwa kuwarubini wakulima kwamba wana uwezo wa kuwapatia maeneo ya kilimo ndani ya shamba hilo maarufu kama 'ploti'.

Meneja wa TFS wa West Kilimanjaro, Magesa Mabeko, alisema mtandao huo hatari wa utapeli umekuwa ukitumia baadhi ya majina ya watumishi wake kwamba wana uwezo wa kuwapatia ploti kwa ajili ya kilimo, hivyo wawatumie fedha.

Alitoa wito kwa wananchi waliomilikishwa 'ploti' katika eneo hilo kwa msimu wa kilimo, kuacha kuuza 'ploti' hizo kwa matajiri kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha utaratibu.

"Watu wengi sana wametapeliwa na watu hao kwa njia hiyo ya kuwapigia simu hasa kipindi cha ugawaji wa 'ploti' kwa ajili ya kilimo cha viazi, vitunguu, nyanya, karoti na kabeji, mazao ambayo huzalishwa zaidi ukanda huo wa mwinuko wa West Kilimanjaro," alieleza Mabeko.

"Haya matukio ya kutapeliwa watu tumewajulisha vyombo husika na mpaka sasa wameshakamatwa watu watatu. Tumetoa matangazo mbalimbali ikiwamo kwenye mikutano ya kijiji, makanisani na misikitini kwa maana ya kupata shamba na kuepukana na hawa watu matapeli," aliongeza.

Mmoja wa wakulima wa West Kilimanjaro, John Mollel, anayeishi Sanya Juu, alisema alipigiwa simu na kuambiwa atoe Sh. milioni tano ili apatiwe 'ploti' kwa ajili ya kilimo kwa njia laini, lakini baada ya kufuatilia aligundua kuwa ametapeliwa.

Meneja huyo alisema katika utaratibu wa kugawa mashamba hayo, TFS huwaita viongozi wa vijiji wakiwamo wenyeviti na watendaji wa vijiji, kata na ofisa tarafa na kuwajulisha kuwa 'ploti' kwa ajili ya kilimo ziko tayari, hivyo wawasilishe majina ya watu wenye sifa ya kupewa hasa kwa kaya maskini.

# Wafugaji walalamikia gharama kubwa kupandisha ng'ombe

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WATAALAMU wa sekta ya kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, wameanza kuwajengea uwezo wananchi wa vijiji sita vya Kahe Mashariki kuhusu namna ya kukabiliana na viwavijeshi aina ya 'fall armyworm' wakati huu wa msimu wa masika.

Viwavijeshi hivyo wenye jina la kisayansi 'spodoptera frugipedra' ndio wadudu hatari zaidi wanaoharibu mazao ya chakula.

Akithibitisha wataalamu hao kufika katika vijiji hivyo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu udhibiti wa viwavijeshi hao iwapo watajitokeza kushambulia mazao, Diwani wa Kahe Mashariki (CCM), Kamili Mmbando, alisema wataalamu hao wameshawafikia robo tatu ya wakulima.

Hayo yamo katika taarifa maalum ya maendeleo ya kata hiyo yaliyosomwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wanaounda halmashauri hiyo.

Kwa mujibu wa Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Chikira Mcharo, viwavijeshi hivyo hupenda kula mahindi machanga na wana uwezo wa kula baadhi ya mimea mingine. Mazao mengine yanayoshambuliwa na viwavijeshi hao ni mchele, mtama, ngano, miwa na mboga.

Asili ya wadudu hao ni nchi zilizo katika maeneo ya kitropiki kwenye Bara la Amerika Kaskazini na Kusini.

Taarifa zaidi za kisayansi zinaeleza kuwa viwavijeshi aina ya 'fall armyworm', huzaana na kuongezeka wakati wowote wakiwa katika hatua zozote za maisha.

'Fall armyworm' ni viwavi na ila si minyoo kama vile jina lao linavyojieleza na hatua yao ya maisha ya mdudu kamili huwa ni nondo au kipopo.



Wazoa taka wakipakia katika eneo la Sinza, jijini Dar es Salaam jana, bila kuwa na vifaa vya kukinga mikono jambo ambalo ni hatari kwa afya zao. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Wataka ripoti uchunguzi hadharani

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

WAKAZI wa Kata ya Kia, Wilaya ya Hai, wamemwomba Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kuwapa mrejesho wa ripoti ya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya askari wa kituo cha Kia juu ya kuwabugudhi wananchi wanaozunguka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (Kia).

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana na wengine kwa sharti la kutotajwa kwa majina yao, wamemwomba Dk. Mghwira kuitoa hadharani ripoti hiyo baada ya kukabidhiwa.

"Tunasubiri majibu ya uchunguzi wa hizo tuhuma zilizotolewa na wananchi wa Kia na hoja yetu kubwa kwa mkuu wa mkoa, mara tu atakapokabidhiwa ripoti hiyo aiweke hadharani kwa kupeleka mrejesho kwa wananchi hao," alisema Zakayo Metishil.

Mei, mwaka huu, mkuu huyo wa mkoa aligiza kuchukuliwa hatua za kisheria askari polisi wa Kituo cha Polisi cha Kia ambao wanatuhumiwa kuwabugudhi wananchi wanaozunguka kiwanja hicho.

Dk. Mghwira alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Hamisi Issah, kuchunguza tuhuma za askari wa kituo hicho kudaiwa kufyatua risasi hewani kwenye makazi ya watu na kuwakimbiza watoto wa wafugaji waliokuwa katika malisho ya mifugo.

Pia aliagiza kufanyike uchunguzi juu ya mkuu wa kituo cha Kia, kwa nini hakuchukua hatua kwa askari wa kituo chake wanaotuhumiwa kwa utovu wa nidhamu kutokana na tukio lililotokea Aprili 7, mwaka huu.

Pamoja na mambo mengine, akiwa katika Kijiji cha Sanya Station, Dk. Mghwira alimtaka Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro kuchunguza utendaji wa askari wa kituo hicho ambao wamekuwa wakilalamikiwa na wananchi wa maeneo hayo.

Alisema tukio la askari hao kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani na kuwabugudhi wananchi linaleta taswira hasi kwamba serikali ndiyo inakandamiza wananchi wake na kusisitiza umuhimu wa kudumisha amani na maelewano baina ya jamii zinazopakana kwenye eneo hilo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 11, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15



## Mahakama na nafasi yake kulinda mazingira nchini

## JE WAJUA



Ukurasa 18

## 'Mtoto Detmold' maiti iliyoishi miaka 6,500



# RAIS MPYA WA SERIKALI MUHAS: Miundombinu ikiboreshwa vijijini madaktari wote watakwenda huko

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# FAHAMU MAANA YA USHAHIDI UNAVYOTUMIKA MAHAKAMANI



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, David Misime.. **PICHA MTANDAO**

USHAHIDI ni maelezo, nyaraka, vithibitisho au kitu chochote kinachokubaliwa mahakamani kuwa vinakidhi vigezo vya kisheria kuwa ushahidi na hivyo kupokelewa na kutumika kuthibitisha au kukanusha tuhuma.

Mtuhumiwa atavitumia vitu hivyo vilivyotajwa hapo juu kukanusha tuhuma dhidi yake katika utetezi.

MIFANO YA USHAHIDI

Kama mtu anatuhumiwa kuvunja na kuiba, Polisi wanaweza kupata alama za vidole za mtuhumiwa kwenye nyumba alipovunja.

Kwa hiyo, alama za vidole zitaletwa kama ushahidi dhidi ya mtuhumiwa.

Kama mtu anatuhumiwa kubaka, Polisi wanaweza kumhoji anayedaiwa kutenda kitendo hicho na kama watu wa ziada au vielelezo wanaoweza kuthibitisha tuhuma hiyo wanaweza kuhojiwa. Vilevile polisi wataagizwa ujazwaji wa fomu namba tatu ya Polisi ( PF 3) na madaktari wenye vigezo ili kuletwa kama ushahidi mahakamani dhidi ya mtuhumiwa.

Kama mtu anatuhumiwa kuiba simu kwenye duka na kuna mtu alimuona akiiba, basi yule mtu anaweza kuletwa mahakamani na kutoa ushahidi kuwa alimuona mtuhumiwa akiiba simu, mtu huyo atakuwa shahidi wa upande wa mashtaka.

Kama mtu anatuhumiwa kuiba simu vingunguti, Ilala, Dar es salaam saa 1 jioni siku ya Jumamosi lakini mtu mwingine ( shahidi wa upande wa utetezi) alimuona mtuhumiwa huyo huyo sehemu nyingine tofauti saa hizo hizo saa 1 jioni Jumamosi maeneo ya Kunduchi, Kinondoni, Dar es salaam tofauti na eneo la awali analotuhumiwa kuiba, huyu mtu mwingine ataletwa mahakamani kama shahidi wa utetezi kukanusha tuhuma au mashtaka dhidi ya mtuhumiwa.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**DAR ES SALAAM**
**Barua pepe: habariphq@gmail.com**



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO** marobarnabas@yahoo.com

# Lugha za waandishi zachusha

'CHUSHA' maana yake ni chukiza; udhi, chosha. Pia ni kiumbe kisichopendeza kwa watu kutokana na vitendo vyake; kirihisha. Kuna maana ingine pia lakini siitumii kwani yaweza kuniletea uhasama (hali ya kufarikiana nao) kwa kukosoa Kiswahili chao.

Ilivyo ni kama Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) limerithiwa na waandishi wa magazeti wanaoonekana kuanzisha lugha yao na kuwakanganya (duwaza mtu asijue la kufanya, fanya mtu achanganyikiwe) wasomaji. Maneno halisi yameachwa na kutumiwa ya mitaani au kuzusha (anzisha kitu kipya ghafla; anzisha na sambaza taarifa za uzushi) 'mapya' kama watakavyo.

Kila lugha ina maandishi na matamshi yake. Lugha inapokosewa kuandikwa, huweza kumtatanisha msomaji kutoelewa maana iliyokusudiwa au kuleta maana tofauti. Kwa mfano, 'gamu' ni neno tofauti kabisa na 'ghamu' kwani maana ya 'gamu' ni uzito wa kufanya jambo kutokana na hisia ya woga au hofu wakati 'ghamu' ni majonzi. Lugha ina maneno yasiyokuwa na wingi kama maji, mate, taa, siku n.k. Kwa sababu hiyo wingi wa 'maji' ni maji badala ya 'mamaji' au 'mimaji.' Pia 'mate' yawe kidogo au mengi hubaki kuwa mate tu. 'Taa' moja husemwa 'taa hii' na nyingi huitwa 'taa hizi.' Kusema 'mataa' si Kiswahili. Kadhalika 'siku moja' yaitwa 'siku hii' na zaidi ya moja husemwa 'siku hizi.' Hakuna 'masiku' kama isemwavyo mitaani.

Kwa utaratibu huo, wingi wa 'kitu' ni 'vitu' na si 'mavitu' au 'mavituz' kama iandikwavyo kwenye magazeti ya michezo, tena kwa upotoshwaji mkubwa. Kwa hakika neno 'kitu' lina maana nne: i) jambo; ii) mali au fedha; iii) mnyama mweusi wa jamii ya paka na iv) ni chochote ambacho si mtu au mnyama. Sasa soma lugha 'mpya' ya waandishi wa magazeti ya michezo: "Zahera aleta Yanga SC mavitu ya AFCON." Vitu ni wingi wa 'kitu' kama nilivyoeleza hapo juu. Waandishi wa michezo hupenda sana kutumia neno 'mavitu' kwa maana ya wacheza kandanda mahiri, kumbe ni sitiari (matumizi ya neno kwa maana isiyokuwa ile ya msingi).

"Simba mpya kujifua Uturuki." Neno 'jifua' hutumiwa sana na magazeti ya michezo, tofauti na maana yake halisi. 'Fua' ni neno lenye maana sita; i) rangi ya kahawia inayopatikana kwenye mizizi ya miti inayotumika kupikia kili (wingi wa ukili); utepe mpana uliosukwa kwa chane za ukindu, muwaa au kiwanda.

'Fua' ii) kutengeneza vyombo au mapambo kwa kutumia madini; iii) kuondosha makumbi kwenye nazi kwa kifulio; iv) kutoa taka kwenye nguo kwa maji na sabuni; v) kumfanyia mtu dawa ili kuondoa nuhusi/nuksi na vi) kutoa taka kutoka kwenye kisima.

Haieleweki wacheza kandanda hujifuaje kama nguo! Au huenda ughaibuni kutengeneza vyombo vya mapambo au kuondosha makumbi kwenye nazi kwa kifulio au kufua madafu? Kutoa taka kwenye nguo kwa maji na sabuni? Kuwafanyia watu dawa ili kuwaondolea nuhusi au kutoa taka kwenye visima!?

Sasa waandishi washindwa hata kuandika mtiririko mzuri wa sentensi zao! "Kama ulidhani Simba pekee yake ndiyo itawakilisha Bara Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, basi maamuzi ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) huenda yakakushutua."

Si 'shutua' ni shitua. Maneno 'pekee yake' hayaendani pamoja. Maana ya 'pekee' ni bila -ingine, peke yake; pweke. 'Peke' ni bila mwenzi, -enyewe tu; bila kuwepo -engine. Neno 'yake' lina maana mbili: i) kivumishi kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja; ii) kiwakilishi kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja.

Kwa hiyo mwandishi hakuwa sahihi kuandika: "Kama ulidhani ni Simba pekee yake ndiyo itaiwakilisha Bara Ligi ya Mabingwa ... basi uamuzi wa ..." (Nimetumia neno sahihi 'uamuzi' badala ya maamuzi.) Badala yake angeandika" "Kama ulidhani ni Simba pekee ..." au "Kama ulidhani ni Simba tu ndiyo itakayoiwakilisha Bara ..."

"Juzi kati kwa pamoja jamaa walisema kwa upande wao wachezaji kuumwa ugonjwa unaotisha hivi sasa (Dengue) kuwa wanapenda sana kuvaa vipensi ndiyo sababu kubwa ya kuumwa na mbu huyo anayeuma mchana." Hii ni taarifa ya mwandishi wa michezo alipowahoji wachezaji Ndemla na Ajib kuhusu ugonjwa wa Dengue. 'Juzi' ni siku moja iliyopita kabla ya jana. Nielewavyo ni kuwa kuna 'juzi asubuhi,' 'juzi mchana,' 'juzi jioni' na 'juzi usiku.' Hili la 'juzi kati' silielewi ingawa latumiwa sana na waandishi.

"Manara aingia chaka Taifa" ni kichwa cha habari kwenye gazeti la michezo kilichofuatiwa na habari: "Umewahi kuona mtu akipotea kwao? Ndivyo ilivyomtokea Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba Hajji Manara alipoingia Uwanja wa Taifa na moja kwa moja kwenda katika jukwaa la mashabiki wa Simba na kukutana na mashabiki wa Yanga, huku wale wa Simba wakikaa upande wa Yanga." Uwanja wa Taifa hauna msitu wenye msongamano wa miti. 'Chaka' ni neno lenye maana mbili, tofauti na lilivyotumiwa na mwandishi. Maana ya kwanza ya 'chaka' ni sehemu ya msitu yenye msongamano wa miti na mimea; mahali penye mkusanyiko wa majani na miti mingi iliyosongamana. Kuna methali isemayo 'chaka la simba halali nguruwe.' Pia ni majira ya jua kali na joto; kipindi baina ya Desemba hadi Februari; kaskazi.

Mwandishi pia katumia neno 'vipensi' linalonitia bumbuazi (mshangao mkubwa unaomfanya mtu awe kimya na asijue la kufanya). Kwani aliona wasomaji wasingeelewa kama angeandika 'nguo fupi' badala ya 'vipensi'?

Methali: Tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

NA FRANSISKO MPANGALA

# Mahakama na nafasi yake kulinda mazingira nchini

MOJA ya vitu muhimu kwenye maisha yetu ya kila siku ni kuwa na mazingira safi na salama.

Kwa kulitambua hili, zimekuwapo juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira nchini.

Hatua hizo ni pamoja na kusimamia na kutekeleza sera, sheria, mikakati na mipango mbalimbali ya kuhifadhi mazingira, kutoa elimu kwa umma ya namna gani wanaweza kulinda mazingira pamoja na kusaini mikataba ya kimataifa yenye lengo la kulinda mazingira nchini.

Juhudi hizi za serikali zinalenga kukabiliana na hali halisi ya kimazingira isiyoridhisha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NAFORMA (National Forestry Resources Monitoring and Assessment) inabainisha kuwa nchi inapoteza takriban hekta 372,000 za misitu ya asili kila mwaka.

Taarifa hii inaonyesha kuwa endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa, kuna hatari nchi yetu ikageuka jangwa siku za usoni.

Kama uharibifu wa mazingira hautadhibitiwa, basi tutarajie majanga yanayosababishwa na ukame kuongezeka, vyanzo vya maji kuzidi kuharibika, mvua kutotabirika, rutuba ya ardhi kupungua na afya za watu kuendelea kuwa hatarini.

Kwa maana hii, pamoja na kuwapo juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kulinda mazingira, ipo haja ya mihimili mingine ya dola kuzidi kutumia mamlaka zake kuiongeza nguvu serikali.

Moja ya mhimili wa dola unaoisaidia serikali kulinda mazingira ni Mahakama.

Mahakama inayo nafasi ya kutoa mchango mkubwa wa kulinda mazingira nchini.

Makala hii itatoa elimu na kufafanua ni kwa namna gani Mahakama inaweza kulinda mazingira.

**MAANA YA MAHAKAMA**

Mahakama ni moja ya mihimili mitatu ya dola. Ina mamlaka ya kutoa maamuzi katika migogoro baina ya pande mbili, kusimamia utawala wa sheria na kufanya maamuzi kuhusu mashauri ya jinai na madai kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mahakama ni mhimili ulio na kauli ya mwisho katika utoaji wa haki nchini. Hii ni kwa mujibu wa ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Yawezekana msomaji wa makala hii ukajiuliza, kama jukumu kuu la Mahakama ni kutoa haki, Je ni kwa namna gani chombo hiki cha kutenda haki kinaweza kulinda mazingira nchini?

Mahakama inalinda mazingira kwa namna mbili.

**ZUIO**

Kwanza, Mahakama ina mamlaka ya kutoa zuio dhidi ya shughuli zozote zinazohatarisha afya za watu au kusababisha uharibifu wa mazingira.

Katika kesi ya Festo Belegele

> “
> Ieleweke kuwa si lazima mtu asubiri mpaka shughuli za kuharibu mazingira zianze ndipo akimbile mahakamani. Mtu anaweza kwenda mahakamani kuomba zuio la kimahakama akijiridhisha kuwa zipo dalili za wazi na ushahidi wa kutosha kuwa mhusika fulani ana mpango wa kuharibu mazingira kutokana na shughuli anazotaka kufanya.



Jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

dhidi ya Baraza la mji wa Dar es Salaam (Mahakama Kuu ya Tanzania, Kesi ya Madai namba 90 ya mwaka 1991), Mahakama ilieleza kuwa kitendo cha Baraza la Mji kutupa taka na uchafu kwenye maeneo ya Kunduchi Mtongani, kilikuwa kinyume na Sheria za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Pia, kitendo cha Baraza la Mji kutupa taka eneo la Kunduchi Mtongani kilikuwa kinyume na Mwongozo Mkuu wa Mji, kwani mbali na kuwaletea kero na usumbufu wakazi wa maeneo hayo, kilihatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo.

Mahakama ilitoa amri kwa Baraza la Mji kusitisha mara moja zoezi hilo la utupwaji taka na uchafu kwenye maeneo ya makazi ya watu kwa kuwa kitendo hicho kilihatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo na kilikuwa kinyume na ibara ya 14 ya Katiba ya nchi inayotoa haki ya ulinzi wa maisha kwa wananchi wote.

Kupitia hukumu hii, tunaona kuwa Mahakama ina mamlaka ya kuzuia shughuli zozote zinazoharibu mazingira kupitia maombi yanayoletwa mbele yake.

Ieleweke kuwa si lazima mtu asubiri mpaka shughuli za kuharibu mazingira zianze ndipo akimbile mahakamani. Mtu anaweza kwenda mahakamani kuomba zuio la kimahakama akijiridhisha kuwa zipo dalili za wazi na ushahidi wa kutosha kuwa mhusika fulani ana mpango wa kuharibu mazingira kutokana na shughuli anazotaka kufanya.

**FAIDA**

Faida kubwa ya mazuio haya ya Kimahakama ni kuepusha mazingira kutoharibiwa kabisa au kutoharibiwa zaidi.

**ADHABU**

Pili, Mahakama inalinda mazingira kupitia adhabu za vifungo au faini (au vyote kwa pamoja) inazotoa kwa watu, kampuni au taasisi mbalimbali zinazokutwa na hatia ya kuharibu au kuchafua mazingira kinyume na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Adhabu hizi za faini na vifungo hutolewa na Mahakama kwa lengo la kubadili tabia ya mkosaji, kumfanya mkosaji ajutie kuharibu mazingira na kumpa elimu mkosaji kuwa vitendo vya kuharibu mazingira haviruhusiwi kwa mujibu wa sheria.

Isitoshe, adhabu zinazotolewa na Mahakama hutumika kama mifano kwa watu wengine kwenye jamii kuwa endapo wataharibu mazingira kinyume na sheria ya mazingira, watakabiliana na adhabu kali kama walizopewa wakosaji wengine waliokutwa na hatia ya kuharibu mazingira.

Adhabu hizi zinazotolewa na Mahakama zina faida katika kulinda mazingira kwa kuwa zinaelimisha, zina adabisha na kujenga hofu kwa watu kuwa wakiharibu mazingira kinyume na Sheria ya Mazingira ya

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA RAPHAEL KIBIRITI

## RAIS MPYA WA SERIKALI MUHAS:

# Miundombinu ikiboreshwa vijijini madaktari wote watakwenda huko

WIKI iliyopita tuliwaletea sehemu ya kwanza ya mazungumzo aliyoyafanya Rais mpya wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Costantine Alex Ntanguligwa na Nipashe juu ya masuala mbalimbali katika sekta ya afya.

Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, Rais huyu anazungumzia masuala mbalimbali yakiwemo ya nini kifanyike ili madaktari wasikwepe kwenda maeneo ya vijijini kuliko na asilimia 70 ya Watanzania wote takribani milioni 55.

Endelea na mahojiano hayo ambapo Ntanguligwa anaanza kufafanua changamoto za rasilimali watu, vifaa tiba na siasa kuingia kwenye kada ya afya.

**SWALI:** Unaweza kuzifafanua zaidi changamoto hizi?

**JIBU:** Tukianza na changamoto ya wataalamu, pengine tatizo hili linaanzia kwenye ajira. Kwamba watu hawaajiriwi wa kutosha kwani kwa sasa hali yetu siyo nzuri sana kama taifa. Bado madaktari wetu wanaona watu wengi sana na hali hii inaifanya sekta yetu ya afya kuwa ni ya watu kama wakujitolea. Hata hivyo uzuri ni kwamba tunapokuwa trained(kwenye mafunzo), tunafundishwa kukutana na hali kama hizo. Kwa hiyo utaona watu wengi hawapendi kwenda vijijini, watu wote wanataka kukaa mjini. Na kimsingi, huduma zetu za afya vijijini bado ziko duni sana. Zinahitaji kuendelezwa kwa kiasi kikubwa. Sasa kwa minajili ya raslimali watu, nchi yetu inapata watumishi wengi sana wa afya wanaomaliza kila mwaka tofauti na miaka ya zamani.

**SWALI:** Sasa shida hapo iko wapi?

**JIBU:** Shida inakuja serikali ina uwezo wa kuajiri kwa kiasi gani ili kuendana na matakwa ya wananchi pengine katika viwango ambavyo Shirika la Afya Duniani (WHO) linavihitaji? WHO inashauri daktari mmoja aone walau wagonjwa 300, lakini kwa Tanzania daktari mmoja anahudumia wagonjwa 20,000. Hata hivyo, wanaohitimu kwa miaka ya sasa nchini ni wengi tofauti na miaka ya nyuma. Vilevile tukiangalia vifaa tiba, utaona mwisho wa siku ni matatizo ya kimfumo na serikali nafikiri ina wajibu sasa wa kuhakikisha dawa, vifaa vinatosha. Kwa kweli ukienda vijijini utakuta hali si nzuri na vifaa vya msingi kabisa unaweza ukakuta vinakosekana. Kwa hiyo niisihi serikali pengine kama inasikia itafute namna ya kuhakikisha madaktari wanapatiwa vifaa vya kufanyia kazi.

**SWALI:** Ulitaja mambo matatu, la tatu nalo unalielezeaje?

**JIBU:** Jambo la tatu ambalo nimeliongelea ni kuhusu matumizi ya siasa katika taaluma ya afya.



Rais wa Serikali mpya ya MUHAS, Constantine Alex Ntanguligwa. **(PICHA:MTANDAO)**

Niseme kuwa siasa ni sehemu ya maisha. Wote tunazaliwa kwenye siasa, tunakulia kwenye siasa, siasa inatuathiri kila siku, lakini lazima tuwe na utaratibu wa siasa kwenye sekta ya afya, kuanzia kwa policy makers (watunga sera) wanaotengeneza hizi sera zetu za kiafya. Hivyo tatizo linaanzia kwenye wizara, kwamba matatizo yanaanzia huko kunakowekwa vipaumbele. Nashukuru kwa mwaka huu bajeti ya afya imeongezeka na itafanya mambo makubwa.

**SWALI:** Kwa hiyo mambo yatakuwa mazuri?

**JIBU:** Inategemea kwenye resource mobilization, resource allocation (upatikanaji na ugawaji wa rasilimali), kote huko kuna haja ya kufanya kitu. Lakini kama nilivyosema wanasiasa hawapaswi kuiingilia taaluma kupitia, matamko yao mfano yale yaliyotolewa Iringa na Arusha, yanakuwa yanatuathiri na kutukatisha tamaa kwa namna moja au nyingine.

**SWALI:** Hivyo ushauri wako ni upi kwa upande huo?

**JIBU:** Kwa hiyo ninawasihi wataalamu wa afya kujiingiza zaidi kwenye siasa kwa sababu tunachokiona ni matokeo ya sisi kuwa nyuma. Kwamba ukiwa na mwanasiasa anayeelewa taaluma vizuri, anakuwa na uwezo wa kudhibiti na kuratibu vitu vizuri zaidi kuliko kukaa nyuma kama watalamu wa afya na kuwaachia wanasiasa wafanye wao, matokeo yake wanatulazimisha tufanye kazi kisiasa kuliko taaluma yetu.

**SWALI:** Hebu tueleze wewe ni mwanafunzi wa udaktari unasomea nini sasa, uko mwaka wa ngapi na kwa nini uliamua kusomea udaktari?

**JIBU:** Eee ahsante.. Swali la kwa nini niliamua kusomea udaktari huwa kuna msemo mmoja kwamba kila mmoja hapa unayemuona kuna sababu iliyofanya asomee udaktari. Eee wanasema, kila mtu ana stori yake, kwangu mimi naamini udaktari ni zaidi ya kazi ila ni wito kama ilivyo miito mingine. Kwamba kuwa daktari unaitwa na pengine inaanzia na baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo baraka hizi na wito huu unaweza kukupitia kwa namna tofauti. Mimi nilizaliwa nikakulia katika familia ambayo mama ni mwalimu na baba ni mhandisi, lakini unaweza ukashangaa mwisho wa siku nimetamani kuwa daktari. Kwa kweli nikiwa shule ya msingi, nilipenda kuwa Mhandisi kama baba yangu na nilikuwa najiita Mhandisi Ntanguligwa mpaka nilipofika kidato cha tatu ndipo nilipobadilisha mawazo. Ni vyema tufahamu pia dunia yetu ni ya utandawazi sasa, hivyo unaweza ukakutana na mtu akaku-inspire (hamasisha) kwa namna tofauti.

**SWALI:** Kwa hiyo kuna mtu wewe aliyekuhamasisha?

**JIBU:** Ni kweli, mmoja wa watu aliye nihamasisha kuwa daktari ni mjomba wangu aitwaye Dk. Floridus Ndokoye. Nimekuwa nikimuona na amekuwa akinihamasisha kuwa daktari. Lakini vilevile kunakuwa na ile sauti



Wahitimu wa astashahada, stashahada, shahada za awali na shahada za uzamili katika upande wa afya wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), wakila kiapo cha uaminifu wakati wa mahafali ya 12 yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

ya ndani ikiniambia juu ya wagonjwa, watu wanapata shida za kiafya na walau unaona ufanye kitu. Hivyo niliamua kuchukua mchepuo wa sayansi, yaani Fizikia, Kemia na Bailojia (PCB). Hata hivyo safari hiyo haikuwa nyepesi kwa sababu ilifika kipindi nikatamani kuhamia PCM (Fizikia, Kemia na Hisabati). Nashukuru Mungu nilipata walezi wazuri darasani shuleni, walimu wakanitia nguvu. Nashukuru mpaka leo niko hapa mwaka wa nne, nasomea udaktari na Mungu akipenda kama inavyoonekana hapa, tunatarajia tuje kuwa watunga sera katika sekta yetu ya afya.

**SWALI:** Sehemu kubwa ya wananchi wa Tanzania, takribani asilimia 70 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 wanaishi vijijini. Hata hivyo madaktari wengi hawapendi kufanyia kazi vijijini, unalizungumziaje suala hili?

**JIBU:** Eeee hapa swali la kwanza inabidi tujiulize ni kwa nini hawa madakatari hawapendi kwenda vijijini? Kwa sababu ukishajua ni kwa nini hawapendi kwenda huko unaweza ukatoa solution (suluhisho). Kama nilivyosema awali bado katika vijiji vyetu kuna hali duni sana ya kimaisha. Hivyo hatua ya kwanza inayotakiwa kufanyika ni kuhakikisha tunapeleka miundombinu ya kutosha katika vijiji vyetu.

**SWALI:** Kwa nini unasema hivyo?

**JIBU:** Kwa sababu huyu daktari mbali na kuwa kazi hii ni ya wito, bado na yeye anatamani kuwa na maisha mazuri, anatamani kukaa sehemu yenye barabara nzuri, sehemu yenye vifaa ili anapotaka kusaidia watu aweze kufanya hivyo. Anatamani kukaa sehemu yenye umeme, maji na kadhalika. Kwa hiyo hatua ya kwanza kabisa ukitaka kushawishi watu kwenda vijijini, ni ya kuhakikisha kama serikali kuna mpango wa kuendeleza vijiji kuwa katika hali nzuri ya kimaisha ya miundombinu yenye mahitaji yote yanayotakiwa. Hivyo, ninaamini hiyo ndiyo muhimu na tukiwa na hivi vyote sidhani kama kuna mtu atakwepa kwenda vijijini. Binafsi napenda sana kuishi vijijini kwa sababu maisha ya kule siyo ya gharama kama ilivyo mjini na ukianzisha programu zako huko ni rahisi kufanikiwa kama mtu aliye mjini.

**SWALI**: Sasa shida hapo ni nini?

**JIBU:** Ukiangalia hapo shida ni kwamba huyu anakaa mjini na anacholipwa ni kilekile sawa na huyu anayekaa kijijini. Hivyo mtu anajiuliza kwa nini aende kijijini kwenye maisha magumu wakati mshahara ni uleule na stahiki ni zilezile? Ninaamini tukiendeleza vituo vya afya vijijini, vikawa katika hali nzuri na kumtengenezea mazingira mazuri daktari, mimi ninaamini huko kunaweza kukashawishi wataalamu wetu wa afya kukaa huko, kuliko tukibaki kulalamika kwa nini hawaendi vijijini. Ninaamini kama kuna maji, kama kuna miundombinu mizuri, barabara, umeme, idadi ya wale wasiopenda vijijini itapungua kwa kiasi kikubwa.

**SWALI:** Tuongelee urais wako... mipango yako ni nini, ajenda yako ni nini na unataka utakapokabidhi madaraka baada ya urais wako, MUHAS ikukumbuke kwa lipi?

**JIBU**: Eee unapoongelea nitaifanyia nini MUHAS, ni suala ambalo limegawanyika katika mambo mawili. Jambo la kwanza ni majukumu ya lazima ambapo kama serikali lazima iyatimize mfano kusimamia taaluma ya wanafunzi na changamoto ya mikopo. Watu wanakosa mikopo na changamoto nyingine za maisha kama makazi ambayo ni changamoto kubwa sana. Ninawasihi wadau kama wananisikiliza, kuna changamoto kubwa ya makazi hapa. Kwa hiyo kama kuna namna yoyote ambayo wadau tunaweza kushirikiana tufanye hivyo. Kwa mfano wenye nyumba maeneo ya karibu ambao tunaweza tukazifanya zikawa sehemu ya kuishi wanafunzi wetu, tutafurahi sana kuwapata.

**SWALI:** Changamoto nyingine?

**JIBU:** Vilevile tuna changamoto kubwa ya wanafunzi wanaokosa mikopo ambayo kama serikali mwaka huu tumeahidi tutafanya kila namna kusaidia. Lakini pia kama kuna wadau wananisikiliza wanaweza wakafadhili wanafunzi wetu. Lingine ni la majukumu ya msingi kabisa ambayo hata katiba yetu inatuelekeza tufanye nini. Kwamba lazima tusimamia wanafunzi na kuhakikisha mahitaji na haki zao hazidhulumiwi na kwamba kuhakikisha taaluma inaenda kama inavyokusudiwa.

**SWALI:** Kuna lingine katika hili?

**JIBU:** Ndiyo kwa maana kuwa ninapenda kuhakikisha kwamba tunatengeneza viongozi wa baadaye na hiyo ni goal (lengo) yangu kubwa. Tunatengeneza kwa namna gani, cha kwanza nataka kutengeneza uongozi wa mfano ambao utakuwa wa maadili. Uongozi ambao utakuwa unagusa maisha ya watu, wa haki na kila mtu afurahie na mwisho wa siku tuhakikishe kwamba hawa wanafunzi wetu tukiachana na majukumu yetu ya msingi, tuwatafutie fursa nje na pia tukitangaze chuo chetu kwa kutumia vipaji mbalimbali ambavyo wanafunzi wetu wanavyo. Kuna watu ambao wanafanya innovations (ubunifu), wana idea (mawazo) nzuri tu. Kwa mfano tulifanya symposium ya artificial intelligence in health care (Mkutano wa ubunifu kwenye huduma za afya) ulipokelewa vizuri sana na wadau. Kwa hiyo lengo pia ni kuhakikisha tunawatafutia fursa wanafunzi wetu, kwamba ukiachana na taaluma, Universities ni universal (a-kiulimwengu) hivyo lazima wawe na kitu cha ziada. Kwa hiyo kuwajengea uwezo wanafunzi wetu wa kupata vitu extra (vya ziada), waonyeshe vipaji vyao, uwezo wao katika kutatua matatizo mbalimbali katika nchi yetu. Kwa hiyo tunataka wanafunzi wetu wawe sehemu ya kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya afya nchini.

**SWALI:** Watu wangependa kumfahamu huyu Rais wa serikali mpya ya MUHAS, ni nani, ametokea wapi hadi hapa alipo, unaweza kutupa historia yako?

**JIBU:** Ahsante sana, kwa majina naitwa Constatine Alex Ntanguligwa.Nimezaliwa Dar es salaam, Hospitali Kuu ya Jeshi ya Lugalo na nimelelewa na wazazi wangu ambao mpaka sasa bado wako hai, mama ni Mwalimu, baba ni Mhandisi. Elimu yangu ya msingi nimeipata hapa hapa Dar es Salaam, Shule ya Msingi Mwenge, baadaye nikasoma Shule ya Msingi Canossa kidogo na mwisho St. Marys-Mbezi. Nilibahatika kwenda seminari kipindi ambacho nilikuwa natamani kuwa Padre. Nilianza kidato cha kwanza pale Visiga. Safari yangu ya uongozi kwa kweli ilianzia toka nikiwa shule ya msingi, madarasa yote ambayo nimesoma nilikuwa kiranja wa darasa, hata nilipofika sekondari, kidato cha kwanza nilikuwa kiranja wa darasa. Kidato cha pili nikawa kiongozi wa maktaba na nilipofika kidato cha tatu nikawa kaka mkuu msaidizi. Nilienda kidato cha tano na sita shule ya sekondari Msolwa, nilikaa Ilboru kidogo, lakini nilirudi tena Msolwa na kule nilikuwa mwenyekiti wa tume ya uchaguzi. Hatimaye ndoto yangu ya muda mrefu ya kuwa daktari niliianza mwaka 2015, nilipojiunga na MUHAS. Kama kawaida ndoto ile ya uongozi ilianza kuchipua tangu mapema sana.

**SWALI:** Kivipi?

**JIBU:** Nilipofika hapa nilikuwa mwakilishi wa darasa mwaka wa kwanza na mwaka wa pili niliingia kwenye Bunge nikiwakilisha wanafunzi. Aidha, nikateuliwa kuwa naibu waziri mwaka huo na nikafanya kazi yangu kwa kadri Mungu alivyonijalia. Mwaka huo huo niliamua kugombea umakamu wa rais ingawa kura hazikutosha lakini haikunikatisha tamaa. Kuingia mwaka wa tatu nilipumzika siasa kidogo, lakini wanaMUHAS wakaniamini nikawaomba kuwa mwenyekiti wa kitivo cha udaktari ambacho kina wanafunzi wa udaktari, maabara na mionzitiba na nikawa mwenyekiti wa wanafunzi wote hao. Mwaka huu wa nne wa udaktari nimeamua kugombea urais na ninashukuru wanaMUHAS wamenidhamini kwa kishindo kabisa, kwani kihistoria haijaweza kutokea kwa rais kushinda kwa asilimia 76. Nashukuru Mungu kwa sehemu zote ambazo nimekuwa kiongozi watu wamekuwa wakipenda uongozi wangu, kwani nimekuwa nikigusa maisha ya watu. Lakini niseme tu kama umezaliwa kuwa kiongozi utaona ile mbegu inamea.

**SWALI:** Kwa nini unasema hivyo?

**JIBU:** Nasema hivyo kwamba pamoja na changamoto zote nilizopitia katika safari ya uongozi leo hii tuko hapa. Natamani baadaye nimalize udaktari wangu, nijiendeleze katika taaluma kwa sababu ninaamini uongozi ni kama kipaji, ni sawa na mchezaji mpira, unaweza kuwa daktari na ukawa mchezaji mpira mzuri. Kwa hiyo vilevile nina mpango wa kujiendeleza katika taaluma yangu ya udaktari na hata kuwa daktari bingwa na kwa upande wa pili kujiendeleza katika fani ya uongozi kwa kufanya kozi mbalimbali za uongozi na pengine Mungu akipenda kuingia katika siasa za nchi.

**SWALI:** Tanzania imejielekeza katika uchumi wa viwanda, ikilenga kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025, unazungumziaje hili katika jicho la afya?

**JIBU:** Tunapoongelea Tanzania ya viwanda katika sekta ya afya, tunaongelea mambo mengi. Jambo la kwanza kutoka kwenye neno lenyewe la Tanzania ya viwanda, ifike wakati sasa kwamba upungufu wa vifaa na baadhi ya vitu katika hospitali zetu, unaotokana na sisi kutegemea sana wenzetu kuliko sisi wenyewe ukome. Tuna viwanda hapa vinatengeneza dawa, vingeendelezwa na pengine kuletwa vingine. Kwa mfano issue kama drip na water injection, sidhani kama kuna haja sana ya sisi kuagiza kutoka nje, kwani tuna maji ya kutosha. Tunaweza kutengeneza vifaa hivi, vitu basic kabisa ambavyo vinahitajika katika hospitali zetu.

**SWALI:** Una maana gani?

**JIBU:** Ninaamini kabisa kama nchi tukijipanga tukawa tunatengeneza wenyewe kama nchi na kupunguza gharama ya kutengeneza hivi vifaa kwa sababu kama vinatengenezwa hapa itakuwa ni vyema zaidi kwa sababu vitapatikana kwa wingi kwa kutengenezwa hapa. Lakini kwenye sekta ya afya, tuna vitu artificial intelligence, yaani uendelezaji wa kiteknolojia. Kuna vijana wengi wenye idea nzuri na kubwa za kutatua matatizo katika sekta ya afya kwa kutumia teknolojia. Naamini tunapoongelea Tanzania ya viwanda, tunaongelea vijana wa namna hiyo kwani wapo vijana hapa wana idea nzuri za kuleta solution katika sekta yetu ya afya. Kwa mfano kuna kampuni zimeanzishwa na wanafunzi hapa, moja inarahisisha kugawa dawa mbalimbali. Lakini kuna idea za wanafunzi wetu kama daktari mkononi, ambayo inatoa huduma ya afya kwa wananchi kwa kupitia mitandao ya simu, mitandao ya kijamii na vitu kama hivyo. Kama nchi tunaweza kuwekeza katika eneo hilo pia na kwamba sasa tunaelekea katika teknolojia ya viwanda, tukawekeza katika eneo kama hili ili kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wetu. Naamini kwamba tunapoelekea kuwa nchi ya kipato cha kati 2025, tutaweza kuboresha walau miundombinu katika hospitali zetu, kuweka vituo vya afya na mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa madaktari wetu na wataalamu wetu wa afya. Ninaamini kama nia ya dhati ya Rais wetu John Magufuli ikitimia, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana katika kuendeleza sekta ya afya kwenye Tanzania ya viwanda.

# Mahakama na nafasi yake kulinda m

Inaendelea Uk. 15

mwaka 2004, watakabiliwa na adhabu kali na hivyo kufanya watu kuacha kuharibu mazingira kinyume na sheria.

Mbali na kusaidia kulinda mazingira, Mahakama pia inasaidia kutoa fidia kwa watu mbalimbali wanaoathiriwa na shughuli za kuchafua au kuharibu mazingira.

Fidia hizi zinatolewa pale tu Mahakama inapojiridhisha kuwa vitendo vya watu, taasisi au kampuni kuchafua au kuharibu mazingira vimehatarisha afya na vimeleta usumbufu kwa wananchi kwenye maeneo yao.

CHANGAMOTO

Zipo changamoto mbili zinazoikabili Mahakama katika kuitumia nafasi yake kulinda mazingira nchini. Kwanza, kuna idadi ndogo ya Mahakama nchini.

Kwenye utafiti uliofanyika kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kata zilizopo nchini ni 3,957. Mahakama za mwanzo zipo katika kata 976 tu kati ya kata 3,957.

Hii ni kama asilimia 24.6 ya kata zote nchini ndio zinazopata angalau huduma ya Mahakama ya Mwanzo.

Ingawa hizi ni takwimu za mwaka 2015 na huu ni mwaka 2019, sidhani kama kuna ongezeko kubwa la idadi ya Mahakama kiasi cha kuathiri hoja yangu kuwa kuna idadi ndogo ya Mahakama nchini.

Hii inasababisha watu kwenda umbali mrefu, kutumia muda mwingi na wakati mwingine kuingia gharama (nauli) kuzifikia Mahakama zilizo mbali na maeneo yao.

Uchache huu wa Mahakama hautengenezi mazingira rafiki kwa Watanzania wengi kupata huduma ya haki ya kufungua mashauri yanayohusiana na uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Changamoto ya pili ninayoiona ni kuwa bado kuna mwamko mdogo wa watu kupeleka mashauri ya Kimazingira mahakamani.

Hii inatokana na ukweli kuwa bado watu wengi wana uelewa na mwamko mdogo wa kulinda mazingira nchini.

Katika mazungumzo niliyoyafanya na hakimu mfawidhi wa moja ya Mahakama nchini, alikiri

JE, WAJUA?

# ‘Mtoto Detmold’ maiti iliyoishi miaka 6,500

ANAFAHAMIKA kama ‘Mtoto Detmold’, kwa miaka 6,500 amekua akiishi kama maiti pekee ya mtoto mchanga iliyohifadhiwa kwa kukaushwa kwa muda mrefu zaidi kwenye historia ya ukaushaji wa maiti.

Maiti ya mtoto huyo aliyefariki akiwa na umri wa kati ya miezi minane na miezi tisa, awali ilikuwa ikihifadhiwa kienyeji na wakuu wa kimila nchini Peru ambao walikuwa wakikabidhiana kizazi kwa kizazi kwa miaka 4,480 Kabla ya Kristo.

Kilichosababisha maiti ya mtoto huyo kuhifadhiwa namna hiyo, ni mazingira mazima ya kuzaliwa kwake ambayo kwa elimu ya watu hao wa kale haikuweza kuwapa majibu ya kisayansi zaidi ya kuamini elimu zao za kimizimu.

Alizaliwa akiwa na moyo mkubwa uliotokeza nje ya kifua chake na kuufanya uonekane kama umehifadhiwa kwenye mfuko wa nailoni huku ukiendelea kudunda. Fuvu la kichwa chake nalo lilikuwa ni refu zaidi kuanzia utosini hadi kushuka kidevuni tofauti na fuvu la mtu wa kawaida.

Kwa nyakati hizo, milenia tatu zilizopita, muonekano wa mtoto huyo haukuwa na tafsiri nyingine zaidi ya muujiza wa kimiungu. Wakuu wa kimila wa Peru, nchi iliyopo Amerika ya Kusini, wakaanza kuzungumza na mizimu yao ili wapate njia ya kuishi na kiumbe huyo.

Matambiko na mambo mengine ya kimila yakafanyika, na alama kadhaa zinajionyesha kwenye maiti ya mtoto huyo ikiwemo hirizi kubwa ya mfupa wa mnyama aliyofungwa na kuning’inia kufuani pake.

Kwa muda mrefu mwili huo umekuwa ikihifadhiwa katika makumbusho ya Volkerkundliches, jijini Witzenhausen nchini Ujerumani kabla ya kuhamishiwa kwenye mji wa Lippe State katika Jiji la Detmold pia nchini Ujerumani.

Na baada ya miaka mingi ya kuishi kama mwili wa muujiza na unaotizamwa kimazingara zaidi, hatimaye mwili huo ulipelekwa nchini Marekani na kufanyiwa vipimo vingi vya kisayansi vilivyosaidia kujua mengi zaidi juu ya maisha mafupi ya mtoto huyo.

Uchunguzi huo umeonyesha kuwa kifo cha mtoto huyo kilitokana na vichomi kilichosababishwa na matatizo ya moyo wake huku pia akikabiliwa na tatizo la kupumua.

Kwa kutokuyajua yote hayo, wazee wa kimila wa Peru waliamini kuwa mtoto huyo alikuwa miongoni wa watakatifu wa kimiungu yao na walipomzika walimzika kwa maziko yote ya kimila wanayofanyiwa viumbe vyenye nguvu za kimungu kwa kumkunja kama anavyoonekana katika picha ikiwa ni sawa na ishara ya sanamu kadhaa zenye kuabudiwa na baadhi ya watu wa Amerika ya Kusini.




‘Mtoto Detmold’ akiwa katika muonekano wake kwenye makumbusho. **PICHA: MTANDAO**

# UTAFITI

## UTAFITI: UPUNGUFU WA MBEGU ZA KIUME UNAHATARISHA MAISHA

WANAUME wenye mbegu chache za kiume wako katika hatari ya kupata magonjwa kwa mujibu wa utafiti mpya.



Wapenzi wakitazama matokeo ya ujauzito. **PICHA: MTANDAO**

Utafiti uliofanyiwa wanaume 5,177 ulibaini kwamba wanaume wenye mbegu chache za kiume wana mafuta mengi mwilini, shinikizo la damu na mafuta machafu katika mishipa ya damu.

Pia wana uwezo mkubwa wa viwango vidogo vya homoni za kiume. Waanzilishi wa utafiti huo wanasema kuwa, wanaume wenye mbegu chache za kiume ni muhimu wakafanyiwa vipimo vya magonjwa mengine.

Hivi karibuni nchini Tanzania, kumeshamiri matangazo mbalimbali rasmi na yasiyo rasmi kuhusiana na dawa za asili haswa za kuongeza nguvu za kiume.

Miongoni mwa dawa hizo ni dawa ya ‘Ujana’ ambayo kazi yake ni kusaidia kuongeza nguvu za kiume.

Dawa zingine zikiwa Sudhi, Vatari, IH Moon na Coloidal Silver ambazo kazi yake ni kudhibiti vimelea mbalimbali.

Baraza la dawa nchini humo limesema hatua hii imekuja baada ya uchunguzi wa kina uliofanywa na kubaini kuwa dawa hizo hazina madhara kwa afya ya binadamu, hivyo hawana budi kuzikubali.

Aidha, Paul Muhame ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa dawa za asili nchini Tanzania anasema baada ya baraza kupitisha vigezo vyote vilivyohitajika kutoka katika dawa hizo, mamlaka ya dawa na chakula pia imethibitisha hilo.

“Suala la muhimu ambalo tumeliangalia zaidi ni usalama wa mtumiaji...katika upande wa kuthibitisha kuwa dawa hizo zinaponyesha au la, linabaki kwa mnunuaji na mtumiaji wa dawa hiyo,” anasema.

**HATARI**

Upungufu wa mbegu za kiume na matatizo ya ubora wa mbegu hizo ni masuala yanayoathiri mmoja kati ya wanandoa watatu kushika mimba kulingana na utafiti huo uliofanywa nchini Uingereza.

Lakini katika utafiti huu mpya wanasayansi walichanganua wanandoa wasioweza kupata watoto nchini Italia, kujua iwapo ubora wa mbegu hizo pia unaathiri afya ya mtu kwa jumla. Waligundua kwamba wanaume wengi walio na mbegu chache walikuwa na matatizo kadhaa ya kiafya ikiwamo mwili ulionenepa na shinikizo la damu.

Hatua hiyo huongeza hatari ya kupata ugonjwa wa kisukari, magonjwa ya moyo na kiharusi.

Wanaume hao pia walionekana kuwa na viwango vya juu vya kuwa na homoni chache za kiume ambazo hupunguza ukubwa wa misuli na mifupa na huenda vikasababisha ugonjwa wa kudhoofika kwa mifupa. **BBC**

# azingira nchini

kupokea malalamiko na kesi chache zinazohusu mambo ya mazingira.

Alisema kuwa bado mwamko wa kutunza mazingira nchini ni mdogo. Yawezekana hii ikawa ni sababu kubwa iliyonifanya kuandika makala hii ya kimazingira, lengo likiwa ni kutoa uelewa kwa jamii na kuhamasisha watu kutunza mazingira yao.

Pia kutunza na kudai haki zao mahakamani pale inapotokea mazingira yao yanaharibiwa.

Tujifunze kwa wenzetu wanaojilaumu kwa kuzembea na kutochukua hatua mapema hadi maeneo mengi katika nchi zao kugeuka majangwa na kutofaa kwa kilimo, mvua kupotea kutokana na ukatwaji wa miti na madhara mengineyo mengi yanayosababishwa na kutohifadhi na kutotunza mazingira.

*Barua Pepe;*
*fransiscompangala08@gmail.com*



**Na Michael Eneza**

# Makatazo na athari zake katika fikra, mawasiliano na mafarakano kijamii

MOJA ya maeneo magumu katika historia ya fikra na hata maisha ya jamii kwa kawaida ni kuoanisha kile mtu anachojua na kile anachosema, au anachoweza kusema, hali ambayo mara nyingi inafanya iwe vigumu kutofautisha ukweli na uongo.

Kwa vile utamaduni na ustaarabu kimsingi umejengwa katika msingi wa kutofautisha maeneo hayo mawili katika hisia, mazungumzo au dhamira, kuwapo kwa mazingira mapana ambako siyo rahisi kusema kile ambacho mtu anafikiria ni tatizo, kwani inafanya mawasiliano au ubadilishanaji hisia kuwa mgumu, kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Majadiliano kwa mfano katika redio za FM ni kielelezo cha mustakabali kama huo.

Mtaalamu mmoja wa Kiswahili anaulizwa katika majadiliano ya redio ya kujiliwaza na kutafakari vipindi vya asubuhi kuhusu neno 'uhuni,' na anakomalia kutoa maelezo kuwa mhuni ni mtu mwenye umri wa kuoa lakini hajaoa.

Kwa msikilizaji wa kawaida, au tuseme msikilizaji aliyeenda shule, hayo ni maelezo ya mzee wa kijijini labda wa umri wa miaka 65 kama siyo zaidi, ambaye anaona ni kioja mtu mwenye umri hata ingekuwa wa miaka 30 kuwa bado hajaoa, na mbaya zaidi, hana mipango ya kuoa.

Inaelekea maelezo hayo ya kuchukua neno 'uhuni' kuwa ni kutokuoa yalilenga wanaume, na kwa jumla neno hilo linatumika zaidi kwa wanaume, ambayo ni sahihi kiasi tu.

Yako maeneo mengi tu ambako hata mwanamke anaweza kuwa mhuni, kwa maana ya mtu asiyeaminika, asiyekuwa na ahadi au kuweza kutumainiwa kutenda kwa mujibu wa kile alichosema, na siyo udanganyifu hata kwa jambo ambalo anayemsikiliza anajua fika liko hivi au vile.

Kimsingi ni tabia hiyo ya kutokuwajibika katika masuala ambayo yanagusa watu wengine ambako dhana ya 'uhuni' imejichimbia, na siyo kuwa na maisha ya ndoa au hapana, au kuwa na maisha thabiti ya ndoa.



Jamii iliyostaarabika katika mawasiliano. **PICHA: MTANDAO**

Hisia ya kuelekeza neno hilo katika uwepo wa ndoa ni uhafidhina, ambako kuingia katika maisha ya ndoa kwa wakazi wa maeneo ya pwani kijadi ni kama jando kwa makabila mengine hasa ya wafugaji, ambako jando ndiyo inatoa heshima kwa kijana awe na sifa ya kuoa. Pwani anaoa tu.

Yako maeneo mengine ambako uhafidhina unaoendana na makatazo ya kitamaduni kwa jamii za pwani yanafikia mahali yanatawala lugha, iwe ni kwa kuunda neno moja kutumika kwa hisia au dhana fulani kwa lengo la 'kupaka rangi' ili ipendeze au isipendeze, au kufanya uhusiano wa dhana hiyo na neno husika kuwa wa msingi sana.

Moja kati ya maneno kama hayo ni matumizi ya dhana ya 'tendo la ndoa' ambayo ni vigumu kusema ilianza wapi, kwani kwa waliokuwapo zamani hapakuwa na mfumo huo wa maneno ila kugusia kwa mfano 'unyumba,' lugha ya adabu ya kuzungumzia mahusiano ya watu wanaokaa pamoja. Na kwa jumla inatazamiwa kuwa wanakuwa katika ndoa.

Sasa kuinua matazamio hayo iwe ni mfumo halisi wa fikra inakuwa kidogo inaleta matatizo kwani inafikia mahali ambapo mtaalamu wa Kiswahili aliyeingiza neno 'tendo la ndoa' hakuwa anazingatia kuwa anazungumza lugha na siyo anatoa mawaidha katika nyumba ya ibada, ambapo kusingekuwa na ukinzani kuhusu usahihi wa msamiati kama huo.

Ila kuna upande mwingine wa kushangaza, kuwa hao hao (inaweza kutazamiwa) walitunga msamiati wa kuzuia uwezekano wa unyumba au uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa, kwa kuchukulia kuwa ile dhana tu ya kushirikiana kimapenzi inajumuishwa na ndoa, walitunga maneno mengine kukinaisha mazungumzo ya ushirika kama huo nje ye ndoa. Inaelekea 'walitohoa' (kukopa, kutwaa maneno) kutoka lugha nyingine za pwani, kwa mfano neno 'ngono' ambalo si rahisi kujua limetoka wapi, na ni moja ya misamiati ya takriban miaka 20 au zaidi.

Pamoja na matatizo hayo ya kupiga pasi fikra na misamiati ili iendane na kinachotazamiwa na wazee katika jamii fulani, bado ni wazi kuwa ipo juhudi ya kuondoa kabisa matumizi ya maneno yasiyo na staha yasisikike hadharani, na kukiuka kanuni hiyo ni moja ya sababu za ugomvi wa kila siku kati ya chombo cha kudhibiti sanaa, mawasiliano na vijana wanaolenga mashabiki, kugusa hisia zao.

Wanajitahidi kuvuka mipaka wakitazamia kuwa wataeleweka vyema kwa njia moja au nyingine, mara nyingine waponee chupuchupu na mara nyingine inabidi wakumbushwe kuwa kuna mipaka inabidi iangaliwe, ili fedheha isitawale anga ya mawasiliano na kusababisha taharuki.

Tatizo la mawasiliano na makatazo ni kubwa kwa sababu utamaduni kote duniani umejengwa katika misingi miwili ya Torati au Jadi kila mahali, kwani torati ilitolewa kwa watu maalum na wengine walipewa mafunuo au amri zinazoendana na torati hiyo maalum, na mara nyingine hata majina ya watoa amri yanafanana. Kwa mfano mmoja wa watoa amri muhimu wa Israeli ya kale ni Mfalme Sulemani ambaye aliandika vitabu viwili/vitatu vya busara, hasa Mithali na Mhubiri, na jina lake likiandikwa kwa Kiingereza, Solomon, linashabihiana na mtungaji sheria muhimu wa Uyunani, Solon. Alipata sifa kiasi ambacho dhana nzima ya kunukuu ilijengeka katika utamaduni wa Kilatini (eneo la pwani ya Kaskazini ya bahari ya Mediterranean) kuwa ni kukumbusha alichokisema Solon katika suala fulani, kwani Kifaransa, 'selon...' ni 'kwa mujibu wa.'

Katika Kiarabu mtoa sheria muhimu, Muhammad bin Abdullah SAW anatambuliwa katika mtiririko kama huo, kuwa pale alipotoa maelekezo kama yeye, na siyo ufunuo (unaotoka kwa malaika) inaitwa 'sunna,' ambayo ni njia nyingine ya kutamka neno 'selon,' au inatoka kwa Solon.

Jitihada ya kuficha kile kinachozungumziwa ni sehemu ya utamaduni wa kumlinda anayesikiliza, ambao upande wake wa pili ni kutamka maneno yenye dhamira ya kumuumiza mhusika.

Hapa pia kuna mwingiliano wa kushangaza kidogo wa lugha, katika neno 'kutukana' ambalo ukiangalia kwa haraka unadhania kuwa kinachotajwa hapo ni kutumia lugha chafu dhidi ya mtu au watu kadhaa, kumbe kuna maana nyingine imejificha, kuwa aliyetamka maneno hayo amekana undugu na wale aliowalenga.

Ni kuwakana kuwa ni ndugu zake, na kwa maana hiyo hawaoni kama wenye heshima au wanaostahili heshima mbele yake, hivyo 'ametukana' haina maana tu kuwa ametoa matusi ila 'hana undugu na sisi' yaani amewakana kama ndugu, ambalo ni jambo la hatari, linaloshangaza.

Ina maana kuwa kuanzia dakika hiyo alipokana undugu wake na wahusika, mtu akiinua upanga akiwa mlengwa wa maneno yale walio karibu wasingefanya lolote.

Makatazo kimsingi yalilenga mahusiano au tabia katika mazingira ambako jamii ndiyo inasimamia sheria, kwa mfano kupiga mawe mwizi, mgoni n.k. utamaduni ambao sasa haukubaliki, kuwa kuchukua hatua ya kutoa hukumu na kuitekeleza ni kujichukulia sheria mkononi, kwani ni Mahakama, si jamii, iliyo na uwezo wa kuamua kama kuna kosa limetendeka.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# MAJANGA ya moto yamekuwa yakizikumba baadhi ya shule na wakati mwingine kusababisha maafa. Je kuna haja ya kuanzisha somo la kujikinga dhidi ya majanga? Wadau wanajadili




**EMMANUEL MANUMBA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWENYE somo la Kemia, wanafunzi wanafundishwa moto na aina zake na jinsi ya kupambana nao. Lakini pia ni vyema kukawapo somo rasmi shuleni linalohusu majanga ya moto ili kuwaandaa wanafunzi kujua namna ya kukabiliana nayo yanapotokea. Kila kitu tunachokijua leo katika maisha tulijifunza. Sasa kama hatuwafundishi watoto wetu shuleni namna ya kukabiliana na majanga especially (hasa) ya moto yanapotokea watawezaje kujua namna gani wakabiliane nayo? Kimsingi athari za matukio ya moto shuleni ni kubwa kwani licha ya kuwaathiri kisaikolojia wanafunzi, pia yanashusha kiwango cha elimu, yanawafanya wasome kwa shida na wengine kushindwa kabisa kutokana na kuunguliwa vifaa vyao. Tumewahi kushuhudia baadhi ya shule zikifungwa kwa muda kutokana na kuathiriwa na matukio ya moto kwa lengo la kupisha ukarabati, hali ambayo kwa kweli husababisha wanafunzi kuwa na wakati mgumu na hasa wale wanaojiandaa na mitihani ya kitaifa. Hivyo nirudie kusema kwamba elimu hii shuleni ni ya muhimu inaweza angalau kupunguza majanga ingawa ajali haina kinga.



**MARGETH NDOMBA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MAONI yangu ni kwamba ipo haja ya kuwa na somo la majanga shuleni ili kuwawezesha kujua namna wanavyoweza kusaidia kuepukana nayo. Moto unaotokea shuleni unasababishwa na shoti za umeme au matumizi ya pasi na mtu kusahau kuizima au matumizi ya vibatari na mishumaa kujisomea usiku, hasa umeme unapokuwa umekatika au unapokuwa wa tabu. Hivyo ni muhimu wanafunzi wapewe elimu, ambayo itawaongezea umakini pale wanapoona nyaya za umeme zipo nje au kuna mahali pana shoti, watoe taarifa kwenye mamlaka husika na kuhakikisha tatizo linashughulikiwa haraka. Pia hata kwenye umakini utaongezeka kutokana na kupewa elimu sahihi ya vitu vinavyoweza kusababisha majanga shuleni na nyumbani pia. Wanafunzi wanatakiwa kusomea katika mazingira ambayo ni salama kwao kwa ajili ya kuongeza mafanikio ya elimu na kukuza maarifa. Kwa maana hiyo ni vyema matukio ya majanga ya moto yakaandaliwa somo ili wanafunzi waweze kujua kiundani zaidi jinsi ya kuyakabili na pia nitoe wito kuwa majanga ya moto ambayo yamekuwa yakizikumba shule mbalimbali yatumike kama darasa la kuyadhibiti ili mengine yasiendelee kutokea nchini.




**IRENE MWITA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIONI umuhimu wowote wa kuwa na somo la majanga shuleni, ila tu inatosha mamlaka zinazohusika na kupambana na majanga kuendesha semina kwenye shule ya kujua namna ya matumizi ya vifaa mbalimbali kama vile fire extinguisher, kwa ajili ya kuzimia moto wa aina tofauti na jinsi ya kuweza kusaidia wenzao pale majanga yanapojitokeza shuleni. Maana ukipita shuleni unakuta kuna vifaa vya kuzimia moto na kutoa huduma ya kwanza, lakini mara nyingi unakuta hivyo vifaa vimeshapita muda wake na kukosa ubora na hivyo majanga yanapotokea unakuta havifanyi kazi. Vingine unakuta havifanyiwi matengenezo, unakuta vinaharibika vyenyewe na vingine unakuta vimeharibika kabisa, lakini hakuna anayejua kama havifanyi kazi, kwasababu watu hawavigusi kabisa. Lakini pia unakuta vifaa vipo na watu hawajui kuvitumia, hivyo majanga yanapotokea watu wanashindwa kukabiliana nayo. Kwa hiyo ni muhimu mamlaka kama za zimamoto kuwa zinafanya semina kwenye shule na kufundisha matumizi ya vifaa vya kuzimia moto na pia kukagua vifaa kama vipo safi. Askari wa Kikosi cha Zimamoto wamekuwa wakizunguka katika shule mbalimbali hapa nchini kufundisha wanafunzi jinsi ya kuepukana na majanga. Hivyo ushauri wangu ni kwamba elimu hiyo iendelee kutolewa shuleni huku wanafunzi nao wakiizingatia. Sioni sababu ya kuingiza kwenye mtaala somo la majanga shuleni. Zimamoto waendelee kuwezeshwa ili waweze kufikia shule zote nchini na kutoa elimu.



**ELVICE MAKUMBO (MKURUGENZI MTENDAJI WA TEFEYOCO)**

NIANZE kwa kusema kuwa Tafeyoco hii ni taasisi inayotoa elimu ya demokrasia, utawala bora, uraia na ya mpigakura. ninaporejea kwenye swali la msingi ni kwamba hakuna sababu ya kuwa na somo la majanga shuleni, bali cha muhimu ni kwa maofisa wa elimu wanaohusika na ukaguzi wa shule kabla ya kutoa kibali cha kuanzisha shule kuwa waaminifu. Yaani wahakikishe kuwa shule imekidhi vigezo vyote vya usalama kabla ya kuanzishwa na baada ya kuanzishwa. Rushwa imesababisha shule nyingi kupewa vibali bila kukidhi vigezo vya usalama. Unakuta shule imejiunganishia umeme kinyemela kwa kutumia njia za panya, ambao unaweza kuwa mkubwa au mdogo kuliko mahitaji ya shule na mwisho wa siku unasababisha shoti, ambayo inasababisha moto na uharibifu wa mali na maisha. Lakini pia shule zinapewa vibali bila vifaa vya kuzimia moto au hazina miundombinu mizuri ya kutokea au kujiokoa na majanga kama ya moto yanapotokea. Shule zinapewa vibali bila kukidhi mahitaji ya msingi ya kuwa na vifaa vya huduma ya kwanza vya kutosha ili kutoa msaada majanga yanapotokea. Wakati mwingine unakuta vifaa vya huduma ya kwanza vilivyopo vimeisha muda wake unaofaa kwa matumizi. Hivyo majanga mengine yanajitokeza sababu ya ukosefu wa uaminifu na umakini kwa watu, ambao wamekabidhiwa dhamana ya kufanya ukaguzi wa kuhakikisha kuna mazingira ya usalama wa kutosha kwenye shule wanazosoma watoto wetu.



**JENNIFER PIUS MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM**

MIMI ninaona kuna umuhimu kutoa elimu shuleni ili kuweza kuwaandaa kisaikolojia wanafunzi namna ya kuishi baada ya majanga kuwa yametokea. Maana baada ya majanga kuwa yameshajitokeza wengine wanapoteza maisha, wengine wanaumia na wengine wanapata ulemavu wa kudumu, lakini pia na miundombinu inaharibika kama majengo na mali. Hivyo ni muhimu wapewe elimu itakayowaandaa kisaikolojia kuwa yatakapojitokeza hayo inabidi wakabiliane na hizo changamoto kwa namna hii na ile. Kwamba mtoto atakapoona mwenzake anateketea na hana namna ya kufanya kumuokoa kisaikolojia inabidi awe ameandaliwa kwamba yapi yawe ni maamuzi sahihi na ya haraka ya kuchukuliwa. Kama kweli nia yetu ni kujenga elimu bora, basi litakuwa ni jambo la maana iwapo tutaweka misingi imara ya kuwawezesha wanafunzi kuelewa, hasa kwa kuwafanya wawe katika mazingira salama ya kusomea. Kikubwa ninachotaka kusema kuhusu mazingira salama ya kusomea ni pamoja na kuwapo kwa somo la majanga ambalo litasaidia kuwafanya watambue mazingira salama na yasiyo salama wawapo shuleni ili waweze kuepuka matukio, ambayo yanaweza kusababisha wakawa kwenye hatari, yakiwamo hayo ya mabweni kuungua moto, ambayo kwa miaka ya nyuma yalikuwa mengi, yakadhibitiwa lakini yameanza kujitokeza tena kama hilo lililotoea hivi karibuni mkoani Kilimanjaro.

# Wanawake, vijana, wenye ulemavu wakopeshwa mil. 290/-

**Na Grace Mwakalinga,** BUSOKELO

HALMASHAURI ya Busokelo imefanikiwa kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 291 kwa vikundi 57 vikiwamo vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu mwaka wa fedha 2018/2019.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani. Alisema licha ya kukabiliana na changamoto ya ukusanyaji wa mapato, lakini waliweka kipaumbele cha kukusanya asilimia 10 ili kunufaisha makundi hayo.

Aliongeza kuwa halmashauri hiyo kwa mwaka inakusanya Sh. milioni 700 kiasi ambacho kinachangiwa na vyanzo vingi vya mapato, na kwamba imesaidia kutenga bajeti za ndani kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo.

"Katika mkoa wa Mbeya, sisi ndiyo tunaongoza kwa kukopesha na kukusanya marejesho kutoka vikundi tulivyovikopesha, hata mwaka jana tulitunukiwa cheti kwa kushika nafasi ya tisa nchini kati ya halmashauri zote," alisema Ngilangwa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Agness Elikunda, alisema licha ya kujitahidi kukusanya kiasi hicho cha fedha, lakini kuna changamoto ya mwamko mdogo kwa kundi la vijana kujitokeza kukopa au kuanzisha vikundi na kuomba mikopo.

Alisema vijana hawajitokezi kuomba mikopo matokeo yake fedha ambayo ilitengwa kwa ajili ya vijana wanalazimika kuhamishia kwa wanawake kwa sababu wamehamasika kwa kiwango kikubwa kuunda vikundi na kukopa.

Alidai changamoto nyingine ya vijana ni kutokidhi vigezo vya kupata mikopo, na kwamba hadi sasa vikundi sita vya vijana na watu wenye ulemavu viwili na vya wanawake 49.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, aliwaagiza wataalamu wa halmashauri hiyo kuwafikia vijana wasiokuwa na sifa ya kupata mikopo kuwapa mbinu za kubuni miradi ya kujiendeleza kiuchumi, ili kuondoa lawama kwamba serikali kuwa haiwajali.

Alisema baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo kuna vikundi ambavyo vimeshindwa kurejesha mikopo, wakidai serikali imetoa ruzuku, jambo ambalo alisema ni upotoshaji, na kusisitiza kuwa vikundi visichukue mikopo kwa mihemko ya kisiasa.

# Wananchi 200 walilia bil.7/- kupisha kituo cha forodha

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WANANCHI 205 wa Kata ya Njisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, ambao walipisha mradi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Malawi na Tanzania, wameilalamikia serikali kushindwa kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kuwalipa fidia ya shilingi bilioni saba, alilolitoa Aprili 30, mwaka huu, wakati wa ziara yake wilayani humo.

Walieleza kuwa walipisha mradi huo tangu 2016 na kuahidiwa kulipwa fidia ndani ya muda mfupi, lakini hawajalipwa licha ya Rais Magufuli kuagiza wawe wamelipwa mwezi uliopita.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara, Mchungaji wa Kanisa la House of Prayer, George Kyamba, alisema kuwa walipata matumaini ya kulipwa fidia zao baada ya Rais kutoa agizo kuwa walipwe, lakini imekuwa tofauti kwani muda alioutoa Rais Magufuli umepita na hakuna viongozi wowote waliofika kuwaeleza sababu za kutotekeleza agizo hilo.

"Kwenye ziara ya Rais tuliandaa mabango ya kueleza kero yetu ya fidia, lakini kuna baadhi ya viongozi walitufuata na kutuomba tusifanye hivyo na kututia moyo kuwa tutalipwa, lakini hakuna kinachoendelea na hatujui hatima yetu," alisema Mchungaji Kyamba.

Juma Mwakalinga alidai suala la fidia limeingizwa siasa na ndio sababu tangu mwaka 2016 hakuna utekelezaji badala yake wanapigwa kalenda.

Alisema watendaji wa Rais Magufuli baadhi yao wanashindwa kutekeleza maagizo hali inayosababisha wananchi wanyonge kukosa haki zao.

Neema Lyolo, alisema kitendo cha wananchi wa Kata ya Njisi kuhamishwa eneo lao ambalo lipo Kasumulu, shughuli za kilimo na biashara zimesitishwa hali inayochangia ugumu wa maisha.

Mwenyekiti wa waathirika hao, Kelly Mwandambo, alisema kutokana na kupuuzwa kwa agizo la Rais Magufuli watajichangisha fedha kwa ajili ya kufikisha mbele kilio chao ili haki itendeke kwa kuwa wamechoshwa na ahadi hewa.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alikiri kupokea agizo la Rais Magufuli la kuagiza wananchi hao kulipwa stahiki zao ndani ya Mei, na kwamba wako katika hatua za mwisho na wakati wowote watalipwa.

"Tumefanya mawasiliano na wataalamu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), kwa ajili ya usanifu mwingine na kuhakiki wanaostahili," alisema Claudia.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo (kushoto), akipokea maelezo kutoka kwa Ofisa wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Haruna Kalunga, wakati alipotembelea ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi kunufaisha shule jijini Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHULE nne zikiwamo za msingi na sekondari jijini Mbeya zinatarajia kunufaika na mradi wa ufuatiliaji na uwajibikaji wa jamii ambao unahusika na udhibiti ubora wa shule ili kuongeza uwajibikaji kati ya viongozi na jamii kupitia sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Child Support Tanzania, Noela Msuya, wakati wa hafla ya kuzindua mradi wa ufuatiliaji wa uwajibikaji wa jamii ambapo alisema mradi huo utawaunganisha wadau wa elimu pamoja na kujadili changamoto zinazowakabili ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Alisema mradi huo utazishirikisha Shule za Msingi Mapambano na Igoma na za Sekondari ni Wigamba na Samora, na kwamba walimu, waratibu, wanafunzi na jamii zinafundishwa masuala ya ufuatiliaji na uwajibikaji ili kukuza sekta ya elimu.

"Mradi huu ambao umezinduliwa leo utakuwa ni wa miaka miwili... matarajio yetu ni kuongeza ufaulu kwa wanafunzi, na pia kukuza sekta ya elimu kwa kuhamasisha maboresho ya maslahi kwa walimu pamoja na mazingira wezeshi ya kujifunzia," alisema Noela.

**Mradi huu ambao umezinduliwa leo utakuwa ni wa miaka miwili... matarajio yetu ni kuongeza ufaulu kwa wanafunzi, na pia kukuza sekta ya elimu kwa kuhamasisha maboresho ya maslahi kwa walimu pamoja na mazingira wezeshi ya kujifunzia**

Ofisa Ufuatiliaji wa Child Support Tanzania ambao wanafanya kazi na mradi huo, Victor Sizya, alisema kupitia mradi huo watachangia jitihada za serikali za kuboresha udhibiti ubora wa shule za msingi na sekondari katika jiji la Mbeya.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema serikali inahitaji nguvu ya wadau ili kuboresha mazingira ya elimu na kwamba mradi huo utakuwa chachu ya kufanya mabadiliko.

Alisema serikali ipo tayari kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu, lakini alishauri kuhakikisha mradi huo unaleta matokeo chanya ili jamii na wanafunzi waweze kunufaika.





# Mgombea ubunge Chadema, wanachama watimkia CCM

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

ALIYEKUWA mgombea ubunge Jimbo la Bahi mkoani Dodoma mwaka 2015 kupitia Chadema, Mathias Lyamunda, pamoja na uongozi wa ngazi ya juu wa wilaya hiyo wamejiengua kutoka upinzani na kujisalimisha CCM.

Viongozi hao walioamua kujisalimisha CCM, pamoja aliyekuwa mgombea wa ubunge mwaka 2015 ni Mwenyekiti wa Chadema Wilaya ya Bahi, Mathias Lyamunda, mjumbe wa mkutano mkuu taifa Damian Mchela.

Wengine ni aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Wilaya, Merzedeck Lesaka, Katibu Mwenezi Wilaya, Shekhe Ramadhani Issa na Mhazini Wilaya, Timotheo Matias.

Wakizungumza mbele ya Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Bahi, Hasani Kidoke, kwenye ziara ya kuimarisha chama kuelekea uchaguzi wa serikali ya mitaa na vijiji utakaofanyika nchi mzima Oktoba mwaka huu, walisema hakuna sababu ya kuendelea kuwa wapizani wakati Rais John Magufuli, ameshatatua changamoto zote zinazowakabili Watanzania.

Damian Mchela na Timotheo Matias, wakizungumza kwa niaba ya viongozi wenzao waliotimuka kwenye chama hicho, walisema ahadi za CCM zilizotekelezwa zimewafanya kutong'ang'ania kwenye upinzani.

"Hakuna sababu ya kuendelea kung'ang'ania kwa kuwa kwa kufanya hivyo unadumaza maendeleo ambayo Rais ameshayakamilisha ikiwamo ujenzi miundombinu mbalimbali," alisema Mchela.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Bahi, Hassani Kidoke, alisema kuibomoa ngome hiyo ya Chadema kunatokana na sera zinazotekelezwa na CCM.

Aidha, aliwataka viongozi hao kutumia nguvu waliyokuwa wakiitumia kwenye upinzani kukiimarisha zaidi chama tawala pamoja na kuleta ushindi kwenye uchaguzi unaokuja.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza na wafanyakazi wa Kituo cha Afya Makole, wakati wa ziara yake ya pili kukitembelea kituo hicho, kushoto ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Charles Kiologwe. **PICHA: PAUL MABEJA** .

# Kituo cha Makole chaimarisha ubora

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KITUO cha Afya cha Makole kilichopo jijini Dodoma kimeboresha huduma za tiba na kuongezeka idadi ya wagonjwa wanaotibiwa kutoka 25,480 hadi 35, 486 kwa miezi mitatu.

Hatua hiyo iliyopongezwa na serikali imefafanuliwa kuwa ni ongezeko la wagonjwa wapya 10,926 ambao ni sawa na asilimia 30.

Sambamba na ongezeko hilo idadi ya wagonjwa waliokuja kupata matibabu katika kituo hicho wanaotumia bima ya afya (NHIF) imeongezeka kutoka 470 hadi 973.

Akizungumza na wafanyakazi wa kituo hicho, wakati wa ziara yake Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, alielezea furaha yake kufuatia kupokea taarifa ya kituo hicho kutoka kwa Mganga Mfawidhi Dk. George Matiko.

Taarifa hiyo ilionyesha kuwapo kwa mabadiliko makubwa ya utoaji huduma.

Dk. Gwajima alisema kuwa ikiwa ni miezi mitatu tangu alipofanya ziara yake kwa mara ya kwanza katika kituo hicho mnamo Februari 17, mwaka huu, safari hii amefurahi kuona namna watendaji wa kituo hicho wakiongozwa na mlezi wa kituo hicho, Mary Shadrack, walivyojizatiti kutoa huduma bora za tiba kwa wananchi.

Alisema kitendo cha watumishi kubadilika na kutoa huduma bora kwa wananchi kinapaswa kuigwa na vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

"Nilipotembelea kituo hiki Februari, 2019 nilikuta kituo chenu kikiwa na malalamiko mengi ya wagonjwa hasa kero ya foleni na malalamiko ya kutoa huduma mbovu kwa wagonjwa, lakini sasa mmebadilika hongereni sana," alisema Dk. Gwajima na kuongeza. "Napenda kuwasihi muendelee na ari hiyo ya kutoa huduma kwani wananchi wengi wangependa kuhudumiwa katika vituo vya afya vya umma, lakini wanakatishwa tamaa na mazingira mabovu wanayoyakuta," alisema.

Wakati huo huo Dk. Gwajima aliwapongeza Makatibu Tawala wa Mikoa ya Morogoro na Ruvuma kwa kufanyia kazi taarifa za ziara zake katika mikoa hiyo na matokeo yake viongozi hao kuamua kufanya mabadiliko kwa timu za usimamizi huduma za afya za mikoa yao.

Alisema jambo hilo litaleta mabadiliko yatakayosaidia kuongeza kasi ya usimamizi kwa watendaji wapya watakaoteuliwa badala ya mazoea.

# Taasisi yahimiza kukumbuka wahitaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya kusaidia wahitaji ya mkoani Dodoma, imewataka watu binafsi, taasisi na mashirika kuwakumbuka kila wakati na kuwasaidia wenye mahitaji muhimu wakiwamo wagonjwa, yatima, wajane na wazee wasiojiweza.

Meneja wa Taasisi ya Dar ul Muslimen Center, Shekhe Muslimen Bhanji, alitoa ushauri huo wakati wa kukabidhi misaada mbalimbali kwa wajane, yatima na wazee wasiojiweza wa kata ya Chang'ombe mkoani Dodoma.

Aidha, msaada huo uliwahusu pia wagonjwa waliolazwa katika hospitali ya rufani ya mkoa wa Dodoma.

Misaada hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 3.2 ilikuwa ni pamoja na miswaki, dawa ya meno, mafuta ya kupakaa, taulo na sabuni kwa ajili ya wagonjwa 120 waliolazwa katika hospitali ya rufani ya mkoa wa Dodoma.

Kwa upande wa wajane, wazee wasiojiweza na yatima 135 wa kata ya Chang'ombe walipatiwa mchele na maharage kwa ajili ya chakula, alisema Sheikh Bhanji.

Akizungumza wakati wa kuwakabidhi wahitaji alisema wanapatiwa misaada mbalimbali kama vyakula, dawa, mavazi na vifaa vya elimu.

Sheikh Bhanji alisema jamii hiyo pamoja na kusaidiwa na serikali kwa upande wa mashirika, taasisi na watu binafsi wana kila sababu ya kuhakikisha juhudi hizo za serikali zinaungwa mkono katika kuwafikia wenye mahitaji hayo bila kujali dini, kabila, rangi au chama.

Taasisi ya Dar ul Muslimen Center imekuwa ikitoa misaada kila wakati kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo katika shule za msingi na sekondari, taasisi za kidini na vituo vya yatima, walemavu pamoja na kambi za wazee wasiojiweza.

"Tunafanya hivyo ikiwa ni sehemu yetu ya kutimiza majukumu tuliyonayo ya kuhakikisha tunawasaidia watu wenye uhitaji wa vitu mbalimbali. Pia tumekuwa tunafanya hivyo kuiunga mkono serikali yetu kusaidia jamii hiyo," alisema Bhanji.



# Utaratibu kuchagua magari ya mchanga wawekwa wazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasilili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar imesema kuwa utaratibu wa kuchagua magari 200 kwa ajili ya usafirishaji mchanga umezingatia vipengele vyote muhimu kuhakikisha kila gari linapata fursa ya kufanya kazi.

Akijibu swali katika Baraza la Wawakilishi Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ali Ussi, alisema kwa hatua za awali wizara ilitoa matangazo katika vyombo vya habari kwa wote wenye magari ya mchanga kupeleka maombi yao kwa katibu mkuu wa wizara hiyo.

Naibu waziri huyo aliyasema hayo baada ya kuulizwa swali na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, aliyataka kujua wakati wa kupanga utaratibu huo wadau wa shughuli hiyo walishirikishwaje ili kuona kwamba kila gari linapata nafasi ya kufanya kazi.

Alieleza kuwa jumla ya maombi 654 yalipokelewa kwa Unguja na maombi 120 yalipokelewa kwa Pemba, na walifanya mchakato wa kuyapembua maombi hayo kiwilaya ili kutoa fursa sawa kwa kila wilaya kupatikana huduma hiyo.

Alisema wizara yake iliweka vigezo muhimu vya kuyachagua magari hayo ikiwamo ujazo wa gari, wilaya pamoja na shehia iliombea kutoa huduma ya kusafirisha na kupeleka mchanga.

Alisema vile vile wizara ilijadili na jumuiya ya wenye magari ya kusafirishia mchanga na kutoa orodha na ushirikiano.

"Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa mamlaka zinazokusanya kodi magari ya mizigo husajiliwa kwa kusafirisha mizigo ya aina tofauti kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ikiwa mchanga ni sehemu ya mizigo hiyo," alisema.

Alisema hata kama gari la mizigo halitopata nafasi ya kusafirsha mchanga kwa kipindi hicho bado linahitajika kulipa kodi ya usajili wa magari ya mizigo kwa kuwa litaendelea na usafirishaji wa mizigo mingine.

Aidha, alisema kwa gari ambalo linahitaji kusafirisha rasilimali ya mchanga linalazimika kukata leseni ya usafirishaji wa mchanga ambayo hutolewa na Wizara ya Kilimo kupitia utaratibu maalum.

Alisema utaratibu huo unatoa fursa ya wenye magari kutuma maombi na hatimaye kuchaguliwa na kupata leseni husika ya kubeba mchanga kwa kipindi cha miezi mitatu kwa thamani ya Sh. 25,000.

Naibu waziri huyo alisema kwa mwaka 2019 wameshatoa leseni za usafirishaji wa mchanga kwa kipindi cha miezi mitatu kwa kila gari liliyochaguliwa na kufuata utaratibu maalum.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akishiriki katika sala ya kuuombea mwili wa marehemu Abdaall Waziri, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar, ikiongozwa na Naibu Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, katika Masjid Noor Muhammad Mombasa kwa Mchina Zanzibar, jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## SMZ yaeleza madaraka ya Rais ya kugawa maeneo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, imesema kuwa kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Rais wa Zanzibar amepewa mamlaka ya kuigawa nchi katika mikoa, wilaya na maeneo mengine kama atakavyoona inafaa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, alisema Baraza la Wawakilishi lilitunga sheria za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 na Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 ambazo zililenga kufanya mageuzi makubwa ya kimiundombinu na kitaasisi katika ngazi za mikoa, wilaya, shehia na serikali za mitaa.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali alilolulizwa na Mwakilishi wa Kijitoupele, Ali Suleiman Shihata, aliyetaka kujua serikali haioni haja ya kuugawa mkoa wa Mjini Magharib Unguja kuwa mikoa miwili.

Alisema kufuatia mabadiliko hayo ya kisheria, Mei mwaka 2015 Rais wa Zanzibar aliigawa upya mikoa, wilaya na shehia.

Alisema miongoni mwa vigezo vilivyotumika na idadi ya watu ambapo wakati wa ugawaji wa mwaka 2015 mkoa ulikuwa na idadi ya watu wasiopungua 593,678 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, ambayo ilizingatia pia makadirio ya ongezeko la watu hadi kufikia mwaka 2022.

"Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba Mkoa wa Mjini Magharib Unguja una idadi kubwa ya watu kulinganisha na mikoa mingine ya Zanzibar kwa mujibu wa sensa ya idadi ya watu na makaazi ya mwaka 2012, mkoa una jumla ya asilimia 46 ya wakazi wote wa Zanzibar.

Alieleza kuwa kwa sasa serikali haioni haja wala hoja za msingi za kuugawa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kuwa mikoa miwili ya kiutawala.

Alisema pamoja na maelekezo hayo, jambo hilo ni la kikatiba na kisheria na bado Rais wa Zanzibar hafunguki kufanya vyinginevyo wakati wowote pale atakapoona kuna haja ya kufanya hivyo.

# Idadi ya wazee Zanzibar yatajwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Shadia Muhammed Suleiman, amesema kuwa Zanzibar ina jumla ya watu wenye umri wa miaka 60 na zaidi 58,311.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo Chakechake, Suleiman Sarahan Said, aliyetaka kujua takwimu sahihi za wazee waliopo Zanzibar.

Naibu waziri huyo alisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, ambayo ilibainisha kuwa wazee hao wapo mijini na vijijini.

Alisema idadi ya watu wenye umri wa miaka 70 na kuendelea ambao wamesajiliwa katika programu ya pensheni ya wazee kwa Unguja ni 17,597 na Pemba ni 10,313, ambapo jumla ya wazee wote waliosajiliwa ni 27,910 hadi kufikia Mei 2019.

"Takwimu zote hizo zipo kimkoa, wilaya, majimbo mpaka shehia," alisema Naibu Waziri huyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Aidha, alisema wizara yake pia ina takwimu za vifo vya wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea ambao wamesajiliwa katika kitengo cha pensheni jamii.

Alisema jumla ya wazee 946 wamefariki upande wa Unguja na 522 kwa Pemba kuanzia Julai mwaka 2018 hadi Machi mwaka 2019.

Aidha, alisema kuwa wizara yake inatambua kuwa mzee mwenye umri mkubwa katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa mujibu wa taarifa walizonazo ni mzee Juma Kombo Makame mwenywe umri wa miaka 115, mkazi wa Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja.

# Sababu Baraza la Ardhi kuvunjwa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

BARAZA la Ardhi na Nyumba la Kata ya Kinungu, Tarafa ya Igurubi, Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, limevunjwa baada ya kubainika kushindwa kuendesha mashauri yao kwa kuzingatia sheria za mabaraza ya ardhi ya kata.

Akivunja baraza hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kinungu, Michael Myapi, alisisitiza kwamba alifikia uamuzi huo baada ya viongozi wa baraza la kata hiyo, kulalamikiwa mara kwa mara na baadhi ya wananchi kwa kushindwa kutoa haki za kisheria kwa wanaopeleka mashauri yao.

Aliyataja baadhi ya malalamiko ya wananchi dhidi ya baraza hilo ni kutozwa adhabu ya faini kubwa kuanzia shilingi 175,000 hadi 300,000 bila kupewa stakabadhi, huku wakituhumiwa pia kujihusisha na rushwa pamoja na kuwafungia watuhumiwa ofisini siku za Jumamosi na kuwanyima dhamana.

Myapi alisema kwamba katika kipindi kifupi alichokaa katika kata hiyo amekuwa akipigiwa simu na wakubwa zake kutoka wilayani mara nyingi juu ya malalamiko ya wananchi dhidi ya baraza hilo.

Alisisitiza pia kuwa baada ya kufuatili tuhuma hizo ndipo alipobaini kwamba baraza hilo halitendi haki kwa wananchi badala yake watendaji wa viongozi wake wanajinufaisha, na kwamba hadi sasa Baraza la Ardhi na Nyumba Kata ya Kinungu halipo hadi hapo litakapochaguliwa lingine kwa mujibu wa sheria.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Bunona Biliya, alikiri kuvunjwa kwa baraza, na kueleza kwamba wananchi walikuwa wakililalamikia kwamba halitendi haki, ingawa alikanusha.

Baadhi ya wananchi wa kata hiyo, Jimoga Ndalago, Mwashamba Ludega na Jihungwa Ngwale walimshukuru mtendaji wa kata kwa kusikiliza kilio cha wananchi wanyonge, maana walikuwa wakiishi kama si Watanzania, kwa kuwa baraza hilo liligeuzwa kitega uchumi cha viongozi wachache.

Ofisa Tarafa ya Igurubi, Judith Haule, alithibitisha kuvunjwa baraza hilo tangu Mei 29, mwaka huu, kutokana na baraza hilo kuwa na udhaifu mkubwa kiutendaji wa kazi kwa wananchi.

Haule alisema badala ya baraza hilo kutatua migogoro ya wananchi, limekuwa likiiongeza, na kwamba nafasi za viongozi wa baraza hilo zimeshatangazwa kwa ajili ya kuwachagua wengine.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Saruji ya Twiga (TPCPLC), Alfonso Velez (wa kwanza kulia), akiteta jambo na mmoja wa wanahisa wa kampuni hiyo, George Chambo, baada ya kumalizika kwa Mkutano Mkuu wa 27 wa mwaka jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mjumbe wa Bodi ya kampuni hiyo, Oswald Urassa. **MPIGAPICHA WETU**

# Saruji Twiga sasa yajivunia faida bil. 80/-

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya saruji ya Twiga (TPCPLC) imepata faida ya uendeshaji inayofikia Sh. bilioni 80.06, ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 ukilinganishwa na mwaka 2017.

Hayo yalibainishwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 27 wa mwaka na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Alfonso Velez, na kueleza kuwa ongezeko hilo la faida limesababishwa na ongezeko la mauzo ambalo ni asilimia 28, uzalishaji pamoja na uthabiti wa bei.

"Mwaka 2018, TPCPLC iliweka rekodi juu ya mauzo, huku soko la saruji likiongezeka kwa asilimia 7 sawa kabisa na ongezeko la pato la taifa la asilimia 6.8. Inakadiriwa kuwa uhitaji wa saruji nchini umefikia tani milioni 4.7, huku TPCPLC ikiwa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 9," alieleza.

Aliongeza: "Usambazaji wa saruji umeongezeka kwa asilimia tisa ikilinganishwa na mwaka 2017 na hii imefanikishwa na mtandao mzuri kwa wateja wetu ambao umeweza kufikisha bidhaa zetu katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi yetu, na kuwezesha bidhaa zetu kutambulika kwa wateja wetu wote."

Velez aliongeza kuwa ujenzi wa miradi ya miundombinu unaoendelea nchini umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko hasa katika nusu ya pili ya mwaka 2018. "Ujenzi wa reli, upanuzi wa bandari, daraja la Ubungo ni baadhi ya miradi mikubwa michache ya ujenzi ambapo saruji chapa ya Twiga imetumika," alifafanua.

Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2018 ya TPCPLC, usambazaji wa saruji nchini umeongezeka kwa asilimia 9 ikilinganishwa na mwaka 2017 ukifanikishwa na mtandao mzuri wa wateja wa kampuni hiyo.

Ili kukabiliana na ushindani uliopo, Velez alisema kampuni imeimarisha timu yake ya masoko, kuhakikisha kuwa bidhaa zinafika mikoa yote.

"Saruji ya ziada inafikia tani milioni nne, hivyo kufanya ushindani kuwa mgumu katika vipindi vijavyo. Pamoja na changamoto hii, kampuni imedhamiria kuwa kiongozi katika soko la saruji kwa kusambaza saruji yenye ubora na kuhakikisha inakidhi mahitaji ya wateja," alisema.

# Ikungi yakarabati, kupanua vituo afya

**Na Salome Kitomari**

HALMASHAURI ya Ikungi mkoani Singida, imekarabati na kupanua vituo viwili vya afya kwa kutumia mafundi wa jamii, uamuzi uliowezesha kuokoa mamilioni ya fedha.

Akizungumza jana na gazeti hili Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alivitaja vituo vilivyokarabatiwa ni Ihanja na Sepuka ambavyo vitatoa huduma muhimu za afya.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 1.13 ambazo Sh. milioni 500 zilikarabati na kupanua kituo cha Ihanja ambacho kiliwekewa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 230.

Aidha, ukarabati unaendelea katika kituo cha Sepuka na kiasi cha Sh. milioni 400 zimetolewa, kutoa huduma za dharura na upasuaji, na kwamba ungetumika utaratibu wa zamani gharama ingekuwa mara mbili.

Kijazi alisema kituo cha Ihanja kimeshakamilika na kazi iliyofanyika ni jengo la maabara, wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, chumba cha kuhifadhia maiti, nyumba ya mganga na jengo la kufulia.

Nyingine ni eneo la kuchomea takataka, ukarabati wa majengo sita ya zamani, ujenzi wa njia za kutembelea na mfumo wa majitaka na majisafi.

Kwa mujibu wa Kijazi, katika kituo cha Sepuka kazi zote zilizofanyika Ihanja zitafanyika na kwamba kwa sasa ukarabati na upanuzi unaendelea.

"Lengo la miradi hii ni kupanua miundombinu ili kutoa huduma za dharura ikiwamo upasuaji kwa wajawazito ambao walitembea umbali mrefu kupata huduma za afya na wengine kujifungulia nyumbani," alisema.

Mkurugezni huyo alisema wanufaika wa vituo hivyo watakuwa wajawazito, watoto na wananchi kwa ujumla.

"Tumejenga kituo cha Ihanja kwa kutumia mafundi wa jamii, tumeepuka utaratibu wa zabuni ambao unagharimu fedha nyingi, tumeunda kamati ambazo zinasimamia kwa karibu kwa kupewa utaalamu na halmashauri," alisema.

Alisema kamati zilizoundwa ni ya ujenzi, manunuzi na mapokezi ambazo zinapata ushauri wa kitaalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

"Tunamshukuru sana Rais John Magufuli kwa kuona umuhimu wa kutupatia fedha za ujenzi na ukarabati huu, huduma za afya zinakwenda kuboreshwa kwa kiasi kikubwa na sasa mama wajawazito na wagonjwa wengine hawatatembea umbali mrefu," alisisitiza.

## HABARI KIMATAIFA

# Kinyang'anyiro cha kumrithi Theresa May chaanza

**LONDON, Uingereza**

KINYANG'ANYIRO cha uongozi wa Chama cha Conservative kimeanza rasmi jana baada yaTheresa May kung'atuka siku ya Ijumaa.

Mshindi katika mchakato huo atachukua nafasi ya May kama Waziri Mkuu wa Uingereza.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Boris Johnson anapewa nafasi kubwa ya kushinda, lakini Waziri wa Mazingira Michael Gove ni mgombea mwenye nguvu pia.

Wagombea 11 wa chama hicho wanawania kumrithi May katika uongozi wa chama hicho kikongwe.

Mchakato wa Brexit ndio hasa uliosababisha kuondoka madarakani May na unatarajiwa kuwa mjadala mkubwa kati ya wagombea hao wanaowania kumrithi.

Wajumbe wa chama hicho wa bunge la Uingereza jana walipokea orodha ya washindani hao.

Miongoni mwa wagombea wanaowania kuchukua kiti hicho ni , Waziri wa zamani wa mambo ya nje na aliyekuwa Meya wa Jiji la London, Boris Johnson, Waziri wa Mambo ya Nje, Jeremy Hunt, Waziri wa Mambo ya Ndani, Sajid Javid, Kiongozi wa zamani wa Bunge, Andrea Leadsom

Kutokana na idadi kubwa ya wanaotaka kugombea, kutakuwapo duru kadhaa za upigaji kura kati ya wabunge 313 wa chama hicho ili kupunguza idadi hiyo.

Wagombea wawili watakaobaki watapigiwa kura na wanachama wa chama hicho wapatao 150,000.

Wagombea wote wamejinasibu kwamba wanaweza kufanikisha kuiondoa Uingereza kutoka Umoja wa Ulaya kwa njia bora kuliko mpango wa May.

Wengi wao wamesema wataiondoa Uingereza kutoka kwenye umoja huo kufikia mwisho wa mwezi Oktoba hata ikiwa bila ya mkataba.

Boris Johnson alisema iwapo atachaguliwa atakataa kulipa madeni yaliyokubaliwa na Uingereza kwa Umoja wa Ulaya katika kipindi cha uanachama wake.

Uamuzi juu ya nani hasa atakayekiongoza chama hicho unatarajiwa kutoka mwishoni mwa Julai, muda mfupi tu ambapo kiongozi mpya atalihutubia Bunge na baada ya hapo Bunge hilo litakwenda likizo ya majira ya kiangazi Agosti na litarejea tena mwanzoni mwa Septemba.

**DW**

# Mwanajeshi auawa kisa 'kiroba' cha pombe

**KAMPALA, Uganda**

MWANAJESHI nchini Uganda, Fred Kimanai (32), ameuawa na wananchi wenye hasira kali kwenye shambulizi linalodaiwa kuchochewa na kugombea pombe aina ya waragi.

Tukio hilo limeripotiwa kutokea katika Wilaya ya Bududa ambapo wananchi hao wenye hasira inasemekana walimvamia mwanajeshi huyo na kumpiga, wakieleza kulipiza kisasi.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Monitor, mwanajeshi huyo aliuawa mwishoni mwa wiki na watu ambao walikuwa wanaomboleza kifo cha kijana Ivan Wamalile.

Gazeti hilo linaripoti kuwa kadhia ilianza baada ya wawili hao ambao wote marehemu kugombea pombe ya kienyeji aina ya 'kiroba' inayoitwa waragi. Mwanajeshi huyo inadaiwa alimchoma kisu mwenzake ambaye alifariki akiwa njiani akipelekwa hospitali.

Waombolezaji wa msiba wa Wamalile walimalizia hasira zao kwa kulipa kisasi kwa kumshambulia Mwanajeshi huyo hadi umauti ulipomfika.

Mwanajeshi huyo alikuwa amerejea nchini Uganda siku chache akitokea Somalia ambapo alikuwa alikinda amani.

Msemaji wa polisi wa eneo hilo, Robert Tukei, amethibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba uchunguzi unaendelea.

"Tumepoteza watu wawili katika mkasa huo, mwanajeshi na raia. Tunachunguza matukio yote mawili," alisema Tukei.

Tukio alitoa onyo kali kwa raia kujichukulia hatua mikononi, na kuwa wote watakaobainika kushiriki kwenye mauaji hayo watakamatwa na kufunguliwa mashtaka.

"Washukiwa watakamatwa na kufunguliwa mashtaka ya mauaji," alisema Tukei.

Alisema kuwa marehemu hao wawili walikuwa na ugomvi uliosababishwa na pombe.

Tukio hilo linatokea zikiwa zimepita siku chache tangu Uganda kupiga marufuku utengenezwaji na usambazwaji wa pombe za waragi.

Miili ya marehemu hao imehifadiwa kwenye hospitali ya wilaya ya Baduda ambapo inaendelea kufanyiwa uchunguzi. Msemaji wa kikosi cha Jeshi, Kapteni Abert Arinaitwe ambacho Kimanai alikuwa anahudumu amethibitisha kifo hicho.

"Tumempoteza mmoja wetu, lakini tayari tumeshatuma kikosi cha kuchunguza tukio hilo. Baada ya hapo tutajua nini cha kufanya kufuatana na ripoti tutakayopata," alisema Kapteni Arinaitwe.

Mwaka jana, askari wa wanyamapori katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Elgon iliyopo kwenye eneo hilo aliuawa na wakazi wa Baduda baada ya askari mwingine kumuua moja ya wakazi wa wilaya hilo.

***BBC***



Wagombea wanaowania nafasi ya Waziri Mkuu wa Uingereza ili kumrithi Theresa May ambaye ameshatangaza kujiuzulu. **PICHA: ALLIANCE**

# Jeshi Sudan lawalaumu wakuu wa maandamano

**KHARTOUM, Sudan**

JESHI la Sudani limewatupia lawama viongozi wa waandamanaji na kueleza kuwa wao ndiyo chanzo cha vurugu nchini humo.

Tangu kutokea kwa vurugu nchini humo, watu wanne wameshauawa wakati maafisa wa usalama walipokuwa wakitawanya maandamano kutokana na uasi wa kiraia ulioanzishwa jana.

Baraza la kijeshi Sudan ambalo hadi sasa ndilo linaloongoza nchini hiyo tangu lilipofanya mapinduzi ya kumuondoa aliyekuwa rais wa nchi hiyo Omar al Bashir, limekuwa likiitupia lawama viongozi wa waandamaji kwa kuendeleza machafuko.

Wakati huo huo, watu wanne waliuawa jana wakati maafisa wa usalama walipokuwa wakitawanya maandamano kutokana na uasi wa kiraia ulioanzishwa jana.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa maduka kadhaa, vituo vya kuuza mafuta na mabasi vimeanza kutoa huduma, ikiwa ni siku ya pili ya uasi ulioitishwa wa kiraia dhidi ya baraza la kijeshi.

Licha ya huduma hiyo kurejea, lakini wakuu wa waandamanaji wamewahimiza wananchi wa Sudan kuendelea na uasi, ili kulishinikiza jeshi kuachia madaraka.

Juzi, maandamano yalianza upya huku watu wakichoma moto matairi barabarani na kuweka vizuizi katika wilaya ya Bahari, Kaskazini mwa Mji Mkuu wa Khartoum, masoko na maduka yaliendelea kufungwa sawa na katika miji mingine.

Lakini maofisa wa polisi waliingilia kati na kuanza kufyatua risasi hewani pamoja na mabomu ya kutoa machozi kwa waandamanaji kisha waliondoa vizuizi vilivyowekwa barabarani.

Baraza la kijeshi la utawala wa mpito limewalaumu waandamanaji kwa kuendeleza machafuko hayo.

Luteni Jenerali Jamaleddine Omar ambaye anatoka katika baraza la kijeshi linaloongoza alisema kitendo cha kuziba barabara na kuweka vizuizi, waandamanaji walifanya uhalifu.

Luten Jenerali Jamaleddine alisema vikosi vinavyoshughulikia masuala ya dharura vimepelekwa katika maeneo mbalimbali Sudan kulinda usalama.

"Baraza la kijeshi limeamua kuwapeleka wanajeshi wa kushughulikia hali ya dharura na wale wa kawaida, ili kurejesha hali ya kawaida na kuwalinda watu ambao hawana silaha. Ili wafungue barabara kuwezesha usafiri wa umma na kulinda taasisi mbalimbali pamoja na masoko," alisema Luten Jenerali Jamaleddine.

Kamati ya madaktari wanaojihusisha na maandamano hayo imesema watu wawili waliuawa wakati wa makabiliano mjini Khartoum na wengine wawili waliuawa katika mji wa Omdurman mkabala na mto Nile. Vifo vya watu wanne vimetokea baada ya vile vya wiki iliyopita ambapo zaidi ya watu 100 waliuawa.

Chanzo cha vifo hivyo ni mvutano kati ya waandamanaji na wanajeshi, ambapo waandamanaji wanalitaka baraza la kijeshi kukabidhi madaraka kwa uongozi wa kiraia.

***DW***

## Zaidi ya 100 kufanyiwa upasuaji bure Aga Khan

**Na Beatrice Shayo**

ZAIDI ya watu 100 wakiwamo wanawake na watoto wa kike, waliopata majanga ya ajali, kuungua moto na kufanyiwa ukatili wa kijinsia, wanatarajia kuwafanyiwa upasuaji wa bure.

Upasuaji huo unafanywa na Hospitali ya Aga Khan kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na madaktari bigwa kutoka nchini Marekani.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Daktari Bingwa wa upasuaji kutoka Hospitali ya Aga Khan, Dk. Aidan Njau, alisema upasuaji huo utafanywa bure katika hospitali ya Aga Khan na wanatarajia kuwafikia wagonjwa zaidi ya 100 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema wanawake na watoto wa kike wenye matatizo hayo wamekuwa wakinyanyapaliwa katika jamii zinazowazunguka hali ambayo imewalazimu kutoa huduma hiyo. Aidha, Dk. Njau alisema upasuaji huo utafanyika kwa awamu mbili kwa mwaka na awamu ya kwanza itaanza Juni 15, mwaka huu.

Alisema anatambua upasuaji huo ni gharama kubwa, lakini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wataendesha zoezi hilo bila malipo kwa kinamama na watoto wa kike watakaojitokeza.

Dk. Njau alisema ni muhimu wakajitokeza wale wenye majeraha makubwa ambao wamelengwa kupatiwa huduma hiyo.

"Zoezi hili tumelianza tangu mwaka 2016 na kiukweli limewanufaisha kinamama wengi hata hivyo tumekuwa tukilifanya mara moja kwa mwaka ila mwaka huu tutalifanya mara mbili ili kuwafikia wale wote wenye tatizo hilo," alisema. Aidha, alisema pia watawatibia kinamama wanaosumbuliwa na saratani ya shingo ya kizazi pamoja na ya matiti ambayo imekuwa ikisababisha vifo vingi nchini. "Tutafanya operesheni ya kutengeneza ziwa kupitia kwenye nyama za mwanamke aliyepata saratani ya ziwa, tunaamini mwanamke aliyekatwa ziwa akifanyiwa operesheni hiyo na kupata ziwa lingine tutamuongezea uwezo wa yeye kujiamini na kupunguza kunyanyapaliwa," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Upasuaji Hospitali ya Aga Khan, Dk. Athar Ali, alisema wagonjwa wamekuwa wakiongezeka kila mwaka na kuamua kutoa huduma hiyo kwa awamu mbili kwa mwaka. "Gharama ya matibabu haya kwa mgonjwa mmoja ni zaidi ya Sh. milioni tano ila sisi tunafanya bure hivyo tunawaomba wananchi wajitokeze kwa wingi tunapotangaza kufanyika kwa upasuaji huu," alisema.

Kwa upande wake mwazilishi wa taasisi isiyokuwa ya kiserikali inayojishughulisha na masuala ya kijamii ya Sadaka, Dk. Ibrahim Msengi, alisema wao waliguswa na matatizo hayo yanayowakumba wanawake na kuamua kukusanya fedha kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kufanikisha zoezi hilo.

# NMB yatangazia bingo Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetangaza kuanza kutoa hati fungani ya asilimia 10 kwa watu wanaotaka kuwekeza na kupata faida, ambayo itadumu kwa muda wa miaka mitatu hadi Juni 2022.

Dirisha la hati fungani hiyo lilifunguliwa rasmi jana na litafungwa rasmi Julai 8, mwaka huu.

Mkuu wa Wateja Binafsi wa NMB, Omari Mtiga, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa katika hati fungani hizo ambazo zinatolewa kwa mara ya pili, mteja anayetaka kuwekeza atalipa kuanzisha Sh. 500,000 ambacho ni kiasi cha chini.

Alisema wawekezaji wa hati fungani hizo watajipatia riba nono ambayo itatolewa kwa asilimia 10 kwa mwaka na mhusika atalipwa riba hiyo kila baada ya miezi mitatu ya mwaka. "Misingi ya NMB ni uwekaji fedha wa wateja wadogo lakini kuna njia nyingi za kutunisha mfuko wetu. Kwa hati fungani ya NMB, tunategemea kutunisha mfuko wa benki kwa Sh. bilioni 25 na tuna fursa ya kuongeza hasi Sh. bilioni 40," alisema.

Mtiga pia alisema kutokana na matokeo ya hati fungani iliyopita ambayo muda wake unamalizika mwezi ujao, wawekezaji wengi wameonyesha nia ya kuwekeza, hivyo benki hiyo imechukulia kwa mtazamo chanya katika hati fungani mpya.

"Tunachukulia hii kama fursa muhimu katika kukidhi kiu ya wawekezaji wetu pamoja na uendelezaji wa mitaji ya masoko ya mitaji na njia mbalimbali za ukuzaji mitaji. Fursa hii itaturuhusu sisi kutafuta fedha zaidi ambazo zitasaidia kutoa mikopo mingi na nafuu kwa wateja," alisema Mtiga.

Alisema riba kwa ajili ya hati fungani hiyo itaanza kulimbikizwa mara tu mteja atakaponunua na kwamba huduma hizo zinapatikana katika matawi yote nchini, mawakala wa soko la hisa na mawakala wa NMB ambao wako maeneo mbalimbali.

Hati fungani ni aina ya uwekezaji ambayo mtu anawekeza katika taasisi hasa shirika la kibiashara au serikali kwa kuikopesha fedha kwa muda maalum na kwa riba isiyobadilika.

# JPM ataja sababu kumng'oa bosi TRA

**Inatoka uk 8**

"Kiwanda kama cha Mbeya cha nguo kinakwenda kubadilishwa kiwe cha pipi, hakiwezekani, tunaonekana tunakula pipi tu, zipo changamoto nyingi kashirikiane na wenzako kuzitatua," alisema.

Akigeukia kilichomwondoa Kichere, Rais Magufuli alisema Waziri Mpango amezungumza alivyokuwa pale Kamishna wa TRA, aliipandisha kutoka Sh. bilioni 850 hadi trilioni 1.3.

"Nikampandisha cheo kutoka TRA akawa Waziri wa Fedha, sasa wengine mnaokwenda mnasimamia hapo hapo kana kwamba ni fomula, lakini tatizo malalamiko ni mengi na hamchukui hatua, kama kuna ujumbe mfupi nimekutumia kamishna uliyeondoka yawekezana zinazidi 20 au 30 zingine nilikuwa natuma saa nane za usiku, nyingine saa tisa na nyingine saa kumi kwa sababu watu wanapolalamika ninamtumia na jamaa huyu ni kama diplomat (mwanadiplomasia) anasema nimepoka mheshimiwa,"

Aliongeza, "Ukifuatilia hakuna matokeo, ndiyo ukweli, mimi huwa sisahau ndiyo dhambi niliyonayo, haiwezekani mkurugenzi wako wa kukadiria anatoa makadirio ya kijinga kwa wafanyabiashara upo unamwangalia tu wakati una nguvu unashindwa kuitumia, unaona makusanyo ya kodi ya ndani yanashuka, labda huyu wa sasa imepanda kidogo, lakini hakuna hatua inayochukuliwa."

Rais alisema: "Unaona kuna wafanyabiashara wanapakia mizigo wanaiandika inakwenda Tunduma hadi nchi jirani, wakifika Tunduma wanagongewa mihuri wanarudi kuishusha hapa Dar barabara yote TRA, lori linatembea kilometa 1,300 linasema linakwenda nchi jirani wanachukua nyaraka wanagonga mpakani wanarudi, kama gharama mtu ameamua kusafirisha hadi Tunduma anarudi halafu amehonga za kugonga muhuri, zingejumlishwa zote angetelemsha mizigo yake hapa si mngemsaidia atumie mafuta vizuri.

Rais Magufuli alibainisha kuwa kuna mwekezaji alikuja na vifaa vyake anataka kuchimba dhahabu, lakini vimekaa zaidi ya mwaka alikuwa kiasi kidogo akaongezewa zaidi.

"Badala ya kuangalia huyu atawekeza hiki atatoa ajira na serikali itapata mapato kutoka kwenye dhahabu, utafikiri TRA wote hawakusoma, ndiyo maana nikasema siwezi, ndio maana siku ile walivyokusema nakuuliza unasema hujui unamwangalia mtu wa nyuma yako utamwangalia mpaka lini ukikuta hawapo, nafuu utoke na wewe hapo hapo," alisema.



Rais Magufuli alimwambia Kichere kuwa amempeleka Njombe akajaribu ukatibu tawala na endapo akiusimamia vibaya atamtoa.

Aliwambia kuwa kuna watu wamebobea pale TRA na kumtaka akawakamate ili kodi ipatikane.

"Hakuna nchi duniani iliyoendelea bila kodi, niache kuwalipa mishahara si nitawakuta Ikulu wamesimama, usicheke na mtu, ni sawa na useme usiende mbinguni tutakuombea wote tunaofaidi utakwenda kwa nguvu tutakusukumiza Watanzania wote milioni 55 uingie mbinguni," alisema.

Pia alimtaka akashirikiane na wafanyabiashara ili wampe taarifa nyingi na wale walioghushi siku za nyuma kutokana na mazingira akakae nao waseme wanaweza kulipa kiasi gani, kwa sababu anayo mamlaka ya kusamehe asilimia fulani.

Kuhusu watumishi wanaokwenda kwa wafanyabiashara kuwapa makadirio makubwa na kusema wametumwa juu, amemtaka asiogope kuwafukuza, awashike na kuwapeleka mahakamani.

"Kama unawafanyakazi 1000, halafu 200 wakaishia kufukuzwa na kwenda mahakamani sawa tu, lakini ukiwa mtaratibu watakukaribisha na siku ukiingia ofisini watakuletea au karibu wote watakuita bosi hata kama naye ni bosi achana na sherehe, jana nimekutumia ujumbe wa mtu analalamika, kabla sijakuapisha," alisema.

Alisema kuna makamishna wa TRA katika mipaka, ambapo mpaka wa Rusumu unafanya vizuri lakini Tunduma na Sirari hakufai.

**GAWIO LA AIRTEL**

Kuhusu fedha za gawio Rais Magufuli ametaka Sh. bilioni moja zilizotolewa ziende kujenga hospitali Dodoma.

Alisema mazungumzo kati ya serikali na Airtel yamechukua mwaka mzima na kwamba wapo waliodhihaki, waliocheka, waliojua haitawekezana lakini wote walioyatakia mabaya Mungu amewaumbua.

"Fedha zitakazokuwa zinalipwa na Airtel Sh. bilioni moja kila mwezi, kwa mwaka itakuwa ni Sh. bilioni 12 na kwa miaka mitano ni Sh. bilioni 60 tutajenga vituo vya afya kwa Sh. milioni 500 maana yake tutakuwa na vituo 120, ukijenga vya Sh. milioni 400 maana yake ni vituo 150.

Rais Magufuli alisema licha ya kwamba serikali ina asilimia 40, lakini kwa miaka 19 serikali haijapata gawio lake kutoka kwenye kampuni hiyo zaidi ya kubambikwa deni la trilioni moja ambalo limeondolewa baada ya mazungumzo hayo.

"Nampongeza mwenyekiti Airtel pamoja na kwamba ametoka India, lakini ana moyo wa kitanzania, kwa kusikiliza ushauri wa wengine, nilijua angeweza kwenda kwenye mahakama ya usuluhushi, lakini alisikiliza, hata hivyo, nilijiandaa kwenye hili," alisema.

Kuhusu uteuzi wa mwenyekiti kwenye kampuni hiyo, Rais Magufuli alisema ameshapatikana na wajumbe wale waliokuwa kwenye timu ya mazungumzo watakaokuwa hao hao kwa sababu wameonyesha uzalendo.

WAZIRI KABUDI

Awali, mwenyekiti wa mazungumzo baina ya serikali na kampuni ya Airtel, Prof. Kabudi, alisema Bharti imefuta deni na madeni mengine ya Airtel kiasi cha dola zaidi ya dola milioni 407.38 (sawa na Sh. bilioni 937), hivyo imeokoa Sh. bilioni 459.13 ambazo zingelipwa na serikali kama mwanahisa.

Mwanzilishi na Mwenyekiti Mtendaji wa Bharti Airtel Mittal alisema baada ya mazungumzo hayo kampuni hiyo inaanza upya na kwamba ipo tayari kushirikana na serikali.

Waziri Bashungwa aliahidi kuanza na Blue Print ili kuondokana na changamoto zinazowakabili wafanyabiashara.

Kichere alimshukuru Rais Magufuli kwa kuendelea kumwamini na kuahidi atakwenda kutekeleza majukumu mapya aliyompatia.

Kamishna Mkuu TRA, Dk. Mhede alisema hawezi kuogopa ilhali kazi aliyopewa inaenda kuamua maisha ya Watanzania milioni 55.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NYUMBA /VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA DODOMA IRINGA RD KARIBU NA KITUO KIKUU CHA POLISI KIWANJA 1680sqm simu 0659 755 011

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311



## KUPOTEA KWA CHETI



**Neema Elias** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0216-0079** kilichotolewa na Baraza Mithihani la Taifa mwaka 1997 katika shule ya Sekondari Ngaza . Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **CD/RB/9539/2000**

215266802

## KUPOTEA KWA CHETI




**KELVIN ERNEST** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE NAMBA **CS130400040** CHENYE INDEX NAMBA **S0313-0128** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TAIFA MWAKA 2013 KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKIZU.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI MBI/RB/40/2019**

215267102

## KUPOTEA KWA CHETI



**KELVIN ERNEST** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA SITA NAMBA **ACS 063478** CHENYE INDEX NAMBA **S0752-0580** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TAIFA MWAKA 2016 KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU..

**TAARIFA YA POLISI MBI/RB/40/2019**

215267102

## GOROFA INAUZWA



BOKO KAMWANGA STR
LOW DENSITY AREA
BLOC "C",
PLOT NO. 65

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**RUFAA/MADAI NO. 17/2019**

**Katika Mahakama ya Wilaya Dodoma**

**Shauri la Rufaa/madai No. 109/2019**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya Chamwino Mjini … Manager wa Benki NMB Mrufani**

**Dhidi ya**

**Labia Helena Mussa**

**Kwa Labia Helena Mussa**

Kwa kuwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakam iliyotajwa hapo juu siku ya juma tano tarehe 12/06/2019 unatakiwa uhudhurie katika Mhakama hiyo Mrufaniwa pamoja na vilelezo vyote kama vipo.

Hati hii imetolewa na amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 30/5/2019

…………………………………..

**sahihi ya hakimu**

215266202

# ILANI

**FRIGORIFICO VICTORIA LIMITED**

Inatolewa ilani kwa watu wote kwamba kampuni tajwa hapo juu iko mbion kufutwa kwa ridhaa yetu.

Wanahisa

215267202


*Uza, Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223 311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO



# MAJALIWA YA NEYMAR PSG SHAKANI ZAIDI

**PARIS, Ufaransa**

MAJALIWA ya Neymar pale Paris Saint-Germain yameendelea kubakia kwenye sintofahamu, baada ya Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Antero Henrique kutarajiwa kuondoka kikosini hapo.

Mkurugenzi huyo ambaye anatajwa kuwa mshawishi mkubwa wa Neymar, anaondoka na nafasi yake inachukuliwa na Leonardo.

Raia huyo wa Brazil ambaye alijiunga na timu hiyo misimu miwili iliyopita kwa ada iliyoweka rekodi akitokea Barcelona, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka.

Na sasa mtu wa karibu zaidi na Neymar, Henrique, ambaye ndiye aliyehusika kumshawishi kujiunga na klabu hiyo anaondoka na kuna uwezekano mkubwa nyota huyo naye akaamua kumfuata.

Gazeti la Ufaransa la Telefoot, limedai kwamba, wakati Henrique anaondoka Leonardo anarudi kuchukua mikoba yake na hivyo kuna uwezekano mkubwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 naye akasepa.

Klabu ya Real Madrid imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Neymar, lakini klabu yake ya zamani ya Barcelona nayo inatajwa kutaka kumrejesha mchezaji huyo.

Wakati Leonardo anarudi kuchukua mikoba ya ukurugenzi kwenye klabu hiyo, ambayo aliondoka miaka sita iliyopita, jukumu lake la kwanza litakuwa ni kumshawishi mchezaji huyo kubaki.

Lakini taarifa kutoka viunga vya pale Parc des Princes, zinasema kwamba, Henrique ndiye mtu ambaye alikuwa akimudu kumshawishi Neymar kwa jambo lolote na sasa kuna uwezekano mkubwa na yeye akaondoka.



# VAN DIJK AAMINI UHOLANZI KUIMARIKA

**LISBON, Ureno**

VIRGIL van Dijk anaamini kwamba Uholanzi itaendelea kuimarika zaidi kiuchezaji licha ya kufungwa kwenye fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya na Ureno.

Bao la Goncalo Guedes liliwawezesha Ureno kupata ushindi wa 1-0 katika Uwanja wa Dragao juzi Jumapili, na hivyo kuwaongezea taji la pili kubwa la kimataifa ndani ya miaka mitatu, baada ya kushinda Kombe la Euro 2016.

Uholanzi maarufu kama Orange ilishindwa kufuzu kwa michuano hiyo na pamoja ile ya Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi.

Hata hivyo, baada ya Uholanzi kushinda kwenye hatua ya makundi ambapo walikuwa kundi moja pamoja na Ujerumani na Ufaransa, Van Dijk anaona kwamba kikosi hicho cha kocha, Ronald Koeman kimeonyesha ishara nzuri zaidi kuelekea kwenye michuano ya Euro 2020.

"Hii haitatufanya tukate tamaa," alisema beki huyo wa Klabu ya Liverpool akiiambia televisheni ya NOS baada ya mchezo huo.

"Tunajipanga zaidi kuhakikisha kwamba, timu inaimarika na kuendelea kufanya vizuri na tunatakiwa kuendelea kufanya hivyo. Tunatakiwa kujivunia sisi wenyewe kwa kiwango tulichofikia kwa sasa."

Aliongeza kusema: "Ni kweli kwamba matokeo haya yametukatisha tamaa kwa sababu tulitaka kushinda fainali, lakini tumefungwa. Nawapongeza Ureno kwamba walikuwa na bahati na bila shaka walistahili ushindi ule."

# De Ligt: Ronaldo kaniomba nimfuate tukacheze Juve

**LISBON, Ureno**

NYOTA wa Klabu ya Ajax na timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt amebainisha kwamba, Cristiano Ronaldo alimuomba ajiunge na Juventus kwa ajili ya msimu ujao.

De Ligt mwenye umri wa miaka 19, anatarajiwa kununuliwa kwa fedha nyingi kutoka pale Ajax kipindi hiki cha majira ya joto, huku Paris Saint-Germain na Barcelona zikitajwa kumuwania mchezaji huyo.

Lakini nyota wa Juve, Ronaldo hakusita kujaribu kumuomba beki huyo kujiunga na miamba hao wa Turin baada ya Ureno kuifunga Uholanzi bao 1-0 kwenye fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya juzi Jumapili.

Alipoulizwa kama Ronaldo alimuomba kujiunga na Juventus, De Ligt aliiambia Televisheni ya NOS: "Ndio. Hilo ni kweli kabisa.

"Sikumuelewa kwa mara ya kwanza. Nilishtuka, hivyo nikacheka, lakini sikujibu chochote.

"Muda mfupi baada ya mchezo huwezi kufikiria hilo, unakuwa na mawazo ya kupoteza mchezo na hicho ndicho nilichokuwa nakifikiria kwa wakati ule."

Klabu za Manchester United na Liverpool pia zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili beki huyo wa kati ambaye alikuwa na msimu mzuri wa 2018-19 na Ajax ambayo ilifika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# MOURINHO

## ATAJWA KUINOA NEWCASTLE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho anatajwa huenda akachukua mikoba ya kuwa kocha wa Klabu ya Newcastle United, huku Rafa Benitez akiwa bado hajaongeza mkataba wake wa kubakia hapo.

Kumekuwa na uvumi mwingi tangu Sheikh Khaled bin Zayed Al Nehayan kutangaza kwamba ana mipango ya kuinunua klabu hiyo ya pale Magpies wiki chache zilizopita.


Gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba, Sheikh Khaled anataka kukiimarisha kikosi hicho kwa kutafuta kocha bora ambaye atakijenga upya kikosi hicho kiwe cha ushindani.

Wakati hatima ya kocha wa sasa wa Newcastle, Benitez ikionekana kufikia mwisho, Mourinho ndiye anayetajwa kuwa mtu sahihi wa kuchukua mikoba yake.

Mourinho kocha wa zamani wa Klabu za Chelsea, Real Madrid na Manchester United amekuwa hana kazi tangu alipotimuliwa kule Old Trafford Desemba mwaka jana.

Taarifa zaidi za Sky Sports zimemnukuu mtu wa karibu na Mourinho kwamba raia huyo wa Ureno yupo tayari kuchukua mikoba ya kuinoa Newcastle United na kurudi tena kwenye Ligi Kuu ya England.

Gazeti la The Mirror limedai kwamba, tayari wawakilishi wa Mourinho wamekutana na Sheikh Khaled kwa ajili ya kumshawishi kocha huyo 'anayeongea sana' ili apewe nafasi hiyo.





## Griezmann sasa mguu na njia PSG

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, ameripotiwa kwamba anajiunga na Paris Saint-Germain kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kukataa ofa ya Barcelona.

Gazeti la Marca limedai kwamba, Griezmann anahofia kwamba, hatakiwi na kikosi hicho cha pale Camp Nou.

Raia huyo wa Ufaransa amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu kujiunga na Barcelona na msimu uliopita alikataa katika dakika za mwisho.

Lakini sasa Griezmann anatajwa kwamba ameshafikia makubaliano na Barcelona baada ya kutangaza mwishoni mwa msimu huu kuwa anaondoka Atletico Madrid na kwenda kutafuta changamoto mpya.

Lakini taarifa za sasa kwa mujibu wa Sky Sports zinasema kwamba, Klabu ya PSG ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa.

Griezmann mwenyewe anadaiwa kwamba ana hofu ya kujiunga na Kikosi cha Barcelona kwa sababu anaonekana kutopendwa na mashabiki wa klabu hiyo.

Aidha, Griezmann ameripotiwa kwamba tayari amekutana na Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi kwa ajili ya kufikia makubaliano ya kutua hapo kchukua nafasi ya Edinson Cavani.

## Rooney atoa ushauri usajili Man United




**MNCHESTER, England**

MFUNGAJI mwenye rekodi kubwa Manchester United, Wayne Rooney amemshauri kocha wa pale Old Trafford, Ole Gunnar Solskjaer kusajili wachezaji vijana zaidi kuliko kukimbilia majina makubwa.

Man United kwa sasa inahusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Gareth Bale kutoka pale Real Madrid na Rooney anaona kwamba hayo ni matumizi mabaya ya fedha.

Pamoja na Bale, Man United pia inahusishwa pia na mpango wa kumsajili beki wa kati Matthijs De Ligt na nyota wa Benfica, Joao Felix, Kalidou Koulibaly na Thomas Meunier.

Lakini, Rooney amemwambia kocha Solskjaer pauni milioni 100 ambazo zinatajwa kwamba atazitumia katika kusajili wachezaji, azielekeze kwenye kusajili wachezaji vijana zaidi.

"Siamini katika kusajili mchezaji mmoja mkubwa kwa pauni milioni 100, kwa sasa Man United inatakiwa kusajili wachezaji vijana kwa ajili ya kukijenga kikosi hicho," alisema Rooney akinukuliwa na Sky Sport.

"Sidhani kama kusajili mchezaji mmoja au wawili kwa fedha nyingi zaidi ya pauni milioni 100 ndiyo kutasaidia kikosi kwa wachezaji waliopo hapo kwa sasa.


"Naamini Ole anahitaji kusajili wachezaji kama watano au sita wenye vipaji na vijana, ambao baadaye watakuwa wachezaji wakubwa. Sio wachezaji wa kutumia pauni milioni 120 au pauni mlioni 130.

"Nadhani asajili tu wachezaji wa pauni milioni 30, pauni milioni 40, ambao watawakuza na kuwa muhimu kwenye timu. Unahitaji kujenga kikosi cha wachezaji watano au sita hivi, ukijumlisha na wachache waliopo inakuwa sawa.

"Sawa unaweza kuwasajili Ronaldo, Sergio Ramos na Messi au Bale kwa mfano, lakini hapo utakuwa umetumia pauni milioni 300."

Man United imeripotiwa kukaribia kumnasa winga wa Swansea, Daniel James kwa pauni milioni 18, huku ikiwapigia hesabu Harry Maguire, Aaron Wan-Bissaka, Patrick van Aanholt, Toby Alderweireld kwa pesa kiduchu, huku ikipanga kuwapiga bei Romelu Lukaku, Alexis Sanchez na Paul Pogba.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO: LA LIGI TAYARI, BADO TAJI LA EURO 2020

Ninataka kuwa sehemu ya mradi huu kwa sababu ninajisikia vizuri na najisikia kuwa tayari...

**Lisbon, Ureno**

Cristiano Ronaldo amefunguka nia yake ya kupania kuiongoza Ureno kutwaa ubingwa mwingine baada ya kuibebesha Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya kwa kuifunga Uholanzi katika mechi ya fainali juzi, Jumapili.

Mshambuliaji huyo wa Juventus amekuwa kinara wa ufungaji kwenye michuano hiyo ya fainali za Ligi ya Mataifa ya Ulaya shukrani kwa hat-trick yake aliyotupia katika mechi ya nusu fainali dhidi ya Uswisi.

Na kisha akaisaidia nchi yake kuifunga Uholanzi kwa bao 1-0 juzi Jumapili, wakati Goncalo Guedes alipofunga bao hilo pekee lililowapa ubingwa wa michuano hiyo.

Na Ronaldo, 34, analenga kuendelea kuitumikia Ureno kwa kadri timu hiyo itakavyokuwa ikiendelea kushiriki michuano mbalimbali, wakati kutetea ubingwa wa fainali za Euro 2020 likiwa ndilo lengo la nahodha huyo lijalo, baada ya kuutwaa miaka mitatu iliyopita nchini Ufaransa.

Alisema: "Timu ya taifa itaendelea, ikiwa ama bila Cristiano. Nadhani timu ina uwezo mkubwa. Kuna wachezaji vijana, wachezaji ambao kwa miaka ijayo watakomaa zaidi na kuwa bora.

"Ninataka kuwa sehemu ya mradi huu kwa sababu ninajisikia vizuri na najisikia kuwa tayari kuisaidia timu ya taifa."

Ronaldo pia aliiambia Uefa.com: "Nadhani timu ya taifa ina uwezo mkubwa wa kuendelea kushiriki na kushinda makombe."

Akiwa na mabao 88 katika mechi 158 alizoichezea nchi yake, ndiye mfungaji bora katika histori ya wafungaji bora kwenye timu za taifa Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid alisema kutwaa medali ya mshindi kutoka kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya kumemfanya kuridhika sana.

"Furaha kubwa!" Alisema. "Ilikuwa vizuri sana, nina furaha sana. Kuweza kutwaa kombe hili hapa Ureno mbele ya watu wa Ureno, kwangu mimi hii ni heshima kubwa."

## KWA UFUPI

### DE GEA KUONDOKA NA KITITA
Manchester United itampa kipa Mhispania David de Gea, 28, pauni milioni 20 ataondoka na kujiunga na Paris St-Germain majira haya ya joto. ***(Sun)***

### UNITED YAGOMEWA WAN-BISSAKA
Crystal Palace imeikatalia Manchester United ofa yake ya pauni milioni 40 kwa beki wa England U-21, Aaron Wan-Bissaka. 'The Eagles' hao wanataka takribani pauni milioni 60 ili kumwachia. ***(Sky Sports)***

### FELIX ATAONDOKA BENFICA- RAIS
RAIS wa Benfica, Luis Filipe Vieira amefunguka kuwa Joao Felix, 19, anaweza kuondoka majira haya ya joto huku kukiwa na taarifa zinazomhusishwa na Manchester United. ***(Metro)***

### EMERY, MEUNIER WATETA
KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amefanya mazungumzo na beki wa kulia wa PSG na Ubelgiji, Thomas Meunier, 27, kuhusu uwezekano wa kumsajili majira haya ya joto. ***(Express)***

### SILVA KUAGWA CITY MWAKANI
KIUNGO wa Manchester City, David Silva, 33, ataandaliwa mechi ya kuagwa katika Uwanja wa Etihad mwaka ujao. Kiungo huyo wa Hispania mkataba wake unamalizika mwaka ujao na anataka kustaafia Las Palmas alipozaliwa, Gran Canaria. ***(Sun)***

### SESSEGNON ATARAJIWA SPURS
Tottenham itatoa ofa kwa winga wa Fulham na England U-21, Ryan Sessegnon, 19, majira haya ya joto. ***(Football.London)***

### RONALDO AMVUTA DE LIGT JUVE
BEKI wa Ajax na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 19, amesema Cristiano Ronaldo amemuuliza kama atajiunga naye Juventus msimu ujao kufuatia Ureno kutwaa Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Uholanzi. ***(NOS - via Goal.com)***

### ARSENAL YAVUTIWA NA VERETOUT
Arsenal inavutiwa na kiungo wa Fiorentina, Jordan Veretout, 26, lakini nyota huyo wa zamani wa Ufaransa U-21, tayari yupo katika mazungumzo na Napoli. ***(L'Equipe - in French)***

### CHELSEA YAMRUDIA BAILEY
Chelsea imerejea tena mpango wake wa kutaka kumsajili winga wa Bayer Leverkusen na Jamaica, Leon Bailey, 21, lakini italazimika kusubiri kuona kama itafanikiwa kushinda sakata lake la kufungiwa kusajili. ***(Mail)***

### ERIKSEN KUMRITHI POGBA
Manchester United imeanza kuandaa orodha ya wachezaji wanaoweza kurithi viatu vya Paul Pogba, 26. Kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, 27, na wa Monaco, Youri Tielemans, 22, wanapewa nafasi ya kusajiliwa endapo Mfaransa huyo ataondoka. ***(Standard)***

### SALIBA AWINDWA ARSENAL
Arsenal inataka kumsajili beki wa Saint Etienne, Mfaransa William Saliba, 18, lakini klabu hiyo ya Ligue 1 itahitaji kumtoa kwa mkopo ili kumrejesha msimu ujao. ***(Football.London)***

### LAMPARD ALENGWA KUINOA CHELSEA
Chelsea inatumai kocha wa Derby, Frank Lampard atakuwa kocha wao ajaye. ***(Mirror)***

### MATETA LULU NEWCASTLE
Newcastle na Southampton zimetoa ofa kwa mshambuliaji wa Mainz na Ufaransa U-21, Jean-Philippe Mateta, 21. ***(L'Equipe, via Sport Witness)***

### KESSIE VITANI WEST HAM, SPURS
West Ham inajiandaa kuingia vitani na Arsenal pamoja na Tottenham katika kuisaka saini ya kiungo wa Atalanta na Ivory Coast, Franck Kessie. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa akicheza kwa mkopo AC Milan tangu mwaka 2017. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA, KMC VITANI KWA MATOLA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yao kupanda daraja la kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Polisi Tanzania umeacha mchakato wa kuboresha benchi lake la ufundi na limeanza kwa kumwania Kocha wa Lipuli FC, Selemani Matola, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinaeleza kuwa tayari uongozi wa Maafande hao wa Jeshi la Polisi wameshafanya mazungumzo ya awali na Matola na sasa wanasubiri majibu kutoka kwa kiungo huyo wa zamani wa Simba.

Chanzo chetu kiliendelea kueleza kuwa Matola aliwataka viongozi wa Polisi Tanzania wasiwe na wasiwasi kutokana na maombi yao na kuwaambia atawapa jibu baada ya kupitia ofa wanazotarajia kumpa endapo atakubali kusaini mkataba wa kujiunga na timu hiyo.

"Ni kweli nimefuatwa na KMC, na sasa Polisi Tanzania, lakini bado sijafanya uamuzi kuhusu wapi nitafanya nao kazi," alisema kwa kifupi Matola.

Kocha huyo aliongeza kuwa pia anaendelea na mazungumzo dhidi ya mabosi wake wa Lipuli FC, ili asaini mkataba mpya wa kuendelea kuifundisha klabu hiyo ya Iringa.

"Hata Lipuli pia tunaendelea kuwasiliana na kuna baadhi ya majukumu bado yanafanyiwa kazi kwa kufuata mapendekezo yangu," Matola alisema.

Naye Ofisa Habari wa Lipuli, Clement Sanga, amesema kuwa baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita kumalizika pamoja na mechi ya fainali ya Kombe la FA, walimpa mapumziko kocha huyo pamoja na wachezaji, hivyo watatoa msimamo kuhusu hatima yake, likizo itakapomalizika.

Mbali na kucheza fainali ya FA kwa mara ya kwanza, Matola aliisaidia Lipuli kumaliza ligi ikiwa katika nafasi ya sita kwenye msimamo.

BAO




Claire Emslie akiifungia Scotland bao la kufutia machozi dakika ya 12 kabla ya mechi kumalizika, wakati England ikishinda 2-1 kwenye mchezo huo wa fainali za Kombe la Dunia wa Kundi D uliopigwa juzi katika Uwanja wa Allianz Riviera, Ufaransa. **PICHA: DAIL MAIL**

## Vodacom kurusha mashabiki Afcon Misri

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA msimu wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania (PLC), imezindua Kampeni ya Data na Afcon kupitia huduma ya "Soka Letu" na itawazawadia wateja wake 10 tiketi za kwenda kushuhudia timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ikicheza huko Misri.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika ofisi za makao makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Biashara wa Vodacom, Linda Riwa, alisema huu ni wakati wa kusapoti vya nyumbani na kwamba kampeni hiyo itaendeshwa nchi nzima ili kutoa fursa kwa kila Mtanzania na shabiki wa Taifa Stars kushinda tiketi ya kwenda kuishangilia.

"Tunafuraha kubwa kuona timu yetu ya taifa imefuzu kuwania Kombe hili la Afcon, na tunasambaza furaha yetu kwa wateja wetu. Kama mnavyojua kwa takriban miaka 39 haikupata fursa ya kuwania mashindano haya, hivyo inabidi tuipe nguvu na kuishabikia.

"Kupitia huduma ya 'Soka Letu' kutoka Vodacom Tanzania, tutawazawadia wateja wetu 10 ambao ni mashabiki wa Taifa Stars tiketi za ndege pamoja na malazi huko Misri, ili wakaishangilie timu yetu ya taifa," Riwa alisema.

Alisema kampeni hiyo ilianza rasmi siku hiyo (Juni 7) na itafungwa Juni 21, mwaka huu, ambapo washindi watatangazwa.

"Kuna zawadi kemkem katika msimu huu wa Kombe la Mataifa ya Africa kupitia Data na Afcon, hivyo ili ushinde inabidi ujiunge na huduma ya 'Soka Letu' kwa kubonyeza *149*84# na utapokea jumbe mbalimbali kuhusiana na mechi zinazoendelea.

"Na si hayo tu, kutazama mechi mubashara unahitaji kuwa na intaneti ya uhakika, hivyo endelea kujiunga na vifurushi vya intaneti upate hadi mara mbili ya kifurushi unachonunua 'Data Datani'," aliongeza Riwa.

Alifafanua kuwa kwa wateja wapya, watapata dakika tano bure za kupiga papo hapo, lakini pia wateja wote wanaweza kujishindia dakika 10,000 za kupiga kutoka Vodacom Tanzania PLC, na pia watapata nafasi ya kujibu maswali na kujishindia pointi nyingi zaidi, ambazo zitawawezesha kuingia katika droo ambayo washindi watapata tiketi za kwenda Misri, huku gharama zote zikiwa zimelipiwa na kampuni hiyo.

Kwa upande wa baadhi ya mashabiki wa Taifa Stars, Juma Hamisi wa Mbagala na Christian John wa Mwenge, waliipongeza Vodacom Tanzania kwa kuwa wadau wakubwa wa soka nchini. "Tunafurahi sana kuona Vodacom wakitusapoti kwa hili, nina imani washindi watakaopatikana wataongeza ushabiki kule Misri na kututia nguvu ya kufanya vizuri katika msimu huu," alisema Hamisi.

## Gharama kuishuhudia Stars Afcon hizi hapa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameendelea kuwahamasisha wabunge kwenda Misri kushuhudia fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, huku akiweka wazi gharama zake kuwa ni Dola za Marekani 1490 (sawa na Sh. milioni 3.4) kwa kila mmoja kwa siku 10.

**Fainali hizo zinatarajiwa kuanza Juni 21, huku timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' iliyopangwa Kundi C ikianza kusaka nafasi ya kutinga robo fainali kwa kucheza dhidi ya Senegal Juni 23, na kisha kuivaa Kenya siku nne baadaye kabla ya Julai Mosi, mwaka huu kumaliza mechi za hatua ya makundi kwa kuvaana na Algeria.**

Akitoa matangazo bungeni jijini Dodoma jana, Spika Ndugai alisema gharama za safari zinategemea na chaguo la mbunge kama anataka kwenda awamu zote mbili au moja.

"Awamu ya kwanza ambayo ni siku nne ni Dola za Marekani 720, hii ni pamoja na usafiri na mambo mengine hadi kupelekwa uwanjani kutoka hotelini.

"Awamu ya pili ni siku sita ambayo ni Dola za Marekani 770, hivyo ukitaka kwenda zote mbili ni zaidi ya Dola za Marekani 1400," Spika Ndugai alisema.

Aliongeza kuwa wabunge wanaweza kushiriki awamu moja wapo na kuwataka kujiandikisha na kulipia mapema.

"Tujiandikishe mapema ili tuweze kwenda kushuhudia timu yetu kwenye fainali hizi, hawa wa awamu ya kwanza wa siku nne na mimi nitalipia nitaenda.

"Tunaweza kuwa pamoja, naomba tuunge mkono timu yetu, ni miaka mingi sana hatujafika Afcon," Ndugai alisisitiza.

Alibainisha kuwa wachezaji wakicheza huku wakiona wabunge wao huko Misri wakiwaunga mkono, watapata nguvu zaidi.

Tanzania ilifuzu kwa mara ya kwanza kushiriki mashindano hayo makubwa mwaka 1980 na baada hapo haikufanikiwa tena kushiriki.


Michezo
Jumanne Juni 11, 2019
Nipashe



## Mourinho atajwa kuinoa Newcastle

HABARI UK 29

MWAKA WETU...



Nahodha wa Ureno, Cristiano Ronaldo, akisherehekea na wachezaji wenzake kwa kunyanyua juu Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya baada ya kulitwaa kwa kuifunga Uholanzi bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Estadio Dragao juzi. **HABARI UK. 30**

# AJIBU AINYIMA USINGIZI YANGA

●●●Yamweka kitako kisa mkataba Simba, atoa matumaini akiitaka...

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Yanga ya jijini Dar es Salaam umesema bado unahitaji huduma ya nahodha na mshambuliaji wao, Ibrahim Ajibu, ambaye anatajwa kusaini mkataba wa awali na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, imefahamika.

Taarifa katika mitandao mbalimbali ya kijamii jana zilieleza kuwa Ajibu amesaini mkataba mpya wa miaka miwili, jambo ambalo si kweli.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa juu (jina tunalihifadhi), alisema bado mshambuliaji huyo hajasaini mkataba mpya na wanaendelea kumshawishi ili akubali kubakia katika klabu hiyo.

Kiongozi huyo alisema wameshafanya vikao mbalimbali na mshambuliaji huyo, lakini hawakufanikiwa kukamilisha mazungumzo ya kusaini mkataba mpya.

"Tunamhitaji sana, ni mchezaji ambaye mchango wake kwetu ni muhimu, tulimfuata kambini Stars Whitesands, tukazungumza naye tukiwa viongozi watatu, lakini hatukumaliza mchakato huo uliotupeleka," kilieleza chanzo chetu.

Aliongeza kuwa mara zote, Ajibu ambaye ametemwa katika kikosi cha Taifa Stars kilichokwenda kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) amekuwa akiwaambia mabosi wa Yanga wasiwe na wasiwasi, atasaini mkataba mpya muda ukifika.

"Kila tukiongea naye (Ajibu), anatupa matumaini, anatuambia hatuwezi kushindwana mabosi wangu," aliongeza kwa kifupi kiongozi huyo.

MUSONYE AWAPONDA

Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, ameziponda klabu za Simba na Yanga kwa uamuzi wao wa kujitoa katika mashindano ya Kombe la Kagame ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 7 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

Musonye alisema klabu hizo zinapoteza fursa ya kujiimarisha kuelekea msimu mpya, na hiyo kuzifanya zishindwe kufika mbali katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

"Viongozi wao ni bure kabisa, timu maana yake ni kushiriki mashindano, huwezi kuwa imara kama huchezi, hushindani, au hujiandai vema," alisema Musonye.

Licha ya kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu, Yanga itashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Simba baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kuipa Tanzania Bara nafasi nne katika mashindano yake ya msimu ujao.

## Siri Stars kutoboa Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

KUJITUMA na umakini ni moja ya vitu muhimu vinavyohitajika ili timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), iweze kufanya vema katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon)2019, zinazotarajiwa kufanyika kuanza Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu nchini Misri, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiungo wa timu hiyo, Himid Mao, alisema kuwa ili waweze kupata matokeo mazuri na kusonga mbele katika fainali hizo, wanatakiwa "kujitoa kwa kiwango cha juu" na si vinginevyo.

Mao, ambaye aliungana na kikosi hicho huko huko Misri anakoitumikia Klabu ya Petrojet, alisema kuwa wachezaji wote walioko Cairo wanaendelea vema na programu ya mazoezi na wanaendelea kujifunza mbinu mbalimbali kuelekea mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

**"Wachezaji wote wana ari, wana morali, tunajituma vizuri, ...tunajua hii ni michuano mikubwa, nchi yetu haijashiriki kwa muda mrefu, tunatakiwa tuhakikishe tunapigana tutoe jasho na damu ili kupata matokeo mazuri," alisema kiungo huyo wa zamani wa Azam FC.**

Kikosi cha Stars kinafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Olimpiki na kabla ya kuanza kwa fainali hizo, kitacheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya Misri itakayochezwa Alhamisi mjini Alexandria na nyingine dhidi ya Zimbabwe watakayovaana Juni 16, mwaka huu.

Stars ambayo iko Kundi C itacheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Segenal Juni 23, halafu itakutana na Kenya (Juni 27) na itamaliza hatua ya makundi Julai Mosi kwa kupambana na Algeria.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >